Kikao cha Tatu – Tarehe 17 Oktoba, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria (Kny: Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao Mengine ya Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya Mwenyekiti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji Karafuu na Mazao Mengine ya Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 15

Ujenzi wa Vyoo Manispaa ya Zanzibar

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Katika kuweka mazingira safi ya Manispaa ya Zanzibar hasa katika zile sehemu zinazoingia wageni wengi, sehemu hizi zinakabiliwa na tatizo la vyoo jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi na wageni hao.
Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka huduma hiyo.

Mhe. Waziri Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua umuhimu wa kuwa na vyoo katika maeneo mbali mbali na hasa yale yenye mkusanyiko wa watu. Katika kulitekeleza hilo Serikali imeweza kujenga vyoo katika sehemu mbali mbali za mji. Kati ya vyoo vilivyojengwa kwa nyakati tofauti tayari vyoo sita vinaendelea kutoa huduma navyo ni kile choo cha Darajani kituo cha daladala, soko la Mwanakwerekwe, soko la Darajani, Bustani ya Forodhani, Malindi madagaa na soko la Malindi; na vyoo ambavyo vinaendelea kufanyiwa matengenezo ili vipate kutoa huduma ni choo cha *African House*, *Wireless* Kikwajuni, Majestic, Kinazini, Mnazi Mmoja Hospitali, Mnazi Mmoja Uwanjani na P.W.D.

Mhe. Naibu Spika, kadri Baraza la Manispaa litakapoona kuna haja ya kujenga choo kwenye mkusanyiko wa watu wengi, basi serikali haitoacha mara moja kufanya shughuli hiyo. Lakini naomba niongezee Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali imefungua milango kwa suala la ukusanyaji taka au la usafishaji mji na tayari wenzetu wa Wilaya ya Magharibi kazi hiyo wameianza. Kwa hivyo, bado serikali inatoa wito kila mwenye uwezo kutusaidia katika suala hili la usafishaji mji au hata kujenga vyoo ni jambo la kawaida tu katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea kujenga vyoo ukalipa senti kidogo ambapo vyoo hivyo vinatunzwa vizuri sana kwa kuweza kufanya haja yako. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kufika salama. Naomba nimuulize Mhe. Waziri je, atakubaliana na mimi kwamba sasa hivi lazima tubadilike kutokana na mji wetu ulivyokuwa ili kuhakikisha kwamba kuna haja ya kuongeza tena vyoo kwani ni aibu mji wetu. Na hivyo vyoo anavyovizungumza Mhe. Waziri kwa kweli mimi mwenyewe nilitembelea haviridhishi hata kidogo hivyo, atakubaliana na mimi kwamba ni bora wakatangaza Manispaa kama kuna mtu ambaye ataweza kujenga vyoo vya kulipia.

Mhe. Waziri Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba vyoo vilivyopo havitoshi kwa kweli hivi vyoo vilivyopo sisi tokea tupo wadogo nakumbuka kama Rahaleo, Kinazini, Mnazi Mmoja vyoo vile tokea Unguja tupo watu 300,000, na leo tupo milioni 1.2. Kwa hivyo, nakubaliana na yeye kabisa harakati zimezidi, shughuli za biashara mjini zimezidi, watu wengi wanakula nje na ukishakula tena lazima uende uani kidogo. Kwa hivyo, hili nakubaliana na yeye na kama nilivyosema serikali kwa kweli imefungua milango kwa shughuli za kusaidiana na *private sector* kwa kusafisha mji ikiwemo ujengaji wa vyoo. Mhe. Naibu Spika, hilo ni jambo la kawaida kwenye miji mikubwa kwa hiyo tunakukaribisha Mhe. Asha kama unaye mtu yeyote anataka kuekeza basi aje serikalini tutakaa pamoja tutalizungumza hilo na tutalijadili vizuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba serikali ilianzisha vyoo maeneo mbali mbali ikiwemo Forodhani, Skuli ya Tumekuja pale nyuma, Kinazini na maeneo mengi. Lakini Mhe. Naibu Spika, kitu cha kushangaza sana ni kwamba kutokana na kutokujua umuhimu wa vyoo na tamaa ya baadhi ya

waliokabidhiwa kusimamia taasisi hizi, kuna baadhi ya vyoo ikiwemo Forodhani na hapa Afica House, Kinazini na maeneo mengine hugeuzwa maeneo ya biashara.

a) Mhe. Naibu Spika, je, hatuoni kwamba tumeshindwa umuhimu wa kuweka usafi mji wetu na kuangalia zaidi mapato.

b) Mhe. Naibu Spika, je, kama hiyo ni kweli maeneo ambayo yalikuwa ni vyoo yakageuzwa maofisi, serikali ina utaratibu sasa hivi ya kurejesha yale maeneo yakawa kama huduma ya hapo ilivyokusudiwa ya vyoo.

Mhe. Waziri Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kutokana na kutofuata madhumuni na makusudio ya kuwekwa vile vyoo baadhi ya vyoo vimegeuzwa kuwa maduka na kimoja wapo ni kilichopo pale Africa House. Ni kweli kabisa kimegeuzwa duka lakini hilo tumeliona na Mhe. Naibu Spika, nawahakikishia hicho tutakifunga mara moja tutakirejesha choo kama kawaida.

Mhe. Naibu Spika, pia kwa hayo maeneo mengine uliyosema nayo tutayafanyia kazi kama nilivyosema kwamba tutafanya utafiti wa kina kila mahala ambapo panahitajika choo, basi tutakiweka. Lakini ninachoomba kwamba Mhe. Mwakilishi tusaidiane katika kutunza vile vyoo kwa sababu kweli kila mmoja choo kile anaona sio jukumu lake kukitunza lakini hata kukiweka usafi, wewe madhali umekwenda umekikuta safi, basi fanya haja yako ukimaliza kiache safi vile vile. Lakini sio hali ya kawaida ilivyo hivyo, ndio tunasema tutajitahidi sisi kuvirudisha hadhi yake na tusaidiane sote tuviweke safi, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa uzoefu wa miji ya wenzetu kama vile Dar es Salaam, Arusha, Nairobi na Mombasa vyoo vimekuwa vya kutosha mno na vikiwa katika hali safi. Na kwa kuwa huduma hii ya vyoo katika miji hii inamilikiwa na watu binafsi na sio serikali na kwa kuwa katika Mji wa Unguja hususan katika maeneo ya Darajani, Malindi mpaka kufikia sehemu ya Maisara kuna nafasi nyingi za kujenga vyoo, lakini nafasi hizi zimegeuzwa bustani. Na kwa kuwa watu wanahitaji sehemu hizi kuweka mambo kama hayo ya vyoo ili kuimarisha usafi katika miji hii, lakini imekuwa tabu sana kupatikana kutokana ukiritimba wa kupata nafasi katika maeneo ya mji ule.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa imefika wakati wa kuwapa nafasi wawekezaji wa vyoo katika maeneo yale badala ya kugeuzwa bustani.

Mhe. Waziri Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, mimi nayakubali kabisa uliyoyasema na nimeshasema hapo awali kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kushirikiana na mwekezaji yeyote atakayekuja kutusaidia kuweka vyoo kwa malipo madogo kwa wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, lengo liwe ni kutoa huduma lakini na yeye apate pesa za kufanya *maintenance* kwa vyoo vile. Kwa hivyo, tuko tayari umezungumza maeneo yamegeuzwa bustani ni kweli kwa sababu unapokwenda kupumzika bustanini unahitaji kupumzika vizuri, sasa usikae

bustanini tena unataka kwenda uani basi unakwenda kwenye maua unayatilia mbolea ambayo haijawa tayari, hivyo sivyo. Kwa hivyo, tutakubali humo kwenye bustani kutaekwa maeneo maalum nafikiri hata Ulaya umeona Mhe. Mwakilishi umeshatembea unajua hilo, umeona miji mikubwa kuna vile vyoo vya kunyanyua vinawekwa vile baada ya muda vinanyanyuliwa vinakwenda halafu vinarejeshwa. Hilo ni jambo la kawaida na hata kwenye maoneshe makubwa makubwa vinawekwa vyoo mle. Kwa hivyo, hilo tutaweka kwenye bustani hizo tutashirikiana na kama unayo kampuni Mhe. Mwakilishi ilete tutakaa nayo pamoja.

Nam. 52

Umuhimu wa Nyaraka kwa Jamii

Mhe. Kazija Khamis Kona - Aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi na hasa wa vijijini hawafahamu umuhimu wa nyaraka kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Je, Mhe. Waziri Ofisi yako imejipanga vipi kuwaelimisha wananchi hao ili nao waijuwe faida ya ukusanyaji na uhifadhi wa nyaraka.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamjibu swali lake hilo naomba kutoa maelezo ya msingi yanayohusiana na suala hilo.

Kwanza napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli kwamba Nyaraka na Kumbukumbu ni moja ya Tunu za Taifa na nyenzo muhimu za uendeshaji wa shughuli za kila siku za Serikali. Utawala bora hauwezi kufanyika bila ya kuwepo kwa mipango bora ya uhifadhi wa kumbukumbu na yaraka za Taifa. Kwa kuelewa hilo Serikali imefanya uamuzi wa makusudi wa kuipa hadhi sehemu ya nyaraka na kumbukumbu kuifanya idara kamili kwa kuiweka chini ya Wizara ya Nchi (Ofisi ya Rais) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, kwa kuelewa kuwa wananchi wengi bado hawafahamu umuhimu wa nyaraka na kumbukumbu, wizara yangu imejiandaa vya kutosha kuwaelimisha wananchi hao ili nao wazijue faida za ukusanyaji na uhifadhi wa nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuaatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu, iliwasilisha mada maalum juu ya umuhimu wa Nyaraka na Kumbukumbu katika Uendeshaji wa Shughuli za Serikali, katika semina elekezi

iliyofanyika katika Hoteli ya *"Zanzibar Beach Resort"* Mazizini tarehe 5 hadi tarehe 7 Mei, 2011 na ambayo iliwashirikisha viongozi wote wa Serikali wakiwemo; Rais na Makamu wa kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, Mawaziri na Manaibu Mawaziri, Wakuu wa Mkoa na Wilaya, Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu. Vile vile mada hiyo iliwasilishwa kwenye semina ya watendaji wengine wa Serikali iliyofanyika katika hoteli hiyo, tarehe 25 hadi tarehe 27 Juni, 2011.

Aidha, shughuli za uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu tayari zimeingizwa katika Programu ya Mkakati wa mageuzi ya Utumishi wa Umma, ambapo shughuli mbali mbali zimepangwa kutekelezwa, zikiwemo elimu kwa umma kwa kutumia vyombo vya habari na pia kuimarisha miundo mbinu ili kuhakikisha hifadhi bora za Nyaraka na kumbukumbu zinabakia kua endelevu.

Mhe. Naibu Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma kilichopo chini ya wizara yangu kimeanzisha mafunzo ya cheti na stashahada ya menejimenti ya Nyaraka na Kumbukumbu na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa baadhi ya kada ya Managementi ya kumbukumbu.

Vile vile wizara yangu imetoa toleo maalum na kuziagiza Taasisi zote za Serikali kuchukua hatua za makusudi za uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka, ikiwemo kutenga chumba maalum cha kuhifadhia kumbukumbu (*Semi Current Records*) pamoja na kuajiri vijana wenye uwezo na taaluma katika fani hii na kujaza nafasi tupu za masjala.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa jumba la kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu ni kongwe na limeanza kujaa. Wizara yangu imeanza kufikiria kujenga jengo jipya la kuhifadhi Nyaraka litakalokuwa la kisasa ili kuhifadhi Kumbukumbu za aina zote muhimu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri umuhimu wa nyaraka na utunzaji wake Zanzibar tumekuwa tukikuwa sana kwa elimu, miaka ya nyuma ilikuwa tunamalizia darala la kumi na nne na sasa Zanzibar ina vyuo vikuu vitatu. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba sioni hatua yoyote inayochukuliwa na serikali kuweka elimu hii na nyenginezo kupitia mafunzo maalum ya vyuo vikuu kwa wanafunzi.

Je, kwa upande wake Mhe. Waziri tukiwa na vyuo vikuu vitatu ni hatua gani ambazo wangechukua kuweka kuhamasisha na kuweka uwazi juu ya umuhimu wa nyaraka kwa wanafunzi wetu ili hao ndio watakaokuwa raia wa baaadae.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, serikali imechukua hatua mbali mbali katika kuona kwamba inawaendeleza vijana wetu katika kutunza kumbukumbu na nyaraka za taifa na kwa kuelewa umuhimu huo ndio maana serikali imeanzisha mtaala katika Chuo chetu cha Utumishi wa Umma. Na vile vile serikali huchukua hatua ya kuwapa fursa wafanyakazi mbali mbali wanaohusika na masuala ya nyaraka katika kujifunza katika vyuo vyengine vya ndani na nje ya nchi katika kuona kwamba tunapata wataalamu katika fani hiyo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri katika jibu lake mama alisema kwamba alifanya semina na viongozi mbali mbali katika hoteli ya Zanzibar Beach Resort.

Je, Mhe. Waziri huoni kuna haja ya wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi na wao kuwapa semina katika ufahamu wa nyaraka.

Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inajipanga kufanya hilo katika mwaka huu wa fedha ili kuwapa taaluma Waheshimiwa Wawakilishi katika kujua umuhimu wa kumbukumbu na nyaraka. Kama nilivyokuwa nikijibu jibu mama nilisema kwamba kwenye mradi wa mageuzi ya utumishi wa umma Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu imetengewa fedha maalum kwa ajili ya kutoa taaluma kwa wananchi, lakini hata na viongozi mbali mbali wa serikali ili kuelewa umuhimu wa suala hilo.

Nam. 35

Ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Katika Mapitio ya Katiba

Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Aliuliza:-

Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mizengo Pinda, alitangaza rasmi katika mkutano wa Bunge uliopita kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano itapeleka Mswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba *(Constitutional Review Bill)* katika mkutano ujao wa Bunge.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshirikishwa kiasi gani katika kuandaa Mswada huo mpya.

(b) Ni mambo yepi ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetaka yaingizwe katika Mswada, kati ya hayo yepi yamekubaliwa na yepi yamekataliwa.

(c) Ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi kauli rasmi kuhusiana na Mswada huo na hatua zilizofikiwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu Nam. 127 ya suala kama hili niliyoyatoa katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha Mwezi wa Aprili, 2011 nilieleza kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa SMZ pamoja na watendaji waandamizi wa Wizara ya Katiba na Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali walifanya vikao vinne na Mwanasheria Mkuu wa SMT pamoja na watendaji wake na kukubaliana mambo ya

kuingizwa kwenye rasimu mpya ya Mswada. Baadhi ya maeneo waliyokubaliana ni pamoja na:-

i) Muundo wa Tume ya kukusanya maoni ya wananchi kuzingatia uwiano wa uwakilishi wa pande mbili.
ii) Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ufanywe kwa mashauriano na makubaliano ya pande mbili.
iii) Muundo wa Bunge la Katiba.
iv) Utaratibu wa uteuzi Wajumbe wa Bunge la Katiba.
v) Utaratibu wa Kuthibitisha Katiba mpya kwa kura ya maoni.
vi) Utaratibu wa kupitisha Mswada wa Sheria ya Mapitio ya Katiba.

Ni kweli kwamba kulikuwa na mambo ambayo tulikuwa hatujakubaliana vizuri; masuala haya baada ya kuiarifu Serikali yetu, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akifuatana na Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Waziri wa Ardhi, Makaazi,Maji na Nishati, Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano,Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Waziri wa Afya na Maafisa wengine,walionana na Mhe. Waziri Mkuu pamoja na watendaji wake kuyatatua masuala hayo. Ninafuraha kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba sasa mambo yote tumekubaliana isipokuwa kuna eneo moja tu ambalo tunaendelea kushauriana. Kitakachofanyika baada ya kumaliza mashauriano hayo ni kwa mswada huo kuchapishwa upya kuingizwa yote tuliokubaliana. Watakapokamilisha hayo na baadae kutuletea nakala na baada ya kuuthibitisha, basi tutawaarifu rasmi waheshimiwa wawakilishi pamoja na wananchi wengine kwa ujumla.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa sababu suala la katiba la mswada huu sio siri na ni suala ambalo linagusa moja kwa moja maslahi ya wananchi, Mhe. Waziri anaweza kututajia ni eneo lipi lilobakia ambalo bado kuna mazungumzo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambalo nadhani wananchi wa Zanzibar ni muhimu wakalielewa kwa sababu linagusa maslahi yao.

b) Katika jibu lake la mwezi wa April, 2011 na hata katika kikao cha bajeti cha Baraza lako Mhe. Waziri aliahidi Baraza lako kwamba kabla ya mswada huu kufikishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waheshimiwa Wawakilishi watapata nafasi ya kueleweshwa yale maeneo ambayo yalikuwa yana matatizo na mswada ule umefikia wapi hadi hivi sasa. Kwa mujibu wa suala langu na kwa taarifa zilizopo ni kwamba mswada huu utafikishwa katika kikao cha Bunge cha mwezi wa Novemba, 2011 ambapo hapo kati kati hapatakuwa tena na kikao chengine cha Baraza la Wawakilishi. Sijui kwa nini Mhe. Waziri asiseme kikao hiki kinachoendelea kuwaarifu Wajumbe wako ili wakapata kujua wajumbe wake ili wakaweza kujua suala

hili na kama wana maoni wakayatoa kabla ya mswada wenyewe kufikishwa, kwani kuna hatari kuwa ukifikishwa katika Bunge baada ya Baraza hili kumalizika hatutapata nafasi hiyo muhimu kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwanza kama nilivyosema ni kwamba mambo takriban yote sasa tumekubaliana, kuna eneo moja ambalo hili kama nilivyosema ilikuwa ni ujumbe kwa waziri mkuu ndiye aliyekuwa akiongoza ujumbe wa Tanzania Bara na ujumbe wa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Sasa ujumbe huu ni mzito, katika ujumbe huu kuna jambo moja ambalo halikukubaliwa au hatukukubaliana, sasa kwa sababu ujumbe huu ni mzito na kuna jambo ambalo hatukukubaliana bila shaka viongozi wa ujumbe hizi zote mbili ni lazima na wao wapate ushauri kutoka kwa wakubwa wao.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya kiwango cha swali lilipo itakuwa si vizuri kwa mimi kulisema hapa, kwa sababu hii ni *consultation* ambayo ipo baina ya viongozi wakuu wa nchi. Hivyo naomba Mhe. Mwakilishi kwamba ajuwe kuwa kuna suala moja ambalo hatujakubaliana lakini hili liko katika ngazi ya juu kwa mashauriano.

Mhe. Naibu Spika, swali lake la pili ni kwamba, bado nasema Waheshimiwa Wawakilishi tutawaarifu yote ambayo tumekubaliana baada ya suala hili kupata ufumbuzi na sisi kupata ule mswada tukaupitia na tukauhakiki na kuhakikisha kwamba, yote tuliyokubaliana ndio hayo yaliyoandikwa katika mswada huo. Ninawahakikishia Wajumbe kwamba hilo tutalifanya baada ya kukamilika utaratibu huu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa rasimu hii ilikuwa inategemewa kupelekwa kwenye mwezi wa Novemba katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tatizo letu Zanzibar kwamba sisi hatuna mamlaka ya kubadilisha kitu chochote kilichokuwemo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ndio maana tuliomba kwanza ilikuwa tupatiwe sio semina lakini japo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi serikali itupe yale mambo ambayo imekusudia kupeleka katika pendekezo la mswada ule, suala hilo hatukulipata.

Sasa hivi Mhe. Waziri anazidi kutwambia kuna suala ambalo liko katika ngazi ya wakubwa na hawezi kutwambia sisi na wakati sisi tumewekwa hapa kwa mujibu wa katiba kuwa sisi ndio wasemaji na kutetea haki za wananchi.

Sasa je, Mhe. Waziri haoni kwamba kuendelea kutufichaficha baadhi ya haya mambo ndio pale hata huo mswada pengine uanweza kuwa na kasoro nyingi ukaja ukaleta matatizo mengine hapo baadae? Na vile vile kwa kuwa sisi Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar hatupati kushiriki katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukapata kutoa yale maoni ya Zanzibar. Hatuoni kwamba tunazidi kukwamisha maendeleo ya watu wa Zanzibar?

Lakini swali la pili Mhe. Naibu Spika, katika rasimu ile ya marekebisho ya mswada wa katiba mpya kuna suala zima la kura ya maoni. Je, katika suala hilo serikali mapendekezo yake kura ya maoni itachukuliwa katika kiwango gani? Kwa sababu ukiangalia Zanzibar sisi tuko karibu milioni moja laki tatu, wenzetu Tanzania Bara wako karibu milioni arobaini. Je, katika suala zima la kura ya maoni juu ya maamuzi ya muundo wa serikali kuna *ratio* yoyote iliyopangwa labda katika kura ya maoni kuwa Wazanzibari wakisema vyenginevyo na wenzetu wa Tanzania Bara wakisema vyenginevyo kuna busara gani zitazotumika ili kuweza kuamua ni maoni gani ambayo yataweza kuheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu kwamba kuna mambo hapa ambayo nimeyataja mambo sita, ambayo haya yalikubaliwa mwanzo na nikasema kwamba kulikuwa kuna mambo ambayo tulikuwa hatujakubaliana na ujumbe kutoka Zanzibar ukiongozwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na ujumbe kutoka Tanzania Bara ambao unaongozwa na Mhe. Waziri wa Mkuu tukazungumza kwa pamoja na tukakubaliana mambo mengine yote isipokuwa lilikuwepo jambo moja ambalo hatujapata ufumbuzi wa pamoja.

Katika mambo ambayo tulikubaliana kwa wakati huo ambapo ujumbe wa Zanzibar na ujumbe wa Tanzania Bara tulikutana, ni pamoja na utaratibu wa kumpata Spika kwa mfano na Naibu Spika katika Bunge la Katiba.

Asilimia ya kura ya maoni kukubalika kwamba zile kura za maoni zitakazopigwa basi ziwe ni kura za maoni za Zanzibar peke yake na kura za maoni za Tanzania Bara peke yake kwa asilimia ile ambayo tumekubaliana.

Pia kuna suala la wajumbe wa Katiba katika kuamua mjadala wowote izingatiwe kwa mujibu wa utaratibu wa katiba yetu *two third majority* ya kila upande. Haya ni mambo ambayo yote tumeshakubaliana. Sasa hili jambo moja ambalo tulilizungumza kwa kweli ni suala ambalo lina maslahi kwetu sote na kwa sababu viongozi wetu wakubwa wameshasema kwamba hili tutalizungumza katika ngazi ya ukubwa, basi bado Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba bado hatutoweza sisi kulitoa hapa kwa sababu bado lina wakubwa ambao kwa maslahi ya Zanzibar, kwa maslahi ya sehemu zote mbili, Zanzibar na Tanzania Bara watakaa tukishakubaliana hapo tutawaarifu wajumbe kuhusu utaratibu mzima na makubaliano yote kama tulivyowaahidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, kabla ya swali langu naomba nimpongeza Mhe. Waziri wa serikali hii ya awamu ya saba kwa kuendeleza dhana ya usiri kwa wananchi wake. Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo nina swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Wanasheria wengi na watunzi wa katiba hutwambia katiba ni mkataba mkataba baina ya watawala na watawaliwa, hivyo hupaswa usiri wowote kwa watawaliwa kwa sababu ndio wamiliki wa katiba ule ni lazima wangeondoshwa. Katiba hii mpya ya Muungano ni mkataba wa serikali na serikali au wananchi na wananchi?

(b) Je, baada ya Bunge kupitisha katiba hii mswada huu utaletwa hapa kuridhiwa na Baraza kama matakwa ya kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mjumbe naomba arejee swali lake nambari mbili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba baada ya Bunge kupitisha mswada huu utaletwa hapa Barazani ili kukidhi matakwa ya kifungu cha Katiba ya Zanzibar ya kifungu cha 132, kwamba Baraza la Wawakilishi liridhie sheria ile.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, katiba

(Kuahirishwa kwa kikao kutokana na tatizo la umeme)

(Baada ya dakika mbili kikao kilirejea)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, katiba si ya serikali katiba ni ya nchi. Suala la katiba na sheria ni sawasawa katika utunzi, ni serikali ndio inayopeleka mswada ule kwa wananchi, lakini serikali ndio inayoanza matayarisho. Kwa hivyo, hapa ni matayarisho ya serikali na tunachofanya ni kuhakikisha kwamba serikali haya matayarisho yanayofanywa basi yanafanywa kwa maslahi ya Wazanzibari, na ndio nikasema kwamba bado kuna mambo ambayo bado kwa upande wa Zanzibar tunahisi lazima tukae pamoja tukubaliane na halafu hapo ndio tutawaelimisha wawakilishi wetu kwa niaba ya wananchi.

Lakini la pili kama katiba hii au mswada huu ukishakupitishwa kama utafuata matakwa ya kifungu cha katiba cha Zanzibar 132. Mhe. Naibu Spika, napenda niseme jambo moja kubwa lifuatalo. Katika mambo ambayo Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar haikueleza wazi ni suala la utungaji wa katiba ya pamoja. Suala hili hata ukitizama katika katiba ya Jamhuri ya Muungano utaratibu wake haupo wala Katiba ya Zanzibar utaratibu wake haupo. Sasa kwa kumega tu kidogo ile siri ni kwamba suala hili ni miongoni mwa hayo mambo ambayo tunayajadili ili kuhakikisha kwamba haki za Zanzibar zinalindwa katika suala hili.

Nam. 12

Baadhi ya Wananchi Kutolipwa Fidia

Mheshimiwa Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 2

Sheria inayotumika kuanzisha Skuli Binafsi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kwa wawekezaji binafsi Skuli ni huduma, wakati huo huo ni kitega uchumi.

(a) Uanzishwaji wa Skuli binafsi unaendeshwa kwa kutumia sheria ipi kati ya Sheria ya Vitega Uchumi na Sheria ya Elimu.

(b) Kama Sheria ya Vitega Uchumi inatumika, kwa nini baadhi ya skuli zinazoanzishwa hazielekei kutimiza masharti ya kuanzisha kitega uchumi kwa jinsi zilivyo.

(c) Kama Sheria ya Vitega Uchumi haitumiki ni kwanini wakati ambapo skuli ni mradi unaoingiza fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 2 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Sheria zote mbili; Sheria ya Elimu namba 6 ya mwaka 1982 na Sheria ya Uwekezaji namba 11 ya mwaka 2000 zinatumika katika uanzishaji wa skuli binafsi ikitegemea na aina ya mwekezaji na mahitaji yake. Kwa mwekezaji mzalendo anaruhusika kuanzisha skuli binafsi kwa kutumia Sheria ya Elimu peke yake, isipokuwa kama atahitaji kufaidika na vivutio vinavyotolewa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*), atawajibika kuwasilisha maombi ya mradi wake kwa kutumia Sheria ya Uwekezaji namba 11 ya mwaka 2000. Kwa mwekezaji kutoka nje anapaswa kuwasilisha mradi wake kwa mamlaka ya uwezekazai kwa mujibu wa sheria nambari 11 kabla ya kupata fursa ya kuanzisha skuli. Wizara ikishirikiana na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar katika kuyapitia maombi ya wawekezaji wa uanzishaji wa skuli binafsi tunawasilisha maombi yote kwa mamlaka hiyo ili kuhakikisha kuwa masharti ya sheria zote mbili yanafuatwa.

b) Skuli zilizoanzishwa kwa kutumia Sheria ya Uwekezaji zinatimiza masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Wizara haina taarifa ya skuli ambayo haikutimiza masharti iliyopewa. Hata hivyo, ieleweke kwamba skuli nyingi za binafsi zimeanzishwa na wazalendo na zimetumia Sheria ya Elimu nambari 6 ya mwaka 1982.

c) Kama nilivyotangulia kusema Sheria ya Uwekezaji namba 11 ya mwaka 2000 inatumika zaidi kwa wawekezaji kutoka nje. Kwa wawekezaji wa ndani wanaweza kuanzisha skuli kwa kutumia sheria ya elimu pekee yake kwani sheria ya uwekezaji imeweka kiwango cha mtaji ambacho mwekezaji wa ndani anapaswa kukifikia kabla ya kuomba idhini. Pamoja na kuwa uanzishaji wa skuli binafsi ni kitega uchumi lakini hadi sasa kiwango cha faida wanachokipata wawekezaji ni cha wastani kwa vile ada anazotozwa bado ni ndogo ukilinganisha na sehemu nyengine za Tanzania.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa wawekezaji wengi binafsi huanzisha skuli kwa kutumia jina la *International*. Je, wizara yake ina hatua gani ya kuchukua kutofuta jina hilo ili wananchi wetu wasije wakapata mshituko kwa kuanzishwa skuli kwa jina la *international.*

Pili kuna utaratibu gani wa kuzikagua skuli hizo za *private*.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ni kweli alivyosema Mheshimiwa kwamba skuli nyingi zinazoanzishwa Zanzibar hutumia jina la*i International*. Hili tumeliona na tumeanza kulifanyia kazi.

Suala la pili Mhe. Naibu Spika, sikulifahamu vizuri naomba anieleze.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba kuna utaratibu gani wa kuzikagua skuli binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, utaratibu upo tunazikagua skuli hizi kabla ya hata kuanza kufanya kazi na baada ya kufanya kazi tuna watu wetu ambao wanazipitia skuli hizi mara kwa mara.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri maswali ya nyongeza. Kwanza naomba Mhe. Naibu Waziri atueleze ni skuli ngapi za watu binafsi kwa Unguja na Pemba.

Pili je, haoni kwamba kuna haja ya kupitia tena upya na kuziangalia skuli hizi kutokana na kila mmoja kuwa ana bei yake ya namna anavyotolesha kama ni skuli za kulala au za kwenda na kurudi. Tunamuomba Naibu Waziri wapitie na kuangalia fedha za mtoto anazozitoa mzee zinaridhisha?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, skuli zote za watu binafsi Unguja na Pemba ni 296, *nursery* ni 213 zilizobakia ni *nursery* na *primary.*

Pia Mhe. Naibu Spika, tuna na vyuo vikuu viwili ambavyo ni vya binafsi. Lakini wazo lake lile alilosema kuwa wizara tunaonaje tukapitia tena si wazo baya lakini pia ieleweke kuwa hizi skuli zinatoza *fee* kutokana na huduma ambazo wanazitoa pale skuli. Lakini tumelisikia na tutalifuatilia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba skuli hizi za binafsi zinafuata sheria ya elimu, na kuna majina ya *International* yanayotumika. Mpaka sasa wamechukulia hatua skuli ngapi ambazo hazikufikia kiwango cha kutumia jina hilo na skuli ngapi zimethibitishwa kwamba zimefikia kiwango kwa kutumia jina hilo.

Lakini swali la pili je, vyuo vikuu vyetu ambavyo vipo chini ya uangalizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanavisaidia vipi vile vya binafsi ili viweze kukua na kuona kwamba vina viwango ambavyo vinahitajika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, skuli za *private* ambazo zinajiita *International* ni nyingi. Kama nilivyozunguzma mwanzo kuwa sasa tunazipitia na kuhakikisha kwamba hawatumii jina hilo wakati hawana sifa.

Vile vile niliwahi kueleza katika Baraza lako tukufu kuwa mpaka hivi sasa skuli ambazo ni *International School* kwa Zanzibar ni skuli mbili tu, moja ni *Zanzibar International School* ambayo iko Maisara na nyengine iko *Zanzibar Beach Resort.* Skuli nyengine zote zilizobakia wanajiita tu majina na kama nilivyosema kuwa hatua zitachukuliwa.

Kuhusu ni namna gani ambavyo tunavisaidia vyuo vya binafsi ambavyo vipo hapa. Mhe. Mjumbe kuna mashirikiano makubwa kati yetu sisi na vyuo hivyo, hata katibu wetu mkuu basi huwa anaingia katika bodi ya vyuo hivi kuhakikisha kama vinakwenda sambamba na sheria za nchi yetu ya elimu kwa jumla.

Nam. 7

Uvutaji Sigara Maeneo Yenye Mkusanyiko wa Watu

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:

Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa matumizi ya sigara yanasababisha madhara mbalimbali kwa watumiaji na hata wale wanaokuwa karibu na watumiaji hao wakati wa uvutaji wa sigara.

Katika kuwalinda wananchi wanaovuta na hata wale wasiovuta sigara ambao hupata athari kutokana na uvutaji, Serikali ina mpango gani wa kukataza uvutaji wa sigara katika maeneo yenye mkusanyiko wa watu.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba uvutaji wa sigara unaleta matatizo kwa wavutaji na walio karibu nao kama vile tafiti zinavyoeleza. Kwa kulitambua hilo, serikali kupitia Wizara ya Afya imeafanya utafiti hivi karibuni ili kujua ukubwa wa tatizo hilo hapa nchini. Matokeo ya utafiti huo yatatolewa mara tu uchambuzi utakapokamilika. Aidha, wizara inaifanyia marekebisho Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 1936 na kwamba suala la uvutaji wa sigara limezingatiwa ipasavyo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru waziri kutokana na majibu yake mazuri, lakini nina swali dogo la nyongeza lenye sehemu a na b.

(a) Kwanza nipongeze hatua za serikali kuanza kuchukua hatua juu ya tatizo hili, lakini kati ya hatua zinazoweza kupunguza ama kuondosha kabisa tatizo la

uvutaji wa sigara ama kuvuta sigara katika sehemu za watu ni pamoja na kutunga sheria ambayo tayari waziri anasema sheria inakuwa *reviewed*. Lakini chengine ni suala la kuongeza ushuru kati ya bidhaa zinazotokana na tumbaku pamoja na serikali kuhamasisha kujenga sehemu maalum za uvutaji wa sigara sehemu zenye mikusanyiko. Je, wakati serikali inafanya mapitio ya sheria hizo, katika hali ya dharura serikali ina mpango gani wa kuongeza ushuru ili kupunguza uvutaji wa sigara ikiwa ni pamoja na kuongeza mapato kwenye serikali.

(b) Lakini vile vile serikali ina mpango gani wa kuhamasisha kujengwa kwa sehemu maalum za uvutaji wa sigara katika sehemu zenye mikusanyiko kama Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumueleza kwamba katika hayo marekebisho ya sheria tumezingatia mambo manne. Kwanza udhibiti wa uingizaji, uuzaji, usambazaji na uvutaji wa sigara zenyewe. Pili jinsi ya matangazo yatakavyotakiwa yawe. Kwa mfano, yeyote yule atakayekuwa anataka kufanya biashara hiyo basi pale anapouza itabidi aandike kwamba sagari ni hatari kwa maisha yako, ukivuta ni athari yako. Yote tumezingatia katika sheria tunayoirekebisha.

Tutawataka watu wenye magari na vipando vyote kutia matangazo kueleza athari za uvutaji wa sigara katika vipando hasa zile daladala itakuwa si ruhusa. Si hivyo tu, lakini na adabu itakuwa kubwa kuliko ilivyokuwa hapo mwaka 1936.

Pili suala la kuongeza ushuru tutawashauri Wizara ya Fedha ambao ndio dhamana kwa shughuli hiyo na tutawaambia hasa kwamba kodi ya sigara iwe kubwa sana ili iwazuie wengi kuacha kuvuta sigara.

Suala la kujenga sehemu maalum namuomba Mhe. Mwakilishi angoje tukamilishe marekebisho ya sheria ili kila tunalolifanya liwe kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri katika majibu yake ametamka rasmi kwamba sheria inakuwa *reviewed* na kuwekwa masharti magumu katika kufanya biashara pamoja na kuvuta hiyo sigara. Kwa kuwa hiyo ibara nambari 11 ya katiba ya Zanzibar inazungumzia uhai wa kuishi katika kifungu kidogo cha (1) na cha (2). Je, kuendelea kuwaachia hawa watu kuvuta sigara si ku-*violet* katiba ya Zanzibar ibara ya 11(1) na (2).

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, pamoja na hali hiyo, lakini tusisahau vile vile katiba hiyo hiyo inasema kuna uhuru wa kuchagua. Kwa hivyo, ni mkono wa kushoto na wa kulia. Hatuwezi kumchagulia mtu kufanya kitu tulichokuwa hatuna haki naye, muhimu ni kuweka sheria na kuhakikisha kwamba anafuata sheria.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe.

Waziri kwa kuwa bado serikali haijakataza rasmi uvutaji wa sigara na kwa kuwa bado wananchi wetu wanaendelea kuathirika sana na uvutaji wa sigara.

Je, Mhe. Waziri serikali hamuoni kwamba ipo haja ya kuwapima wavutaji wote wa sigara kila baada ya muda.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nafurahi sana kwamba Mhe. Amina Iddi ameliona suala la kupimwa watu kila baada ya muda. Tatizo hili sio kwa wavutaji wa sigara tu, lakini kwa kawaida wananchi wote wanahitaji kupimwa afya zao. Suala hili Mhe. Naibu Spika, ingekuwa ni uwezo wa waziri peke yake basi kupima afya zetu ingekuwa ni jambo la lazima. Lakini kwa sababu nalo ni suala la hiyari, hatuwezi kuwalazimisha wananchi, isipokuwa tutawahimiza wananchi wote wapime afya zao.

Nam. 41

Mmong'onyoko wa Maadili

Mhe. Fatma Mbarouk Said - Aliuliza:-

Kadri siku zinavyokwenda mbele tatizo la mmong'onyoko wa maadili linaongezeka.

Mhe. Waziri, Wizara yako inaguswa kiasi gani na tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto) - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 41 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu inaguswa sana na kwa kiasi kikubwa katika tatizo hili la mmong'onyoko wa maadili kwa vijana.
Lakini Mhe. Naibu Spika, napenda nieleze wazi kwamba suala hili ni suala mtambuka na sio la wizara hii tu bali hata jamii na wazee ni lazima tujikaze ili kupiga vita suala hili.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango enedelevu wa vijana walio nje ya maskuli na wale walio maskulini unaotekelezwa na sekta ya elimu. Wizara yangu pamoja na Wizara ya Afya na asasi za kiraia katika kuhakikisha maadili ya vijana wetu yanaimarika kwa kujilinda yenyewe. Mpango huu ni ule wa kazi za *study* za maisha kwa vijana wa rika zote wanawake na wanaume.

Hadi kufikia sasa muongozo na mpango wa utekelezaji wake umeshakamilika na upo katika hatua ya kuchapishwa na kugaiwa kwa wadau kwa utekelezaji wake.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nimwambie tu kwamba mmong'onyoko huu

unasababishwa na utandawazi. Je, serikali itachukua juhudi gani ili kudhibiti tatizo hili la mmong'onyoko wa maadili haya ya Wazanzibari zaidi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto): Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba utandawazi ni moja katika vyanzo vikubwa vya mmong'onyoko wa maadili ya vijana. Lakini kama nilivyosema mwanzo kwamba sio wizara tu, kwa sababu wizara ni kuanzia saa 2:00 au saa 1 na nusu hadi saa 9 na nusu. Lakini zaidi wazazi nao wana jukumu kubwa, kwa sababu huu utandawazi uko nyumbani. Kuna *internet* kule, kuna TV na kuna mambo chungu nzima. Sasa kama wazazi na wao hawajashikilia nguvu suala hili, basi kwa kweli hali ya vijana wetu itakuwa ni mbaya.

Kwa hivyo, wito wangu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wazazi pamoja na jamii, tujitahidini kuyafuatilia haya na kuwaasa vijana wetu ili waondokane na tabia hizi mbaya.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba wizara yako haiko tayari kuliondoa tatizo hili na ndio maana mmong'onyoko unazidi kuwa mwingi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto): Mhe. Naibu Spika, sikubaliani na yeye hata kidogo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la mmong'onyoko wa maadili unaendelea siku hadi siku, na kwa kuwa pengine sisi wazee tunachangia kwa kiasi kikubwa mmong'onyoko huu wa maadili hasa majumbani kwetu.

Je, Mhe. Waziri huoni haja sasa wakati umefika wa wizara yako kuwafanyia semina wazee japo kwa makundi ili kuweza kujua majukumu yao.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: (Kny: Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto): Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna haja ya kuwaelimisha wazee na jamii kwa ujumla. Ndio maana nikasema kwamba huku kuna asasi mbali mbali. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina jukumu lake, Wizara ya Afya ina jukumu lake, Wizara yetu ya Wanawake na Watoto inajukumu lake na asasi nyengine zina majukumu. Ndio nikasema suala hili ni mtambuka, sasa sote kwa pamoja tuna wajibu wa kuelimisha jamii katika suala hili ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hili la mmong'onyoko wa maadili.

Nam. 16

Ukosefu wa Maji Safi na Salama Shehia ya Kikobweni

Mhe. Abdi Mosi Kombo - Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa wananchi wa Shehia ya Kikobweni wanakabiliwa na tatizo la kupata maji safi na salama.

Je, Mhe. Waziri, ni lini wananchi hawa wataondokana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imeliona tatizo hilo lilitokana na kuzidiwa uwezo wa uzalishaji wa Mradi wa Chaani. Kwa kuliona hilo Wizara ina mpango wa kuchimba visima vyengine katika maeneo ya Chaani na Kisongoni kupitia mradi utakaosalidiwa na Ubalozi wa China nchini, na mara tu kazi hiyo itakapo kamilika wananchi wa Kikobweni watafaidika na Mradi huo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Katika mkutano wa Baraza la Wawakilishi uliopita, Mhe. Naibu Waziri aliwahi kujibu kwamba Zanzibar hakuna shida ya maji, lakini leo anakiri kwamba kuna shida ya maji, ikiwa ni pamoja na Nungwi na Matemwe. Naomba anisaidie lipi ni jibu sahihi katika mawili haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie kidogo, sijamfahamu.

Mhe. Naibu Spika: Anasema katika kikao kilichopita ulizungumza kwamba Zanzibar hakuna shida ya maji. Sasa leo unazungumza kuwa ipo shida ya maji. Je, lipi jibu la uhakika, shida ipo au imeondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, hatujajibu kwamba Zanzibar hakuna tatizo la maji. Tumesema kwamba Zanzibar tatizo la maji lipo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itajitahidi kuliondoa tatizo hili kwa njia zake zote inazozijua wenyewe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri umetuambia hapa kwamba tayari mmeshatiliana saini na makampuni hayo ya nje ya kuweza kuchimba visima hapa Zanzibar. Je, Mhe. Naibu Waziri kazi hiyo itaanza lini ili wananchi waondokane na tatizo la kunywa maji machache kwenye mabonde.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Ni kweli tumeshafunga mikataba na wafadhili na miradi ambayo itashughulikiwa na Benki ya Afrika *(ADB)* itaanzia mwezi wa 11 mwaka huu.

Nam. 23

Semina Elekezi Kuhusu Uvuvi Haramu na Halali

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Wizara yako iliobwa na semina elekezi na jamii ya wavuvi wa Kojani juu ya Ufafanuzi wa uvuvi halali na haramu, lakini hadi sasa hakuna matumaini wala dalili ya kupata mafunzo hayo.

(a) Je, ni kitu gani kilichozuwia utekelezaji wa jambo hilo kama si dharau dhidi ya jamii ya Kikojani wakati ulishatoa agizo la utekelezaji wa jambo hili

(b) Kwa kuwa Wakojani wengi ni wavuvi na mchango wao katika taifa hili kwenye sekta hiyo unafahamika, kwa nini kumekuwa na kero endelevu dhidi ya jamii hii hasa katika maeneo wanayoegesha vyombo vyao kwa kuanza kumilikishwa watu binafsi licha ya wao kuwepo katika maeneo hayo kwa muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 23 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba inafanya kazi kwa karibu na kamati ya uvuvi ya shehia ya Kojani na kamati ya uvuvi ya shehia ya Mpambani zikiwa ndio wawakilishi rasmi wa shughuli za uvuvi katika kisiwa cha Kojani kwa mujibu wa sheria.

Pamoja na kwamba mimi mwenyewe nimewahi kuzungumza na kamati hizo za uvuvi za shehia mbili za Kojani mbele yake Mhe. Mwakilishi katika kikao hicho na wala sikupitia Idara ya Uvuvi baadae. Haikutokea ombi kwamba kamati hizo zinahitaji semina elekezi juu ya ufafanuzi wa upi ni uvuvi haramu na upi ni uvuvi halali. Ninachoelewa mimi ni kwamba wawakilishi hao wa uvuvi wa kisiwa cha Kojani wana maarifa makubwa na wamekuwa walimu wazuri wa kuwaelekeza wengine juu ya uvuvi usioharibu mazingira, sio tu katika kisiwa cha Kojani, lakini katika wilaya ya Wete na kisiwa cha Pemba chote na ndio maana Mwenyekiti wa Kamati ya Wavuvi wa Wilaya yote ya Wete ni mzaliwa wa kisiwa cha Kojani.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli nakiri kupokea barua ya Jumuiya inayojiita ya maendeleo ya uvuvi wa Kojani wanaoishi hapa Unguja Mjini, kutaka mdahalo baina ya Jumuiya hiyo na wataalamu wa wizara yangu juu ya kwa nini sheria nambari 7 ya mwaka 2010 iliyopitishwa na Baraza lako tukufu, ilipiga marufuku baadhi ya taratibu za uvuvi ambazo kitaalamu inaonekana kuharibu mazingira. Kimsingi wizara imekubaliana na ombi hilo na wakati muafaka ukifika utekelezaji wake utafanyika kwa mujibu wa mpango kazi wa

wizara yangu iliyojipangia baada ya kuidhinishiwa na Baraza lako tukufu kwa bajeti ya mwaka huu wa fedha miezi miwili iliyopita.

Aidha, hakuna malalamiko yaliyopokewa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kutoka katika kamati za uvuvi za shehia za Kojani kuhusiana na usumbufu au kero wanazopata wavuvi wa Kojani katika kuegesha vyombo vya uvuvi. Hata hivyo, kama Mhe. Mwakilishi amepata kero hizo, ofisi za taasisi zangu ziko tayari kushirikiana naye katika kuzitafutia ufumbuzi wake.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba siku ya tarehe 16 mwezi Machi, mimi na Jumuiya ya Maendeleo ya Wavuvi wa Kojani tulifika ofisini kwako na waliomba na ukaridhia kuwapa semina elekezi, umeshapewa maelekezo na mpaka leo hii inafika mwezi wa 8 au wa 9 hawajapata jibu lolote.

Je, kwa sababu wavuvi wa Kojani wana nia njema ya kutaka ufahamu, wizara yako ina mpango gani wa kuwapatia semina hiyo, ili wakajifunza kutoka wizarani kwako.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokiri kwamba ni kweli kuwa yeye na Jumuiya ya Wavuvi wa Kojani wanaoishi hapa Unguja Mjini, walikuja ofisini kwangu katika mwezi wa Machi na kuomba mdahalo baina yao wavuvi wa Kojani na wataalamu wa wizara yangu.

Kimsingi kama nilivyoeleza kwamba ombi lake tumelikubali, lakini ni miezi miwili tu iliyopita ndio wizara hii mpya imeidhinishiwa bajeti na katika mpango kazi wa wizara iliyojipangia masuala ya taaluma ya uvuvi imepangiwa kuanzia kipindi cha pili cha mwaka, yaani miezi mitatu inayokuja. Kwa hivyo, ombi lake limepokewa, programu imepangwa wakati ukifika Jumuiya itaarifiwa lini mdahalo huo wa semina hiyo elekezi utafanyika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa taaluma kwa wavuvi kuhusiana na uvuvi kwa jumla ni muhimu na wavuvi wanatarajiwa wamiliki madiko yao. Je, inapotokezea wavuvi wanapokonywa umiliki wa madiko na Halmashauri za Wilaya, ni hatua gani wizara yake inachukua ili kuwarejeshea haki zao na kuweza kupata taaluma inayohusika katika wizara.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe Mhe. Rashid Seif Suleiman Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, ambapo ndani ya jimbo hilo kuna diko la Kichwaani. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kwamba madiko ni taasisi zilizochini ya wizara yangu kwa mujibu wa sheria. Kifungu nambari 10 cha sheria nambari 7 ya mwaka 2010 inataja hivyo na kwamba yanasimamia kwa pamoja baina ya Wizara ya Mifugo na Uvuvu na wananchi husika. Sasa ikitokea kwamba wavuvi wamenyang'anywa mamlaka ya usimamizi wa diko lao basi ni jukumu la wizara yangu kushirikiana na kamati yao ya uvuvi ili kuona kwamba waliowanyang'anya wanawarudishia umiliki huo. Sasa kama wananchi wa eneo la Kichuani katika Jimbo la Ziwani diko lao wamenyang'anywa na

Halmashauri ya Wilaya Chake Chake, basi namuahidi kwamba Idara ya Uvuvi ilioko ndani ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tutashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ili kuona kwamba wavuvi wa Kichuani wamerudishiwa mamlaka na umiliki wa kuendesha diko lao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekubali kuwa sheria ipo na atakubaliana na mimi kwa kuwa sheria ipo na hivi sasa dimbwi la uvuvi haramu unaendelea Unguja na Pemba. Je, waliofanya vitu hivyo ni wangapi ambao sasa hivi wameshachukuliwa sheria.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, samahani naomba arudie tena swali lake.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Waziri ulikubali kuwa sheria ipo na ilitungwa katika Baraza hili tukufu la Wawakilishi na hivi sasa Unguja na Pemba wimbi hilo la uvuvi haramu linaendelea. Je, ni wangapi ambao walikamatwa na sheria ikachukua mkondo wake kwa hao waliofanya vitendo vya haramu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mwakilishi wa Jimbo la Kitope ambako kuna shughuli nyingi za uvuvi haramu katika maeneo ya Pwani Mchangani. Ni kweli kwamba sheria ya uvuvi nambari 7 ya mwaka 2010 imepiga marufuku uvuvi haramu. Taratibu hizo zinasimamiwa kwa pamoja baina ya wizara yangu na kamati za shehia husika. Kwa hivyo, kamati ya Shehia ya Pwani Mchangani nayo ni mdau katika suala hili ambapo Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Kitope naye anasehemu yake katika usimamizi huo. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Naibu Spika, mheshimiwa mwakilishi ashirikiane na kamati yake ya uvuvi ya Pwani Mchangani ili kuona kwamba tunashirikiana na wizara ili kuhakikisha kwamba uvuvi haramu katika maeneo hayo yanadhibitiwa.

Swali lake la pili alilozungumzia ni kwamba katika mwezi wa Ramadhan vikundi vinne vilikamatwa katika maeneo ya Kaskazini Unguja vikijishughulisha na uvuvi haramu. Hatua za kisheria zimechukuliwa na hivi sasa zinaendelea. Juzi tu katika eneo la Kizimkazi boti moja kubwa ya uvuvi ilikamatwa ikivua uvuvi haramu katika maeneo ya Minai, ripoti yake imepelekwa polisi na hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa.

Nam. 38

Wataalamu Kuelimisha Wajasiri Mali

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

Lengo kuu la serikali yetu tukufu ni kuimarisha maisha ya wananchi wake, ndio maana ikaanzisha Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Inaelekea lengo hilo bado halijafahamika licha ya juhudi kubwa tunazozichukua sisi wawakilishi

kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujikusanya pamoja kwa lengo la kupatiwa nyenzo ya kujikwamua kiuchumi.

Je, wizara haioni kuna haja ya kuwaleta wataalamu katika majimbo kutoa taaluma katika kufanikisha suala hilo ndani ya majimbo yetu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 38 kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakiri kwamba ipo haja ya kuwa na wataalamu hao katika majimbo yetu. Pia katika kufanikisha hilo, wizara yangu imeweka wataalamu ambao ni maafisa ushirika katika ngazi za wilaya kwa lengo la kutoa taaluma juu ya dhana ya ushirika na umuhimu wa wananchi kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi, yaani za uzalishaji mali na huduma kupitia vyama vya ushirika.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hayo wizara yangu kwa kupitia Idara ya Ushirika imekuwa ikiwahamasisha na kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuanzisha vyama vya ushirika vya fedha, yaani *SACOS* bank kwa lengo la kuwawezesha kujipatia nyenzo na mahitaji ya kujikwamua kiuchumi kwa kuptia mikopo yenye masharti nafuu.

Mhe. Naibu Spika, haya yote yanalenga katika kutekeleza azma ya serikali ya kuimarisha maisha ya wananchi wake. Mhe. Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo, bado dhana ya uwezeshaji haijaeleweka vyema kwa wananchi.

Aidha, suala la taaluma linahitaji juhudi zaidi na endelevu kwani inachukua muda kwa watu kubadili na kuunga mkono mipango inayopendekezwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukuwe fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi kwa juhudi zao za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kujikusanya kwenye vikundi, ili waweze kusaidiwa kupatiwa nyenzo za kujikwamua kiuchumi. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na viongozi wa ngazi zote, kuanzia masheha, wakuu wa wilaya pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi ili dhana ya uwezeshaji iweze kufanikiwa vizuri zaidi miongoni mwa wananchi wetu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, jimbo langu mpaka sasa hivi kutokana na mifuko mbali mbali iliyotolewa, lakini Jimbo langu la Amani bado halijafaidika. Je, Mhe. Waziri ananiahidi nini juu ya kuwawezesha wananchi wangu wa Jimbo la Amani kiuchumi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Ahsante Mhe. Naibu Spika, ahadi yangu kwa waheshimiwa wote ni kwamba tushirikiane kwa pamoja, na mimi nawaahidi kabisa katika suala zima la uwezeshaji, serikali imejipanga vizuri na tuko tayari kuhakikisha kwamba tunawawezesha wananchi wetu. Juhudi mbali mbali

zimechukuliwa na serikali. Hivi sasa tumo katika juhudi ya kutafuta fedha za ziada na kuanzisha mfuko maalum na tunatarajia katika mwezi wa Januari, kufuatia mfuko wetu wa kujitegemea kutimia miaka 20, basi tutamuomba Mhe. Rais kwamba siku hiyo tutasherehekea miaka 20 ya mfuko wa kujitegemea, lakini pia tuanzishe mfuko huo utune zaidi kwa lengo la baadae kwenda katika majimbo yote, sio Jimbo la Amani tu, lakini majimbo yote 50 ya Unguja na Pemba katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Katika jumla ya mambo ambayo yanaonekana wananchi bado hawajayaelewa kuhusu dhana nzima ya uwezeshaji ni fikra ambazo tumekuwa tukizizungumza mara nyingi katika Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ina nafasi za kazi katika nchi ya Qatar ambazo zinatolewa, pamoja na kujitahidi kuelimisha wananchi lakini bado inaonekana kuwa wanaamini nafasi hizi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atueleze kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, sisi pamoja na wananchi kwa jumla nini uhalisia wa suala hili zima, ili wananchi waweze kulielewa?

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima yako pamoja na taarifa kwa Waheshimiwa Wajumbe, ingawa swali la msingi ilikuwa la uwezeshaji. Tumekuwa tukilizungumza kweli na wananchi bado hawajalielewa suala hili. Tatizo liliopo ni kwamba redio vifua zinafanyakazi zaidi kuliko redio halisi. *(Makofi)*

Ukweli wa suala hili kama tulivyosema na ninaendelea kusema pia kwamba tayari tumeshafanya mazungumzo na waziri anayehusika na mambo ya *labor* wa Qatar. Kwa kweli nilikutana naye ana kwa ana na ndipo pale aliponiambia tunahitaji vijana au wananchi kutoka Zanzibar kwa ajili ya kuja kufanyakazi Qatar na wala hatuhitaji viwango vya elimu kwa sababu kazi za aina nyingi zipo.

Lakini pamoja na hayo yote sisi tulisema sisi hatuwezi kusema tunawapeleka tu, isipokuwa lazima kuwe na makubaliano, kwa sababu kuna hatima na maisha, hivyo tunataka kazi ambazo watapewa ni kazi za heshima na wala hawawezi kupelekwa wananchi wetu kule halafu wakapata kazi ambazo si za heshima.

Kwa hivyo, tunachokifanya hivi sasa na hivi punde nilikuwa nikimnong'oneza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Uchumi anitafutie fedha kidogo kwa sababu ya kwenda kukamilisha mazungumzo yangu pamoja na kusaini makubaliano kati ya Qatar na Zanzibar katika suala zima la kuwapeleka vijana wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hilo bado halijachukuliwa hatua, isipokuwa tangazo au taarifa iliyotoka kulitoka nafasi na walitangaza kwa ajili ya Saudi Arabia. Hivyo, majina hayo

tayari tumeshayapokea na hivi sasa taratibu za kuwapeleka huko Saudi Arabia zimeanza kuchukuliwa na tayari wapo ambayo wameshakwenda huko.

Lakini suala la Qatar bado na wananchi naomba wawe watulivu na *Inshaallah* suala hili litakapokuwa tayari tutalitangaza na mimi naahidi nitalileta hapa Barazani, ili wananchi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wajue.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Shirika la Taifa la Biashara ya Mwaka 2011

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: *Bismilahi Rahman Rahim,* Mswada wa Sheria mpya wa Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*). Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa hii ya kuweza kusoma mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria Mpya wa Shirika la Biashara la (*ZSTC*).

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Taifa la Biashara la (*ZSTC)* lilianzishwa chini ya sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1966 kwa Tangazo la Kisheria (*Legal Notice No*. 39 la mwaka 1968) Tangazo hili lilitoa mamlaka kwa *ZSTC* kufanya kazi zifuatazo:-

1. Kuchukua na kuendeleza kazi zote zilizokuwa zinafanywa na Jumuia ya Wakulima wa Karafuu (*Clove Growers Association*) ikiwa pamoja na mali na madeni yake.

2. Kuimarisha mazao ya kilimo na uendelezaji wa masoko yake kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

    (a) Kuuza nje mazao ya kilimo, yaani *export*.
    (b) Kuendeleza usarifu wa mazao ya kilimo.
    (c) Kununua na kuwauzia wakulima vifaa mbali mbali ikiwa pamoja na vifunganisho vya bidhaa.
    (d) Kuwanunulia na kuwauzia wakulima wa karafuu magunia ya kuhifadhia mazao ya kilimo na
    (e) Kumiliki mali zisizohamishika kama vile majengo, mashine, viwanda na kukodisha mali hizo.

3. Kutoa fursa za mikopo kwa madhumuni maalum au kama itakavyoelekezwa na Rais kwa ajili ya utekelezaji wa mambo mbali mbali yafuatayo:-

    (i) Uvunaji wa mazao ya kilimo.
    (ii) Msaada wa kifedha kwa wakulima baada ya kuweka amana nyengine yoyote kulingana na Sheria ya Mazao ya Kilimo.

Utekelezaji wa Majukumu ya Shirika:

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu nilioutaja hapo juu ulifanyika kwa ufanisi mkubwa katika miaka ya 1970 na kwa kiasi katika miaka ya 1980. Hali ya utekelezaji huo hata hivyo ulianza kuteremka kuanzia miaka ya 1990, ambapo *ZSTC* iliacha kushughulikia baadhi ya mazao ya kilimo ambayo yalikuwa maarufu wakati huo na kujikuta inashughulikia na zao moja tu la karafuu, ambalo nalo linaendelea kukumbwa na matatizo ya kiuzalishaji, kibiashara pamoja na kukithiri biashara ya magendo.

Mhe. Naibu Spika, takwimu za mwenendo wa uzalishaji wa karafuu zinadhihirisha kuwa zao hilo linaendelea kupungua mwaka hadi mwaka kwa kiwango kikubwa kutoka wastani wa tani elfu 10 kwa mwaka, katika kipindi cha mwaka 1964/1965, 1973/1974 hadi kufikia wastani wa tani 2,400 katika kipindi cha mwaka 2004/2005 na 2009/2010. Wastani huu ni sawa na asilimia 27 ya uzalishaji uliokuwepo katika kipindi cha mwaka 1964/1965 au 1973/1974.

Hali hiyo, imesababisha kwa kiasi kikubwa kushuka kwa hadhi ya *ZSTC* kifedha, kibiashara na hata haiba yake mbele ya wakulima wa mazao ya kilimo na hasa wakulima wa karafuu.

Kutokana na mwenendo huo mbaya ambao umepunguza kwa kiasi kikubwa mchango wa sekta hiyo katika shughuli za kiuchumi na mapato ya fedha za kigeni, ulifanya serikali kufikiria njia ya kuliimarisha zao hilo kwa kuzingatia uzito huo.

Serikali iliingia zao la karafuu pamoja na biashara yake katika mpango wa mageuzi ya kiuchumi na fedha (*Economic and Financial Reform Program*) katika utekelezaji wa mpango wake wa kuondoa umasikini (*ZPRP*) mpango huo wa mageuzi bado unaendelea kutekeleza kupitia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini (MKUZA).

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2003 serikali kwa kushirikiana na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (*UNDP*), ilifanya utafiti uliokuwa na lengo la kubaini kwa undani matatizo ya zao la karafuu na usimamizi wake, ili kuandaa mkakati wa kushughulikia zao hilo pamoja na biashara yake.

Baadhi ya kasoro kubwa zilizobainishwa katika utafiti huo ni kama zifuatazo:-

1. Kupungua kwa uzalishaji wa zao la karafuu na kuuzwa katika soko la Kimataifa.
2. Kuwepo kwa matatizo ya usafirishaji wa zao hilo.
3. Kuwepo kwa utaalamu mdogo wa kuimarisha soko la karafuu.
4. Kuwepo kwa huduma duni za kifedha kwa kuendeleza zao hilo la karafuu.
5. Kutokuwepo kwa usarifu wa zao hilo, ili kuweza kuongezeka thamani.

Kwa kuzingatia ukubwa wa athari za matatizo hayo, serikali iliandaa mkakati wa kuendeleza zao la karafuu, yaani *Clove Development Strategy* (*DCS*).

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla mkakati huo wa kuendeleza zao la karafuu umejielekeza katika maeneo makubwa yafuatayo:-

(i) Kuimarisha uzalishaji wa zao hilo kwa kushughulikia matatizo yanayokwaza uzalishaji.

(ii) Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa biashara ya karafuu wa kuweka sheria mpya pamoja na muundo mpya *ZSTC* na kuainisha majukumu yake na kupunguza gharama za uendeshaji wake.

(iii) Kuweka mfumo wa huduma za kifedha kwa ajili ya uendelezaji wa zao la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na sababu mbali mbali hata hivyo, utekelezaji wa mkatati wa kuimarisha zao la karafuu na biashara yake haukuweza kuanzishwa. Hivyo, mapendekezo ya mswada huu ni hatua ya awali ya kuanza rasmi utekelezaji wa mkakati huo, ambao pia ni sehemu ya utekelezaji wa mageuzi ya kiuchumi na fedha kama ilivyobainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini (MKUZA).

Mswada huu unakusudia kuweka majukumu mapya *ZSTC* hadhi yake kisheria pamoja na mamlaka yake katika usimamizi na biashara ya zao la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, mswada unaowasilishwa leo mbele ya Baraza lako tukufu ni matokeo ya kazi ya muda mrefu iliyokuwa inafanywa na serikali kwa madhumuni ya kubainisha matatizo ya shirika, hivyo kuandaa hatua madhubuti za kuchukuliwa kwa ajili ya kuliimarisha shirika hilo.

Kazi ya msingi ya kutathmini shirika ilifanywa na Mshauri Mwelekezi, ambaye alipata wasaa wa kutosha wa kuchukua maoni ya wadau wote wa zao hili, ikiwa pamoja na wasafirishaji wa magendo ya karafuu.

Kutokana na hali hiyo, mswada huu wa sheria ni sehemu moja tu ya utekelezaji wa hatua za uimarishaji wa Shirika la *ZSTC* pamoja na uhuwishaji wa zao la karafuu.

Hatua nyengine za kurekebisha muundo wake, kuimarisha uwezeko wake wa kibiashara, upunguaji wa gharama za uendeshaji wa kilimo cha karafuu pamoja na huduma za kifedha zitatekelezwa kulingana na Mkakati wa Uendelezaji wa Karafuu pamoja na *Program* ya Mageuzi ya *ZSTC* ambayo inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 hadi kukamilika kwake.

Mswada wa Sheria inayopendekezwa. Mhe. Naibu Spika, madhumuni makubwa ya kuandaa mapendekezo ya mswada huu wa sheria ni kutandika misingi imara ya utekelezaji wa mageuzi yanayokusudiwa kufanywa, ili kulifanya shirika hili kuwa imara kibiashara na kusimamia vizuri maendeleo ya zao la karafuu.

Kwa ujumla mapendekezo ya mswada huu wa sheria yanakusudia kuweka masharti ya kisheria kuhusu uendeshaji, ukuzaji pamoja na usimamizi wa biashara ya karafuu kwa kuzingatia misingi ya ushindani, kuweka muundo mpya wa kitaasisi za *ZSTC* na kubainisha majukumu ya chombo hicho.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia haja ya kutekeleza madhumuni yaliyotajwa hapo juu inapendekezwa kutungwa sheria itakayoweka masharti na usimamizi mzuri wa Shirika la Biashara la Taifa la *ZSTC* pamoja na mambo mengine yanayohusiana na shirika hilo.

Kwa ujumla rasimu ya sheria hii imegawika katika sehemu kuu tano, ambapo kila sehemu inafafanuliwa madhumuni yake na masharti ya kisheria kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza, kama ilivyokawaida ya uandishi wa sheria sehemu hii ya kwanza inaweka masharti ya kisheria kuhusu jina la sheria, tarehe ya kuanza kwake, upeo wa mamlaka ya sheria, yaani *scope and application* pamoja na tafsiri ya maneno mbali mbali yanayotumika katika sheria hii inayokusudiwa kutungwa.

Sehemu ya pili, inapendekeza kwa masharti ya kisheria kuhusu uundwaji wa Shirika la Biashara la *ZSTC* pamoja na kuweka hadhi yake ya kisheria.

Sehemu ya tatu, inaweka masharti ya kisheria kuhusu majukumu, uwezo, uongozi wa Shirika jipya la *ZSTC* pamoja na masharti ya uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Shirika. Kadhalika katika sehemu hii rasimu inapendekeza masharti ya kisheria kuhusu uundwaji wa Bodi ya Wakurugenzi, majukumu na mamlaka yake, utaratibu wa maslahi yao, uwezo wa kuanzisha kamati na utaratibu wa mikutano ya bodi pamoja na taratibu za ushughulikiaji wa masuala ya nidhamu.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya nne ya rasimu inaweka masharti ya kisheria kuhusu fedha za shirika na kubainisha vianzio vyake, uwekaji wa vitabu vya hesabu pamoja na ukaguzi wa hesabu hizo. Vile vile sehemu hii inaweka masharti ya kisheria kuhusu uandaaji, uwasilishaji pamoja na uzingatiaji wa taarifa za mwaka kuhusu mapato na matumizi yake, taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya shirika kwa mwaka unaohusika.

Sehemu ya tano, inaweka masharti ya kisheria kwa mambo ya mchanganyiko kuhusu uwezo wa waziri anayehusika na biashara katika utekelezaji wa sheria hii. Makosa na adhabu kwa makundi tofauti shirika, kampuni, wakala na kadhalika. Makosa ya jumla na adhabu, uwezo wa waziri kutunga kanuni, uwezo wa *ZSTC* kutunga miongozi maalum, yaani *rules*. Vile vile sehemu hii inaweka masharti ya kisheria ya kufuta sheria zilizoanzishwa kwa Shirika la *ZSTC*.

Mhe. Naibu Spika, rasimu ya mswada wa sheria hii ina jaduweli moja ambalo linaweka utaratibu wa kisheria kuhusu utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Bodi ya Wakurugenzi.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, katika maelezo yangu hapo juu nimejaribu kujenga hoja ya kwa nini imeonekana ni muhimu kuiandika upya sheria za *ZSTC* na kuandaa mswada wa sheria ambayo itapendekeza muundo mpya na majukumu yake. Kadhalika kwenye hotuba yangu hii nimetoa kwa muhtasari maelezo ya uchambaji wa kila sehemu ya mswada wa sheria yenyewe, ili kurahisisha mazingatio ya Waheshimiwa Wajumbe.

Hivyo, ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba wamepitia mapendekezo yaliomo pamoja na kuzingatia maudhui ya mswada wenyewe kwa uzito na umakini unaostahili.

Kwa hivyo, kwa imani na matarajio hayo Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako liupokee mswada huu, kuujadili na hatimaye kuukubali, ili kuwezesha kutungwa kwa sheria itakayounda *ZSTC* mpya.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo) Mhe. Naibu Spika, ifuatayo ni hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji wa Karafuu na Mazao mengine ya Kilimo na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhana Wataala)* kwa kutujaalia uzima wa afya na tukaweza kuhudhuria katika Baraza lako tukufu, na wale waliokuwa wagonjwa Mwenyezi Mungu awajaalie wapone haraka, ili tuweze kuungana nao katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Pili, nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika kwa kunipatia nafasi hii ya mwanzo kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo yanayohusiana na Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji, Biashara na Ukuzaji wa Karafuu na Mazao mengine ya Kilimo na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nitoe mkono wa pole kwa Wazanzibari na Watanzania wote kwa msiba mkubwa uliotufikia wa kuzama kwa meli ya MV. *Spice Islanders*, ambayo ilisababisha vifo vya wapendwa wetu wengi. Kwa kuelewa kwamba msiba huu ni wetu na unamgusa kila mmoja wetu; kwetu sisi ni kusema tu *Inalillahi Wainnailaihi Rajiuun.* Tuendelee kuwaombea Dua kwa Mwenyezi Mungu wenzetu waliotangulia awalaze mahala pema Peponi AMIN. Nasi tuliobakia atupe moyo wa subra.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo Baraza letu nalo limeondokewa na mjumbe mwenzetu, marehemu Mussa Khamis Silima mjumbe wa Baraza hili kupitia Jimbo la Uchaguzi la Uzini. Naomba nitoe pole kwa familia ya marehemu pamoja na wananchi wa Jimbo la Uzini. Tumekuwa nao muda wote wa msiba na tupo pamoja nao katika kumuombea dua mwenzetu tukijua safari hii si ya mmoja ni yetu sote.

Mhe. Naibu Spika, aidha nitumie nafasi hii ulionipa kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa mashirikiano yao ya dhati kabisa

waliyonipa kwa muda wote tulipokuwa tunafanyakazi ulizotukabidhi ukiwemo mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe hao kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Mohamed Ali	-	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa	-	Mjumbe
4. Mhe. Rufai Said Rufai	-	Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-	Mjumbe
7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad	-	Mjumbe
8. Ndg. Amour Mohammed Amour	-	Katibu
9. Ndg. Shemsa Maabad Mohamed	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kwa kumpongeza Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kuandaa mswada huu muhimu sana na kuuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, ili ujadiliwe na hatimae upitishwe.

Pongezi hizi pia ziwaendee Mhe. Naibu Waziri wa Wizara hii, Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote walioweza kusaidia kwa namna moja au nyengine kuandaa mswada huu. (*Makofi*)

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika watendaji hawa wamekuwa ni washauri wazuri kwake yeye binafsi Mhe. Waziri lakini pia wametoa mashirikiano mazuri na maelekezo kwa kamati yetu muda wote tulipokuwa tunajadili na kuupitia mswada huu. Tunawapongeza na kuwashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba tegemeo kuu la uchumi wa nchi yetu bado liko kwenye zao la karafuu, pamoja na jitihada nyingi ambazo serikali yetu imezifanya za kutafuta maeneo mengine lakini bado jicho letu linaiangalia karafuu kama ndio mkombozi wetu. Kwa kutambua hilo, serikali kupitia Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko inafanya jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba zao hili linaendelea kutunzwa na kuimarishwa kikwelikweli, ili liendelee kuleta tija tunayoitarajia.

Mhe. Naibu Spika, serikali katika azma yake ya kuliendeleza zao la karafuu, imekuwa ikipambana na changamoto nyingi kama vile maradhi ya mikarafuu inayotokana na mabadiliko ya tabia nchi, kuzeeka kwa mikarafuu yenyewe, kukatwa katwa ovyo kwa matawi ya mikarafuu wakati wa uchumaji na hata kukatwa kwa kupiga mkaa. Vile vile changamoto nyengine ni kuyaacha mashamba ya mikarafuu bila ya kupaliliwa kwa muda mrefu, mikarafuu midogo iliyopandwa kufa kabla ya muda wa kuzaa, lakini kubwa kuliko yote ni usafirishaji wa zao hili kwa njia ya magendo.

Mhe. Naibu Spika, hali hii imelisababishia Shirika letu la Taifa la Biashara kununua kiwango kidogo sana cha zao hili kinyume na linavyozalishwa. Ni jambo la kushangaza

sana kuona nchi jirani haina hata mkarafuu mmoja lakini ina nafasi katika Soko la Dunia kama msafirishaji mkubwa wa zao hilo.

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa 2009 pekee nchi jirani iliuza kwenye Soko la Dunia jumla ya tani 2,269 wakati sisi wenye mikarafuu tuliuza jumla ya tani 4,823. Hii inaonyesha dhahiri kwamba suala la usafirishaji wa zao la karafuu kwenda nchi jirani ni changamoto kubwa kwetu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inatoa wito kwa wakulima wa zao la karafuu kuacha kabisa tabia ya kuwauzia karafuu zao wafanyabiashara wanaosafirisha karafuu kwa njia ya magendo, badala yake wauze karafuu zao katika Shirika letu la Taifa la Biashara (*ZSTC*) na kwa kufanya hivyo tutaiwezesha serikali kuwa na uwezo wa kufanya shughuli za maendeleo kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake ya mwaka 2011/12 alilieleza Baraza lako juu ya mikakati ambayo serikali imejiandaa nayo katika kulinusuru zao la karafuu.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuwa na sera kuhusu biashara ya karafuu, ambapo kwa sasa serikali imeamua kumlipa mkulima asilimia 80 ya bei itakayouzwa katika Soko la Dunia. Utekelezaji wa jambo hilo tayari tumeuona kwani kwa kipindi kifupi tu bei ya zao la karafuu imepanda mara tatu, kutoka shilingi 10,000/-, shilingi 12,000/- na hadi sasa ni shiling 15,000/- kwa kilo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kufanya marekebisho juu ya muundo wa Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC*), ili kuweza kubainisha majukumu yake mapya ambayo yataliwezesha kuwa na sheria madhubuti na kuliimarisha kiutendaji kwa kuajiri wafanyakazi wenye uwezo mkubwa zaidi na mbinu za kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza kwa dhati wizara kwa kuanza utekelezaji wa mikakati hiyo, mswada unaohusu marekebisho hayo ya shirika ndio uko mbele yetu ukiwa na madhumuni ya kuimarisha utendaji ambao hautaishia kwenye ununuzi wa karafuu tu, bali hata kwenye mazao mengine ya kilimo kama ambavyo sheria hii inayotaka kutungwa itakavyompa waziri uwezo wa kuyatangaza.

Kamati inaamini hata yale malengo mengine wizara iliyojipangia nayo yataweza kutimia. Kwa mfano, kuimarisha mfumo wa biashara ya karafuu yetu kimataifa kwa kuipatia utambulisho maalum *(Branding)* kwa kutumia misingi ya *Intellectual Property* pamoja na kuanzisha mfuko wa maendeleo ya karafuu *(Cloves Development Fund)*, ambao pamoja na mambo mengine, utashughulikia kilimo cha karafuu na kutoa huduma za kuendeleza zao hilo.

Katika kuhakikisha kwamba Shirika la Taifa la Biashara linaundwa likiwa na nguvu mpya yenye kulipa uwezo mkubwa wa kuweza kuhimili si tu kumuwezesha mkulima wa karafuu kuneemeka kwa zao hili, bali pia kuingia vyema katika ushindani wa kibiashara

katika Soko la Dunia. Jambo ambalo litaliwezesha kusaidia kwa kiasi kikubwa kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imeridhishwa na muundo, majukumu na malengo ya *ZSTC*, kama yalivyopendekezwa katika mswada huu ikiamini kwamba hayo ndiyo yatakayosaidia kuifikia azma tuliyoikusudia. Uongozi wake pamoja na bodi itakayoundwa ndivyo ambavyo kamati ingeomba viwe chachu ya maendeleo ya shirika. Kamati yetu isingependa hata kidogo kuundwa kwa chombo hiki kwa muda mfupi tu halafu tukafikiria kukiunda tena upya.

Kamati yetu iliupitia mswada kifungu kwa kifungu na kupendekeza na kukubaliana na Mhe. Waziri baadhi ya maneno yaliyotumika pamoja na kuongeza kifungu kimoja ambacho tumependekeza kiwe kifungu cha 25 tukiamini kwamba kulikuwa na umuhimu wa kuwepo kwake. Aidha Kamati ilikubaliana kukifuta kifungu cha 9(1)(f), ambacho tayari utekelezaji wa kifungu hicho upo kwenye sheria nyengine Nam. 11 ya mwaka 1985.

Mhe. Naibu Spika, maeneo mengine ambayo kamati imeona ni vyema kubadilisha baadhi ya maneno ni kama tulivyoyaambatanisha kwenye karatasi ambazo tayari Waheshimiwa Wajumbe wameshagaiwa. Tunaamini kwamba Wajumbe wa Baraza lako tukufu watapata nafasi nzuri ya kuujadili kwa kuuchangia na bila ya shaka hatimaye wataupitisha na kuwa sheria ili kuliwezesha shirika letu la *ZSTC* kutimiza malengo yake.

Mhe. Naibu Spika, Tunapenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wa Zanzibar kwamba zao la karafuu bado litabaki tegemeo kuu la kiuchumi kwa Nchi yetu. Ni vyema tukaendelea kulitunza na kulilinda ili uzalishaji wake ukue na hadhi yake idumu kwa muda mrefu. Na kwa vile ni zao tulilolitegemea kiuchumi, si busara hata kidogo kufikiria kulibinafsisha, Kamati inaishauri Serikali iendelee kulidhibiti na kuliimarisha kwa kuzingatia kuleta tija kwa wakulima wenyewe na Serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Pamoja na jukumu hilo la utunzaji na uendelezaji wa karafuu, mazao mengine ya kilimo ya biashara ni muhimu nayo yakaimarishwa, kama vile hiliki, pilipili hoho, vanilla na mengineyo, ili nayo yazidi kutoa mchango mkubwa kwa wakulima na uchumi wa nchi yetu. Kamati yetu inaishauri Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuwa na mashirikiano ya karibu mno na Wizara ya Kilimo na Maliasili ili haya malengo yote yaweze kutimia.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naunga mkono mswada huu nikiwaomba na Wajumbe wenzangu nao waukubali ili tumuwezeshe Mhe. Waziri aitimize azma yake.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mara nyengine naomba nikushukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mfukufu kwa kuendelea kuturuzuku neema yake ya uhai na uzima, na

kutuwezesha kuendelea na shughuli zetu muhimu hapa katika kutunga sheria na kujadili mambo aliyoyagusa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Mjumbe wako wa kwanza wa Baraza lako tukufu kutoa mchango wangu kuhusiana na mswada huu wa sheria ya kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar yaani ZSTC.

Nimpongeze Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko kwa juhudi zake mbali mbali anazochukua za kuona vipi tunaweza kuwasaidia wakulima wa karafuu na wananchi wan chi yetu kupata tija zaidi katika zao hili muhimu, vile vile zile fikra nyingi ambazo alikuja nazo katika Hotuba yake ya Bajeti ambazo ni imani yangu kwamba itatekelezwa moja baada ya nyengine ili kuendelea kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuingia katika mswada huu moja kwa moja nilikuwa naomba nitoe maoni yangu ya jumla kama ifuatavyo.

Kwaza mimi nimeelewa kwamba madhumuni ya mswada huu kama ulivyoelezwa kwamba lengo lake pamoja na kuanzishwa shirika lakini ni kuweka masharti bora pamoja nausanifu, ukuzaji, uendelezaji, uzalishaji, bisahra na ukuzaji wa karafuu na mazao mengine ya kilimo na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi kwa maoni yangu ni kwamba bado pamoja na kuona uzito wa kulikubali suala hili njia sahihi zaidi ya kuendeleza zao la karafuu, wakulima wa karafuu nchi yetu na uchumi wake kwa jumla itaendelea kubakia ni kulibinafsisha zao la karafuu, nimesikiliza kwa makini sana maoni ya kamati ya baraza lako ya Fedha, Kilimo na Biashara. Walilisisitiza kwambasi vyema zao hili likabinafsishwa na ni vyema kwa maslahi ya taifa likaendelea kubakia chini ya udhibiti wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, naweza kuelewa husdu zetu na mara nyingi tumekuwa na kwaida ya kuogopa mabadiliko ya mambo mbali mbali, lakini mara zote uzoefu umetuonyesha kwamba yale tunayohofia mara nyingi yamekuwa ni kinyume na vile ambavyo tumekuwa tukifikiria, naomba niseme hivyo kwa mifano michache Mhe. Naibu Spika.

Katika miaka mingi Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukihofia sana kuruhusu mabenki binafsi katika nchi yetu, tulichukua kila juhudi kuilinda PBZ tukiamini kwamba kuingia kwa mabenki binafsi kunaweza kuidhoofisha PBZ na pengine kungeleta hasara katika uchumi wa nchi yetu, lakini leo tumeshuhudia kuruhusu kwa mabenki binafsi kumetoa chacho ya ushindani kwa PBZ, pamoja na kuwepo na mabenki mengi Zanzibar bado PBZ imeendela kubakia kuwa ni benki bora kuliko benki zote zilizopo hapa Zanzibar na ndio inayotegemewa na wananchi wa Zanzibar na inaaminika zaidi.

Lakini zaidi kuja kwa mabenki mengine kumetoa chachu ya ushindani kwa PBZ ione njia bora za kuimarisha huduma zake, sote leo ni mashahidi kwamba PBZ ya leo sio PBZ iliyokuwepo kabla ya kuruhusu mabenki mengine katika nchi yetu.

Katika mfano mwengine Mhe. Naibu Spika, vile vile hapa tulikuwa tukihofia sana kuruhusu soko huru la sarafu za kigeni katika nchi yetu, tukidhani itayumbisha uchumi. Lakini leo kuruhusu biashara huria katika eneo hilo kumeondoa dhiki katika suala hili lakini pia kumeiongezea mapato serikali kutokana na maduka mengi ya ubadilishaji wa fedha za kigeni katika nchi yetu.

Kwa hivyo nata kusema kwamba ipo mifano mingi ya mambo ambayo tumekuwa tukiyahofia lakini leo badala yake hali imekuwa tofauti, mimi naamini kwamba hata katika suala hili la biashara ya karafuu, kwamba kubinafsisha kutasaidia kuleta ushindani zaidi wan chi yetu kunufaika kuliko tunavyofikiria, hata kwa shirika letu la ZSTC naamini kwamba tukibinafsisha kukatokea ushindani kutalifanya shirika hili liamke kama ilivyoamka PBZ, na kuweza kujipanga zaidi nikiondoa kile kitu walichokiita wenzetu yaani kujiachia kwa sababu tu ya kuamini hakuna mpizani dhidi yao.

Lakini naamini kubinafsishwa kwa karafuu Mhe. Naibu Spika, kutaondosha hata hili suala la magendo, sasa hivi naamini watu wengi wanaendelea kushiriki magendo pamoja na jitihada kubwa za serikali kuzuia na kutumia gharama nyingi kuzuia, kwa sababu wanaamini kuna sehemu ambapo wanaweza kupata tija zaidi kuliko ndani ya Zanzibar. Lakini ukibinafsisha utafanya wale wanaonunua katika maeneo hayo waje wafungue masoko yao hapa ndani ya Zanzibar, kwa hivyo kwanza ile hofu na ile iliyoelezwa katika maoni ya Kamati kwamba kuna nchi jirani na mimi nitaitaja Kenya katika rekodi zote za soko la dunia tunaiona kwamba Kenya inaongoza kwa usafirishaji wa karafuu tukijua kwamba haina karafuu.

Mimi naamini litaondoka kwa sababu tutakapokuja hapa wale watakaonunua watakuwa wananunua na wanauza kwa ajili ya Zanzibar wakiwemo ndani ya Zanzibar, lakini sio hilo tu watakapoweka masoko yao humu Zanzibar serikali itakuwa inanufaika kwa sababu itakuwa inapata kodi zake kwa mujibu wa sheria zake ilizoweka. Kwa hivyo bado mimi naamini kwamba mkombozi wa saula la kuendeleza zao la karafuu ni kuingiza ushindani katika soko hilo nab ado nchi yetu ikafaidika, ikawa ndio msafirishaji mkubwa ikalilinda zao laki likiwemo ndani ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hilo katika haya ya jumla niseme na labda Mhe. Waziri akija hapa atanisaidia mimi nimeupigia sana mswada huu, niseme hili jina la sheria sioni kwamba limetoshelezwa kwa kilichomo ndani ya sheria, jina la sheria linasema Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na kuweka masharti bora kwa ajili ya usafifu, uendelezaji, uzalishaji, biashara na ukuzaji wa karafuu na mazao mengine ya kilimo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, nilichokiona ndani ya mswada huu kikubwa ni uanzishwaji wa Shirika na kazi zake, haya mambo mengine yanayotajwa yote haya usafiru, uendelezaji, uzalishaji, biashara sikuyaona humu ndani, labda ndio madhumuni ya serikali kutwambia kwamba kifungu namba sita na namba saba cha Sheria hii kwa sababu kinaorodhasha mambo mengi ambayo Shirika litafanya kwamba ndio yatakidhi haya yametajwa hapa.

Lakini kwa maoni yangu mimi Mhe. Naibu Spika, kwamba haya yametaja mambo ambayo shirika linaweza kuyasimamia lakini zile taratibu gani zitafuatwa kuongeza usarifu, uendelezaji, uzalishaji, ukuzaji pamoja humu ndani ya sheria hatuyaoni. Imeipa mamlaka Shirika njia za kufanya mambo hayo lakini kwa hivyo ningesema ingelitosha kama ile sheria ingalikuwa ni shirika kuanzishwa na kazi zake, lakini kwa maana ya mambo haya vipi tutasafiru, vipi tutaendeleza, vipi tutaongeza uzalishaji, vipi tutafanya biashara katika sheria hii siyaoni katika kifungu namba sita na saba ambavyo vimetaja hayo mambo, sana sana naona kazi za shirika.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine la jumla ambalo linasema kidogo limevunjika moyo kwa sababu lilikuwa likizungumzwa sana ndani ya baraza lako, nilitegemea sheria hii katika hayo yanayotegemea kufanywa basi pia lingeanzisha utaratibu wa branch na kuona hizo taratibu zinafuatwa ili kunufaika na mfumo huo, lakini nimeangaza mote humu sikuliona hilo.

Lakini nashukuru Kamati pia imeliona na imelisisitiza lakini katika huo mswada lili Mhe. Naibu Spika, sikuliona kabisa.

Kwa hivyo hayo ni maoni yangu ya jumla ya kuhusiana na mswada huu.

Lakini sasa nikiingia ndani ya Mswada wenyewe Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe maoni yafuatayo.

Kwa katika kurekebisha maneno kwa ufupi katika kifungu cha tatu kinachoweka tafsiri ya maneno, naomba kwanza katika hili niipongeze sana Kamati kwa kufanya kazi nzuri sana ya kufanya marekebisho mengi ya msingi katika mswada huu, lakini yapo machache ambayo ndio ubinaadamu itakuwa labda haikuyaona ningeomba tuyarekebishe.

Moja katika tafsiri ya Mjumbe imeandikwa Mjumbe maana yake ni Mjumbe wa bodi inajumuisha mwenyekiti kwa maana hiyo isomeke mjumbe wa bodi na inajumuisha mwenyekiti.

Nikitoka hapo nije kifungu cha saba kifungu cha 2 (a) hapa tumezungumzia kununua na kuuza karafuu na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani, tatizo langu Mhe. Naibu Spika ni hii bei ya ushindani tunayoitaja hapa. Katika tafsiri ya maneno huku haikutafsiriwa bei ya ushindani ni ipi, kwa hivyo imeliachia shirika lenyewe kuamua bei ya ushindani ni ipi. Katika hili mimi napata wasi wasi pamoja na nia nzuri ya serikali naipongeza kwamba imeongeza bei ya karafuu lakini kuna kitu nadhani hatusemi kweli, hata kamati hapa katika hotuba yake wameipongeza serikali kwamba sasa inalipa asilimia thamanini ya bei ya soko.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima mimi sikubaliani nayo taarifa hii, katika kuangalia taarifa ambazo siku hizi zinapatikana kirahisi tu katika mtandao bei ya karafuu ya Zanzibar katika soko la Dunia hivi tunavyozungumza ni $ 35 kwa kilo za kimarekani, dola 35 Mhe. Naibu Spika, kwa hesabu za haraka haraka tu kwa kiwango cha ubadilishaji wa fedha hivi sasa ni shilingi 60,000 kwa hivyo serikali inapolipa shilingi 15,000 kwa

kilo inalipa asilimia 25% ya bei ya soko la dunia iliyopo hivi sasa. Sasa tunaposema tunalipa 80% hatusemi ukweli.

Mimi nilikuwa binafsi nilikuwa na mashaka mwaba kweli serikali wakati wote inaweza kulipa asilimi 80 kwa sababu ya gharama nyingi zinazojumuisha mambo haya zaidi ya ile kusafirisha, kwa hivyo mimi ningetegemea bora tungesema ukweli kama tunaweza kulipa asilimia hamsini lakini ikawa ni asilimia hamsini kweli, ili tukajua kwamba kuna gharama nyingi serikali inapaswa kuziingia hapa kati kati mpaka kuifikisha karafuu katika soko.

Lakini kusema unalipa asilimia thamanini wakati kama nilivyosema siku hizi taarifa zinapatikana kwa urahisi tu, bei ya soko la duni ni shilingi sitini elfu kwa maana ya dola 35 za kimarekani hapo tutakuwa hatujamwambia ukweli mkulima wa karafuu. Ndio maana nikasema katika kufungu cha 7(2)a ukinambia litanunua kwa bei ya ushindani bila ya kutafsiri ushindani hasa ni ipi.

Mhe. Naibu Spika, kuna maneno mengine naomba ninusuru muda nisiyaseme hapa na uje uniruhusu wakati wa kupitisha vifungu katika kutafsiri maneno ya kiingereza, nadhani mengi kidogo yamechanganyika changanyika mno baadhi Kamati imejitahidi imerekebisha lakini bado yapo mengine, lakini haya kwa sababu ni ya lugha uniruhusu nirekebishe katika kupitisha vifungu.

Kifungu changine ambacho nina matatizo nacho katika kufungu hichi cha saba ni kufungu cha 7(2)m hiki kinazungumzia kuwe na Muwakilishi au Ofisi ndani au nje kwa kusimamia masuala ya kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii hii katika kifungu chengine imeliruhusu shirika kuwa na wakala wa shughuli zake mbali mbali, mimi nadhani Mhe. Naibu Spika, ni busara zaidi nitapunguza gharama kwa shirika kuona utaratibu huu wa kuwa na wakala kuliko kuruhusiwa kuna na muwakilishi au Afisi ndani au nje ya nchi kwa kusimamia masuala yake ya kibiashara. Kule katika kuweka wakala tumesema kwamba wakala huyo hatoshughulika na masuala ya kibiashara, nadhani hapo ndio imewekwa hii kwamba kwa masuala haya itakuwa na muwakilishi au Ofisi yake.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tunao udhoefu huo wa kuanzisha Afisi kama hizo za kibiashara katika baadhi ya nchi na wajumbe wa baraza laki waliokuwemo katika baraza lililopita ni mashahidi, jinsi gani Afisi hizi zimeongeza gharama za uendeshaji na utawala kuliko shughuli zilizokusudiwa. Kwa hivyo nina wasi wasi kuibebesha shirika mzigo huu kwa kuwa na Afisi zake za nje, nadhani tukubaliane hapa yatakuja mambo mengi ya kufungua Afisi za nje kutuongezea gharama shirika kuliko ile kazi yake iliyokusudiwa.

Kwa hivyo ulimwengu wa sasa wa kibiashara na Mhe. Waziri kwa bahati ni mfanya biashara mzuri na mzoefu ambae amejenga jina kubwa ni kwamba tunafanya shughuli nyingi kwa kutumia mawakala, kwa nini tusitumie mawakala kufanya shughuli hizi ambazo pengine wanalipwa kamisheni kwa kile ambacho itakuwa imekiletea nchi au Shirika badala ya Afisi ambazo itabidi kuziendesha na kusimamia utawala wake na

uendeshaji muda wote wa miezi kumi na mbili katika mwaka mzima, pengine shughuli zake ni chache sana katika muda huu.

Kwa hivyo mimi nadhani nipendekeze kwamba hichi kifungu (m) kingeliondoshwa na kule kwenye wakala ikaruhusu pia kuwa na wakala kwa upande wa biashara. Kama nilivyosema katika vifungu vyengine pia kuna maneno lakini tutarekebisha huko wakati wa kupitisha vifungu.

Lakini eneo jengine ambalo linakwenda sambamba na yale maoni yangu ya jumla ya kusema kwamba bado naamini kwamba kuruhusu biashara huria katika eneo hili kutasaidia zaidi, ni kile kifungu cha 9(1)a ambacho kinazungumzia kama Shirika litakuwa Muuzaji na msafirishaji pekee wa karafuu. Mimi kama nilivyosema ni imani yangu kwamba tukiruhusu ushindani tutalifanya shirika liimarike zaidi litaacha kusinzia pale kama ilivyokuwa PBZ huko nyuma na litachangamka zaidi kibiashara ikiwa karuhusu ushindani katika ununuzi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hapo hapo kifungu cha 9(1) kifungu cha (d) kimeipa mamlaka shirika kupanga bei ya kununulia karafuu na mazao mengine ya kilimo, hapo ndipo nilipokuwa nasema kwamba kuna mambo yanafanyika ambayo hayatoi nafasi ya kuwa na *balance* ya kuwalinda wananchi wetu. Shirika ndio mnunuzi wa karafuu halafu vile vile ndio mpangaji wa wa bei ya karafuu, linampangia mkulima bei ya kununua mazao yake, hii mimi nadhani hatutendi haki hata tukichukua mfano wa Tanzania Bara ambako kumeachiwa biashara huria ya mazao mengi, kuna wale walionunua lakini kuna bodi ambazo zimewekwa za mazao mbali mbali ndizo zinazoweka bei za kununulia.

Kwa hivyo nadhani hapa kwetu kulipa shirika mamlaka ya kununua lakini pia kupanga bei tutakuwa hatutoi utaratibu nzuri wa kuhakikisha, kama nilivyosema tutasema tunamlipa mkulima asilimia thamanini kumbe ukweli tunamlipa asilimia ishirini na tano ya baei ya soko la Dunia.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze kamati kwa kuona kifungu cha 9(f) na kupendekeza kukifuta na mimi nakubaliana nao, kwa sababu hatupaswi kulipa shirika mamlaka ya kukamata. Lakini mamlaka ya kukamata ni ya polisi na tayari kuna sheria ya karafuu ya Na. 11 ya mwaka 1985 ambayo inaweka utaratibu huo, kwa hiyo sioni sababu ya kuwa na kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika, nisogee katika kifungu cha kumi hapa nina maoni ya jumla, kifungu cha 10(1) kama zilivyo Sheria zote tunazoletewa hapa kinaendeleza utaratibu wa kwa mba mtendaji mkuu wa shirika au idara, au chombo chochote kinachoundwa anateuliwa na Rais, mimi nadhani nina bahati mbaya Mwanasheria Mkuu hayupo lakini Serikali ipo inasikia. Nadhani nimefika pahala ile dhana ya kuwa na katiba za kidemokrasia zinazopunguza mamlaka ya Rais tuitekeleze hapa Mhe. Naibu Spika, huu utaratibu wa kumfanya Rais anamteua kila Afisi au kiongozi mkuu wa chombo sio utaratibu mzuri, matokezeo yake unalimbikiza watu wengi sana wanangojea kuteuliwa na wanakuwa hawateuliwi sijui kama tunafahamu.

Moja katika mambo ya nchi hii ni kwamba mrajis wa Ardhi anateuliwa na Rais, kama ilivyokuwa kawaida kila sheria inayoletwa hapa au mswada basi mtendaji mkuu wa chombo anateuliwa na Rais, leo Mhe. Naibu Spika, tokea mwezi wa Februari, hakuna mrajis wa ardhi na hajateuliwa mwengine. Suala la Msingi kama hili ambalo linahusu *Transation* siku hizi za kibiashara kila siku unapotaka kuweka amana ya ardhi yako, lakini mrajis wa ardhi ukitaka kwenda pale hayupo tokea mwezi wa Februari.

Sasa haya ndio matatizo ya kila mtu au mkuu wa chombo lazima ateuliwe na Rais mimi nadhani tumefika hapala tuwe na utaratibu wa kuwaamini pengine ikiwa waziri, au utaratibu wa kutangaza nafasi hizi. Lakini utaratibu wa kuwapa watu hawa ukawekwa utaratibu mwengine kuliko utratibu wa kuendeleza udhoefu huu wa kwamba kila mkuu wa kampuni, idara au shirika hata juzi Mkemia Mkuu tumeona hapa kila chombo inapelekea kuwa na mlundikano wa nafasi ambazo bado zinachelewa mno kujazwa, kwa hivyo huwasumbua wananchi ambao wanategemea kupata huduma katika maeneo yale.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nadhani serikali imefika pahala ipitie upya suala hili la kuona kuna haja ya kuyagawa madaraka haya badala ya yote kuyaweka kwa mtu mmoja ambao sio utaratibu mzuri wa kimokrasia katika nchi zetu, na nchi nyingi duniani.

Mhe. Naibu Spika, hapo hapo katika kifungu cha 10 kifungu kido cha 4 kimesema. Mkurugenzi Muendeshaji atateuliwa kwa kipindi cha miaka mitano na kutokana na utendaji wake bora na wa kuridhisha anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi cha miaka mitano, mimi binafsi sikubaliani na utaratibu wa huu, kama nimekifahamu cha kiingere ni kwamba hataruhusiwa kuchaguliza zaidi ya miaka kumi ndio maana yake. Mimi nadhani hizi nafasi kwanza sio za kisiasa au nafasi nyengine ambazo zinamfanya mtu mpaka azoee pahala. Lakini hili ni shirika la kibiashara Mhe. Naibu Spika, kama tumempata mkurugenzi muendeshaji mahiri, mzoefu, mzuri zaidi akafanya kazi vizuri na shirika likapata tija kwa nini tumuwekee *respection* ya miaka kumi.

Kwa wenzetu unaweza kumkuta mtu kakaa muda mrefu hasa katika mambo ya kibiashara kwa sababu ya kujenga uzoefu zaidi nap engine kaonyesha ufanisi zaidi, kwa hivyo nadhani hatuna haja ya kumuwekea vizingiti kwamba ahakikishiwe miaka kumi, lakini pia hatuna sababu ya kumkisia kwa kumuwekea miaka kumi kama ilivyopendekeza sheria, ilikuwa nadhini tungeweka wazi kwamba ikiwa mamlaka yote ya uteuzi kwa sasa hivi ni Rais, huko mbele tutakavyorekebisha vyovyote kama nilivyopendekeza awali basi kama kuna mtua ambae anafanya kazi vizuri tuweze kumruhusu aendelee na nafasi yake, sioni sababu ya chombo kama hiki ambacho zaidi ni chombo cha kibiashara kuwekewa mipaka ya muda wa utendaji wake kwa mtendaj mkuu.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze kamati kifungu cha 17 kukiona kwamba yale mashauriano na mkutano yanapaswa kuwa baina ya bodi na Wizara, badala ya kusema serikali tu ambapo serikali ina tafsiri pan asana, tusingeweza kujua ni chombo gani, naipongeza kamati kwa kuliona hilo na marekebisho ya lugha tutarekebisha katika vifungu.

Lakini jengine ambalo ningependekeza tulitazame ni katika kifungu cha 22, 23, 24 na hiki kipya ambacho kimependekezwa na kamati cha 25, nafurahi kwamba kifungu cha 22 kamai imekirekebisha na sasa wameweka lile ambalo wanalizungumza hapa kuweka kikomo cha *minimum na maximum.*

Lakini kufungu cha 23 kitaendelea kubakia kama kilivyo kwa sababu kamati haijakigusa, nilikuwa naona tuendeleze utaratibu ule ule kwenye kifungu cha 23 (2) pale kinaweka utaratibu ule ule kwamba kimeweka faini isiyopungua milioni 20, lakini huku juu hakuna *sealing* kwa hivyo kama nilivyowahi kusema kwenye miswada mingi, inaweza mtu akaadhibiwa kwa kuambiwa alipe faini ya milioni mia mbili, mia tatu au milioni moja kwa sababu hakujaweka *sealing.* Kwa hivyo napendekeza pia tungeweka *sealing* au ukomo wa ile adhabu ambayo inapendekezwa na hivyo hivyo katika kifungu cha 24.

Lakini vile vile mbali ya suala la kuweka kikomo pia nilikuwa napata tatizo na ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie, katika kifungu cha 23(1) na kifungu kipya kilichopendekezwa na Kamati cha 25, ukivisoma ineonekana vinatoa fursa ya kuwepo makosa sio tu yaliyoweka na sheria hii lakini pia na kanuni.

Mhe. Naibu Spika, nikikisoma kifungu hiki kinasema. *“ endapo kosa chini ya Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii 23(1)”.*

Na kipya kilichoongezwa na kamati kama kitakubaliwa kinasomeka. *“Kifungu cha 25 Mtu yoyote atakayepatikana na hatia chini ya sheria hii na kanuni zilizotungwa.”*

Sasa Mhe. Naibu Spika, nilikuwa napata mashaka kidogo mimi ninavyojua kanuni zimewekwa kufafanua mambo ambayo yamo ndani ya sheria, lakini ku-*introduce* mambo mengine mapya, na suala la kuweka makosa katika sheria ni imani yangu chombo chenye mamlaka ya kufanya hivyo ni baraza hili tukufu. Lakini siamini kanuni ambazo zinatungwa na Waziri kwamba zinapaswa kupewa nafasi kwa waziri kuja kuweka makosa mengine kuliko vile ambavyo inatarajiwa sheria hii.

Sasa tukivikubali vifungu vya 23 kama kilivyo sasa na kifungu cha 25 kilichopendekezwa na kamati vikaendelea kuwepo, kwamba kutakuwa na makosa chini ya sheria hii na kanuni ambazo zinatungwa na waziri tutakuwa tunampa madaraka makubwa sana Mhe. Waziri kwamba anaweza kuweka makosa ambayo yatamtia mtu hatiyani, mimi nadhani tutakuwa tunampa waziri madaraka makubwa ambayo ni mamlaka ya chombo hichi hapa. Kwa hivyo hivyo Mhe. Waziri angepaswa awe na nafasi yake ya kutunga kanuni lakini zikawa za tafsiri kama ilivyo kawaida utekelezaji wa sheria hii na sio kutunga vitu vyengine ambavyo viko nje, hasa katika maeneo ya kuweka makosa na adhabu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kidogo kwa kuingia katika jaduweli ambalo liko katika ukurasa wa 258 mpaka 259. Kwanza katika kifungu cha nane cha jaduweli ukurasa wa 259 naomba palipoandikwa nusu ya idadi ya wajumbe wote itafanya kije kikao cha bodi, isomeke zaidi ya nusu. Koram siku zote ni zaidi ya nusu ya wajumbe kwa hivyo pale tuongeze maneno zaidi ya nusu ya wajumbe kufanya kile kikao cha bodi.

Lakini hapo hapo Mhe. Naibu Spika, nieleze nafsi yangu juu ya kifungu cha kumi na moja ambacho kwa maoni ya haraka haraka ni kifungu cha 2 katika sheria mbili tofauti ambazo zimeletwa katika baraza lako katika mkutano huu unaoendelea, kifungu hiki kinazuangumzia Mwenyekiti na wajumbe wengine wa bodi watalipwa posho na malipo mengine kwa kiwango kama atakavyoamua waziri, katika sheria ya Mkemia Mkuu iliyopitishwa Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa na kifungu kama hicho kwamba wajumbe wa bodi ile ya Ushauri ya Mkemia Mkuu watalipwa posho kama takavyoamua Waziri.

Mimi kidogo ukatibu unanipa mashaka kwa sababu nadhani hata katika binasi basi viwango vya posho vinaamuliwa na bodi za kampuni kaatika sekta za binafsi, seuze kwa serikali inaonekana *trend* inaanzishwa ya kwamba yeye ndiye ana *determine* malipo ya posho na malipo mengin, viwango vyake anaviamua yeye. Nadhani hii nayo vile vile tunatoa madaraka makubwa sana kwa mawaziri katika nchi. Mhe. Spika, nadhani hili tunapaswa kulirekebisha.

Mimi nilikuwa nataka kupendekeza kwa *trend* hiyo ambayo inaonekana inajitokeza. Tungeweka utaratibu wa serikali kuwa na muungozo kwa vyombo vyake. Ikiwa mashirika, ikiwa taasisi kama hizi za Mkemia Mkuu, ambazo zitawaongoza ulipaji wa posho au mafao mengine yoyote ambayo yataonekana wanapaswa kupewa. Ili ijulikane kwamba kuna fomula fulani, kuliko utaratibu huu ambao tunaokwenda nao sasa. Unaonekana unampa waziri nafasi ya kuamua posho kama hizi na unaweza utaratibu kama huo ukatumika vibaya katika shughuli za serikali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo niseme kwa jumla maeneo mengine ya Mswada sina matatizo nayo. Liko suala moja tu la mwisho kabisa naomba niliseme.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi nyingi duniani sasa hivi, ambapo serikali zinaona umuhimu wa kuwekeza kwenye kujiongezea mapato na kulinda wananchi wake na uchumi wake. Kumekuwa kuna utaratibu wa kuanzishwa *Sovereign Wealth Fund*. Mfuko ambao unaweka hakiba fulani ya mapato ya nchi ambayo yanaweza kutumika katika uwekezaji. Lakini mara nyengine yanapotokezea matatizo kwa mfano kama haya tuliyokuwa tunayo sasa hivi za mfumko wa bei za vitu katika nchi. Serikali inaweza kutumia mfuko kama huo ikaingiza fedha fulani katika katika eneo fulani ili kupunguza makali kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi za wenzetu wenye madini, wamekuwa wakitenga fedha au mapato yanayotokana na madini kuanzisha. *Sovereign Wealth Fund*. Naamini Ishallah Zanzibar itakapoanza kuchimba mafuta muda mrefu baada ya Mhe. Shamuhuna kufanya kazi yetu ya kuhakikisha suala la mafuta linaondolewa katika suala la Muungano. Tutaanzisha *Sovereign Wealth Fund* kwa ajili ya kuchukua mapato yanayotokana na mafuta kiasi fulani kuweka huko ili yatumike katika uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, nchi kama Singapore zimefaidika sana na mfuko kama huu, Malaysia na nchini nyengine nyingi. Sasa kwa kwetu sasa hivi hatujaanza kuchimba mafuta kwa sababu ndugu zetu wa damu hawajataka tuchimbe bado. Lakini kwa hili ambalo

tunauwezo nalo ambalo la karafuu nilikuwa nadhani katika hali kama hii tuliyonayo ambayo ya bei imepanda vizuri. Si vibaya serikali ikafikiria kuanzisha utaratibu au kutuletea sheria baadaye ya kuwa na *Sovereign Wealth Fund* kupitia kwa Waziri anayehusika na mambo ya fedha ili kukawa kunatengwa mapato kama haya yakasaidia nchi yetu kwa siku za baadaye.

Mhe. Spika, baada ya hayo, kama nilivyosema nitaunga mkono hoja baada ya kuridhishwa juu ya hoja ambazo nimezitoa. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai, uzima na taufiqi ya kuzungumza.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijachangia ndani ya Mswada wenyewe kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa kuamua kuuleta Mswada huu katika kipindi hichi. Ili kazi na madhumuni ya hili shirika yaweza kufahamika.

Napenda kusema kwamba mkarafuu na mikarafuu ni mali ya watu mbali mbali ndani ya nchi hii, haimilikiwi na serikali. Yapo mashamba yanayoitwa ya serikali ndio yanayomilikiwa na serikali, lakini mikarafuu inamilikiwa na watu wenyewe binafsi waliyoipata miaka mbali mbali kwa nguvu zao na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ikakuwa mikarafuu ile na wanachuma mazao yao. Pamoja na mipango yetu mingi tunayoipangia, tuamini kwamba wananchi wenyewe ndio wanaomiliki mikarafuu na sio serekali kama inavyochukuliwa.

Magendo ambayo yanazungumzwa sana yalisababishwa katika vipindi mbali mbali na dharau iliyofanywa na Shirika la ZSTC kwa zao la karafuu. Ikiwa ilikuwa ikiuza nje kwa bei wanayoipata au sivyo. Lakini wananchi walikuwa hawanufaiki na bei ya zao la karafuu. Ilifika wakati wananchi wakasema bora upande mbirimbi kwa sababu utapata achari kuliko kuwa na karafuu. Umefika wakati tumeamua kwamba sasa karafuu ina maana basi ni lazima tufate vile vile na haki za binaadamu na tuwachukulie kwamba wale wenye mikarafuu ni yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wewe ulikuwepo katika kipindi kilichopita, tulifika wakati humu sekta kiongozi iliitwa utalii na sisi tukapiga kelele sana. Uralii haiwezi kuwa sekta kiongozi. Matokeo yake yameonekana. Kwa ufupisho huo naomba serikali iangalie taratibu zetu za uchumaji wa karafuu na mipango inayohusiana na hayo. Karafuu mbichi isipewe uzito sawa na karafuu kavu iliyokuwa karafuu haijachambuliwa.

Wananchi wengi wamerithi mikarafuu uyao 10, 15 katika maeneo mbali mbali, lakini wakienda akichuma karafuu na kuzichukua wanapoishi, wanakamatwa na askari na kupatiwa adhabu mbali mbali. Hii si haki wanayofanyiwa. Kama wanaosafirisha ni karafuu kavu pale inajulikana, lakini karafuu wanaianza kuichuma anakwenda anapoishi anakwenda kuichambua, anakamatwa. Pamoja na kuzuia lakini mikarafuu ni yao wananchi, sio ya serikali. Hilo la mwanzo.

La pili tunashukuru serikali kupitia Wizara ya Biashara imeona haja ya kuangalia bei ya karafuu katika soko la dunia na kuwapa wananchi uwezo zaidi wa kuuza karafuu zao ZSTC. Sisi Wawakilishi karibu wote kama sio wote tuliyokuwepo Pemba tumefanya kazi ya kuwaelimisha wananchi wetu na wameitikia. Juu ya serikali sasa kuwatizama wale wasafirishaji na sio wananchi mmoja mmoja mwenye mkarafuu. Kwa sababu wasafirishaji wanajulikana na wanaowasaidia wanajulikana, mpaka vyombo vya ulinzi vilikuwemo au vimo katika kuwasaidia. Kwa nini wanakwenda kusumbuliwa wananchi moja mmoja mwenye kipakacha chake, wakati wale mang'weng'we wanajulika. Tani 2000 atazipataje mwananchi kama hawakuingia vigogo waliokuwa na pesa, wakati huo pesa ilikuwa hakuna. Kwa hivyo tunapoendelea kuliimarisha hili zao tusilete usumbufu mpaka wale wananchi wakachukia. Baada ya hayo naomba sasa niingie katika Mswada wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nikianza sehemu ya mwanzo. Mimi kidogo napata mashaka na tafsiri ya Shirika. Kwa sababu unaposema mazao ya kilimo bila ya kufafanua kilimo kipi? Muhogo nao umohumo, utashughulikiwa na ZSTC. Hakuna *close* ya kuingiza mazao ya kilimo ya biashara. Lakini pia sisi Zanzibar hatuna ardhi tu, ardhi yetu ni ndogo kuliko bahari. Je, mazao ya baharini hayamo katika biashara. Ina maana mwani unaendelea kusafirishwa hivyo hivyo bila ya kutizamwa nao kama unamaslahi na mazao mengine ya baharini.

Tukija tukifanya uvivi wa Bahari Kuu hatujaweka kipengele chochote, tena tuje na sheria nyengine ya kuanzisha shirika la kusafirisha samaki sasa. Mbona tunaishukua kama ile tafsiri ni finyu. Tumeanzisha Shirika la kununua na kusafirisha bidhaa, lakini tumeiweka finyu. Au wale Wizara ya Biashara ndio watakaosafirisha sasa, Wizara ya mifugo na Uvuvi, wizara ya vitoweo, ndiyo itakayosafirisha samaki. Kwa hivyo kwa sababu tunaleta sheria tungekaa kitako tukakubaliana serikali yote mustakbali ya miaka 10, miaka 15 ijayo ni vipi. Ili tukatunga sheria ambayo itaingiza mambo yote kwa jumla.

Hapa pamezungumzwa karafuu tu peke yake mika 10 iliyopita mbata zilikuwa zikisafirishwa na mafuta ya nazi, tumeshavunjika moyo? Hatuna tena zao hili? Au limeshatolewa? Karibuni tulianza kutoa karafuu, tukaupa utalii. Sasa karafuu tumezirudisha tena lakini tunasahau nazi sasa. Je hatuna tena muelekeo wa kuimarisha zao la nazi, hata ikawa nazi haikutajwa tena humu? Hilo ndilo suala jengine.

Suala la pili katika hichi kifungu cha (2) Sehemu ya Pili, hebu tuangalie Mhe. Naibu Spika. Kifungu namba 7 na kifungu namba 9 mbona yamerudiwa mambo yale yale. Huu Mswada umefanywa mkubwa kifungu nam. 7 kimesema "kazi za Shirika" kifungu nam. 9 kimesema "Uwezo wa Shirika" lakini mambo ni yale yale, kupanga bei, kununua, kusafirisha, kuweka. Sisi tutauchukulia hivyo hivyo lakini tujue kwamba mambo yamerusiwa rudiwa bila ya ulazima.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kifungu nam. 9 ambacho kimezungumza mambo kwa ufupi yaliyokwisha kuzungumzwa katika kifungu nam. 7. Miye vile vile sikubaliani na wazo kwamba ZSTC iitwe muuzaji au msafirishaji pekee wa zao la karafuu. Mimi sikubaliani nalo. Kwa sababu tunaweka sera huku nyuma ya uhuru wa biashara *trend*

labialization ambayo ni ya ulimwengu. Kwa nini sisi tuchague zao moja tu katika mazao yote tuyawekwe kwamba sio huru hili. Lakini mazo mengine yote tuyaweke kwamba huru. Ni sababu ipi, nilisema pale mwanzo kwamba zao la karafuu kama ingelikuwa ile mikarafuu yote ni ya serikali basi tungelikuwa tupo sawa kusema ZSTC ndio pekee. Kwa sasa ZSTC ndio pekee kwa chombo cha serikali, ndani ya serikali hatuwezi tena kuanzishwa chombo chengine cha kununua na kuuza karafuu, kinachonunua kwa niaba ya serikali. Lakini ikiwa ni hivi mimi sikubaliani nalo hilo.

Mhe. Naibu Spika, hii inadhirisha wazi, naamini miaka mitatu iliyopita ulinzi ulikuwa mkali zaidi kuliko mwaka huu kule Pemba. Hiyo nakuhakikishia. Kwa sababu hapa tulikuja tukaletewa maelezo kwamba zimetumika fedha nyingi sana za ulinzi katika miaka mitatu, mine iliyopita. Mara hii ile bugudha tu imekuwa nyingi lakini ulinzi ni mdogo. Watu wengi wenyewe wameridhika kwenda kuuza kwenye ZSTC. Ukiwauliza utajua, sasa tunaogopa nini kuweka hichi kifungu wazi? Kama alivyosema mchangiaji wa mwanzo kwamba katika bei zinazoshindana, zinashindana na nani? Ikiwa ZSTC ni peke yake, tena bei hiyo ya kushindana anashindana na nani na hewa? Ikiwa bei za kushindana awe yupo huyo mshindani, ukiwa hayupo unashindana na nini. Lazima zile jumla ziowane, tukisema bei za kushindana awepo huyo mshindani.

Kwa hivyo katika sheria tuanze kumuweka. Hayupo sasa hivi lakini tuanze kumuweka katika sheria, ZSTC ni mnunuzi na msafirishaji wa karafuu kwa niaba ya serikali. Sasa akitokezea wa binafsi atapewa masharti yake ya serikali, jenga afisi hii, toa ushuru huu, jengo liwe na viyoo na choo kiwemo, pahali pa kupitia pawe hivi, meza iwe ya *electronic*, atapewa masharti yote, atayafuata, atanunua. Lakini ni lazima awepo katika sheria tokea mwanzo, kwamba kuwepo na *close* ambayo inamruhusu mnunuzi binafsi kuchukua nafasi. Kifungu hiki kama hakijarekebishwa mimi peke yangu nitanyanyua mkono sikitaki. Nikipata na wenzangu nawashawishi kwamba kifungu hiki tusikitake kabisa.

Katika kifungu nam. 9(d) kimeandikwa kupanga bei ya kununulia karafuu na mazao mengine ya kilimo. Mimi hiki kilivyo sikubaliani nacho. Mpaka kifungu hicho kiseme kulingana na bei ya soko la dunia. Kama serikali itakubaliana 80 na wananchi watakubali ndiyo hivyo. Tatizo lililotupata huko nyuma mpaka Kenya wakatuweza. Kwanza nilikwambieni kwamba miye nilifuatilia huko Kenye mwanzo kulikuwa hakuna wanunuzi. Ikawa sisi tunakwenda kuwalazimisha kwa sababu ndio wanakwenda wananchi wetu wanauza wananunua na bidhaa wanapata faida zaidi. *Transaction* ile ikaendelea mpaka wakahisi kwamba kumbe hii ni biashara nzuri, ndio wakaanza kununua kwa wingi. Lakini tumeilazimisha Kenya kununua karafuu kwa sababu ya bei ndogo iliyokuwepo na usumbufu uliyokuwepo.

Kwa hivyo tukijirudia kama hivi wananchi tulivyokwisha kuwaeleza na wakafahamu tuki *maintain* ile, yoyote atakayekuja, akija Waziri Shekhe Nassor, akija Waziri Shekhe Ali, Akija Waziri Shekhe Saidi, lakini anajua tunalingana na nini na soko la dunia. Sio *perspective* kwamba tunapanga bei, laaa. Tunapanga bei kwa mujibu wa soko la dunia, iwepo katika *close* ndani ya mswada huu.

Nashukuru kwamba Kamati imekiona kifungu cha 9(f) lakini mimi nilikuwa nina wazo jengine. Nilikuwa nafikiria kwamba kwa vile biashara ni huria na tumeikubali hiyo sera ya kidunia, sheria hii nayo imepitwa na wakati. Sheria hii ilikuwa ilete sheria kwa mujibu wa kifungu hiki Sheria Nam. 11ya mwaka 1989 kuhusu zao la karafuu imefutwa. Itaendelea lini? Hapa pana mambo mawili, kuna kukamatwa ya kusafirishwa na kukamatwa ipo ndani inahifadhiwa.

Sasa mtu atakamatwajwe na karafuu aliyoihifadhi ndani wakati tunasema sisi tunge utamaduni wetu, au tuuhifadhi utamaduni wetu. Ni watu wangapi waliyo na kanga ndani ambazo siku nyingi hajazivaa, mbona mtu haambiwi madhali huivai ukaitoe. Kwa sababu kaiweka hakiba. Ni wangapi wanaojiweza wana dhahabu kwa nini hawaambiwi madhali wewe huitumii sasa ipeleke dukani kwa sonara, huna haki ya kukaa na dhahabu na mambo mengineyo. Basi huyu mtu aliyeweka kigunia chake kimoja, hajaweka ghala, kaweka ili akitokezewa na wakati wa shida auze. Wewe unakwenda kumwambia lazima ukauze ZSTC. Tena mbaya zaidi hivyo inavyofanywa wanaonewa huruma kidogo naona. Hapa katika sheria inasema kwamba itataifishwa kwa mtu aliyeweka karafuu zake ndani. Mambo mengine yalikuwa ya kimapinduzi ni lazima tuyatizame sasa hivi. Hali tunayokwenda nayo ya kidunia. Wananchi wetu hawatayafahamu.

Mhe. Naibu Spika, sheria ni nzuri ukiacha mambo hayo kwamba tuwe na shirika ambalo linajiendesha, linajitegemea, linajulikana, linatoa hesabu zake, linatoa hasara zake, linatoa maendesho yake, hiyo ndio sheria. Hapa kuna kazi moja, Wizara ya Biashara mara nyingi ninavyouliza suali hili wanalikwepa.

Mhe. Naibu Spika, moja katika shughuli kubwa inayofanywa duniani na viongozi ni kuwahakikishia chakula watu wake. Hata juzi ulivyofanyika mkutano wa ZBC nimemsikia Mhe. Rais analizungumza *food security*. Moja katika sababu mbili za kuweka ghala ya akiba kwanza lipo katika Wizara ya Kilimo ni kuwa watu wameharibikiwa na mazo yao kwa hivyo wanapewa hakiba ya chakula iliyomo. Mfano kumeingiwa mafuriko mazao hayakupatikana, ukame mazao hayakupatikana, watu wanapewa chakula cha hakiba iliyo katika ghala ya akiba.

Pamoja na kuwa Mswada ule umeletwa na Wizara ya Kilimo, kuna *aspect* ya pili kuweka ghala ya akiba wanasema ni kuweka wastani wa bei. Kwa mfano inatarajiwa ikiwa ni serikali, ikiwa ni ZSTC, ikiwa ni Wizara ya Biashara, inunue mchele ambao tunatumia kwa wingi. Katika hali ile mchele unapokuwa bei nzuri duniani. Mchele ule utakapopanda bei badala ya kuwategemea wafanyabiashara ule ndio unaouzwa sasa kwa sababu watu wetu wa chini hawawezi kumudu kununua basmati unaoliwa na matajiri, utanunua huu huu mchele wa kati na kati au wa chini itaweka.

Sikuona humu kama ZSTC imeachiwa jukumu la kushiriki katika ghala ya akiba na hili ndilo Shirika la Biashara. Kwa hivyo mimi nilikuwa nauliza Mhe. Waziri, je, *close* ile serikalini mmekubaliana vipi? Hebu uje utueleze. Kwamba hakuna *component*. Mhe. Waziri wa Kilimo aliponijibu suala langu katika mchango wangu alikiri kwamba moja katika suala muhimu la kuweka ghala ya akiba ni kueka wastani wa bei wakati bei zinapopanda katika dunia. Suala hili linajitokeza mara kwa mara sasa hivi kwa sababu

huko kunakolimwa mchele mara hutokezea mafuriko, mara kunatokezea hili. Sahivi hili ni suala muhimu. Watu wetu wanalalamika sana hatujawa na ghala ya akiba mpaka sasa hivi. Lakini hapo itakapopatikana ni nini *role* ya ZSTC katika hili kuweka ghala ya akiba.

Mhe. Naibu Spika, naingia sehemu ya tatu sehemu ya mwisho nayo ni Uongozi wa Shirika. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba Mswada umefupizika kidogo, kwa kutaja mtu mmoja tu. Hakuna uongozi wa mtu mmoja *at list* tungetajiwa watu watatu wa juu. Shirika linahitaji watu watatu, mmoja ndio anakuwa kiongozi, wawili wanakuwa chini yake. Lazina wangekuwa wanatajwa katika Mswada. Baada ya *managing director,* meneja muhimu kabisa katika masoko ni wawili nao ni meneja masoko na meneja wa uzalishaji. Tumeshasema humu maneno mengi tutaingiza, tutafanya ubora, tutazalisha, huyu meneja masoko ndio atakayeshughulikia mambo yote yale ya masoko na kuongeza thamani na mambo mengine. Lakini meneja uzalishaji je? Mara hii tunataka meneja uzalishaji awepo Pemba. Kwa sababu Pemba inazaidi ya asilimia 80 ya karafuu zinazozalishwa awe kituo chake ni Pemba. Hatutaki meneja uzalishaji tukamuona Maisara, aondoke Maisara tumuone Wete au Chakechake au Mkoani awepo. Hapo ndio tutajua kwamba mmekuwa *serious* na zao la karafuu. Lakini meneja uzalishaji anakaa huku anapiga simu tu, ‘mikarafuu iko vipi huko’, aaa hiyo hatutaki. Meneja wawili hawa watajwe katika Mswada huu.

Zao hili meneja mtendaji peke yake haliwezi. Sio kwenye Bodi tena wanakwenda kusema wanavyotaka wao. Tunasema sisi watungaji sheria tunataka *toop management* itajwe ndani ya sheria nao ni watu watatu. Mimi mawao yangu ni watu watatu, tunataka meneja masoko atajwe na meneja uzalishaji atajwe katika sheria. Lakini wote hao wakiwemo huyo mkurugenzi muendeshaji. Mimi sikubaliani kwamba wapewe muda. Shirika linakwenda uzuri, hawa ni waajiriwa waendelee na shughuli yao mpaka wakapofikia umri wao wa kustaafu, wastaafu. Unapompangia mtu muda na yeye anajipangia muda vile vile. Eee miye karibu nitaondoka hapa na inategemea na atakayekuja. Kama tunawapa shirika tuwape hili shirika endesheni. Mtu anajua akivurunda ataondolewa kwa kuvurunda kwake. Likitengenea shirika anakwenda mpaka anastaafu muda wake umemaliza. Lakini sio kila baada ya miaka 5 anayekuja ananitizama rafiki yangu gani atakayekwenda kufaidi pale. Ah! Nina shemegi yangu atakwenda pale. Kwa hivyo, Shirika la ZSTC liendeshwe kiutalaamu ili wale waliopo wawe wamepata uzoefu, wamepata kuona hali inavyokwenda hivyo waendelee kama kazi ya serikali inavyokwenda, mtu anafika muda wake wa kustaafu anajuulikana. Kwa hivyo, kifungu cha kumuwekea muda Mkurugenzi atakuwa miaka 5 au mingapi mimi sikubaliani nacho.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo iwapo vifungu vyangu vitarekebisha nitaunga mkono mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika siku hii ya leo tukiwa wazima wa afya. Pili nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi yakusema angalau machache juu ya Mswada huu mzuri wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Shirika la Taifa la Biashara ya mwaka 2011.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mhe. Waziri mwenye dhamana pamoja na wasaidizi wake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuona kwamba sasa wakati umefika ya kuwa na sheria hii. Hiyo ni sifa nzuri kwa sababu binadamu pale anapotambua kwamba kajikwaa akaweza kutafuta namna ya kunyanyuka bila ya kuadhirika. Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu zao tulilitupa muda mrefu, tukayataja mambo kwamba ndio sasa yataunyanyua uchumi wetu na wenyewe nayo hatukuyawekea mashiko madhubuti. Hivyo, hatimae nayo hayafanyi vizuri katika masuala mazima ya uchumi wetu bado malalamiko hadi sasa yanaendelea siku hadi siku, juu ya jinsi gani uchumi unatupiga chenga ndani ya Zanzibar yetu.

Mhe. Naibu Spika, sisi Wawakilishi wa wananchi mara zote huwa tunaendelea kuiambia serikali kwamba hatuna tatizo la uchumi kwani tuna vianzio vingi, tena vinaweza kuzalishwa kwa faida ya watu na maslahi ya nchi hii Wazanzibari nao wakaishi kwa raha na furaha. Lakini bahati mbaya Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tumekumbwa na wimbi hapa, mimi naomba niseme haya na wengine nawaomba wanivumilie kwa sababu huwezi kujenga bila ya kuvunja.

Mhe. Naibu Spika, tumepata wimbi kumbwa la baadhi ya watendaji kutokana na mawazo ya wana siasa, nyengine zina *logic* kwa sababu wenzetu ndio wataalamu, lakini nyengine sio sahihi sana kwa sababu mwenzetu anatwambia kwamba mtungi huu wa gesi ile ya zamani iliyokuwa ikitumika majumbani kwa kupikia nafikiri ilikuwa ina balaa kubwa kuliko hii ya sasa kwani teknolojia ilikuwa bado haijakuwa vizuri. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba mtungi wa gesi unafunguliwa kwa kupeleka ***clockwise***, lakini kumbe unaweza mtungi huu huu ukaufungua kwa kunyanyua tu ule mfuniko.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tunakwama katika kuzalisha vianzio vyetu. Mimi leo nikiuliza hivi kama sheria hii kuanzishwa kwa shirika hili na hilo lilokuwepo limeendelea kungangania karafuu inunue hiyo, iuze hiyo hivyo kuna nini? Lakini mchangiaji wa mwanzo alisema jambo moja kwamba soko linapokuwa jema duniani serikali nadhani ndio hofu kwamba hawataki kulipechua lazima wanunue wao. Mhe. Naibu Spika, mimi nisingelalamika sana, lakini mbona linapoanguka wenyewe wao hawang'ang'anii wakulima wa zao hili, maana *experience* ya duniani nchi nyengine wananunua mazao ya wakulima kwa bei ya juu kabisa halafu wao wakawauzia kwa bei ya tahafifu.

Maana yake ni kuwapa morali na kuwajenga matumaini kwamba serikali yao ipo kwa ajili yao iwe shida au iwe raha ni kwamba wafaidike wote lakini wao athari ya bei isiwaathiri. Nadhani ZSTC sasa kwa sababu bado hamjataka kuliachia zao hili, sisi tunasema serikali haitaki kuyaingia mambo ya biashara tunawaachia watu wenyewe waendeleze biashara. Mhe. Naibu Spika, hii karafuu ni nini hapa? Maana yake huku kulia mnaachia, kushoto mnadhibiti tena kwa nguvu zote. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi bunduki mpaka kwetu kule Chanjaani ziko kwenye mikandaa.

Mhe. Naibu Spika, nyanja za mapato zipo nyingi sana na jana tulikuwa mahali tuliwaomba wataalamu kwamba watupangie namna ya kukaa nao wiki nzima. Hawa wataalamu wetu kwa mambo ya uchumi na hawa waliopo Afisi ya Mhe. Rais kwa sababu

tukitaja kwamba hapa fungu ni dogo hivyo taasisi hii itashindwa kuendesha haya yaliyopangiwa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wanatujibu kuwa sisi kama wawakilishi wa wananchi mamlaka hiyo hatuna, basi angalau tutaje pia na chanzo cha kupatikana fedha ya kuongeza mahali hapo. Mhe. Naibu Spika, leo tunazungumza kwenye chombo hiki kwamba uwezo wa kuwaonesha vyanzo vya mapato tunao.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kwanza waachie karafuu wabinafsishe, kwa sababu serikali imezoea kutaja uchumi wa hesabu kama barabara inajengwa mwezi huu wa kumi mwezi wa kumi na moja viraka huku nyuma vimeshajaa, ukiuliza unaambiwa ndio utamaduni wa barabara za ndani. Mhe. Naibu Spika, wanatudanganya kiasi chote hicho ni kwamba hatufahamu kwamba barabara ina viwango ya mjini iweje na ya kijijini iweje. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba gharama yote hii mikopo inayoingia serikali hatimae barabara zinakuwa mbovu. Mhe. Naibu Spika, nazungumzia barabara ya Kusini Pemba nikamuuliza mtaalamu akaniambia hii ndio nzuri nenda Msumbuji mheshimiwa ukaone. Mhe. Naibu Spika, kweli Msumbuji kuna uchafu ule.

Mhe. Naibu Spika, karafuu nilikataa na leo bado naendelea kukataa kwamba halijapikuliwa hapa kwetu hadi sasa hivi, ni kwamba ni zao tegemezi kabisa kwa uchumi wa visiwa vyetu. Mhe. Naibu Spika, naamini hata serikali inajua hivyo ndio maana ikawa inaling'ang'ania halitaki kulitoa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye kifungu cha 6 kuhusu malengo ya shirika kwamba watatia nguvu, watahamasisha kupata ufanisi wa uzalishaji bora. Mimi nataka niseme kwamba mswada huu umetiwa lugha nyingi sana maneno kamati imefanya kazi siku kidogo, marekebisho mimi nimefanya baadae nimeacha Mhe. Waziri utanisamehe kwa yale ambayo sikuyafikia maana nimeona muda unamaliza na bado. Lakini nasema kuna maneno mengi yanajirudia rudia tafsiri ni ile ile cha msingi ni kwamba sote tunazungumza lugha moja tunafahamu haya yote yanafungwa na neno tu kwamba ZSTC watalisimamia zao hili kuweza kupata mazao bora.

Mhe. Naibu Spika, ZSTC kama ina nia ya kutoa vifaa ama vitendea kazi hapa Mhe. Waziri labda kwa ushauri ni nia njema hiyo, lakini shirika kama litaendelea na kazi moja kubwa kutafuta soko bora. Jambo la pili ni kwamba miti hii tokea ilipoletwa na Sultan huyu aliyeleta kokwa hii ikaota mche, hakuna tafiti za kisayansi zilizoendelea kufanywa na ndio maana tunafika mahali leo misitu ya mkarafuu leo ni jangwa. Mhe. Naibu Spika, kazi kubwa ipo iliyotukabili hapa sio ya ZSTC peke yake lakini tuna haja ya kuendelezwa tafiti za kisayansi kuhakikisha tunarudisha haiba ya mkarafuu unarudi katika visiwa hivi, na sio mkarafuu ule tu ambao wao kuwa mita mia tatu au mia mbili, hapana ni kwamba wataalamu wetu sasa wafanye kazi kama walivyoweza kupata mbegu bora inayozaa vizuri ya mpunga basi tupate mikarafuu angalau iwe na kimo cha wastani.

Mhe. Naibu Spika, haya yaliyoelezwa namna ya kufundisha uvunaji labda sasa tuvune kwa ngazi, kupiga dawa ni sahihi wenzetu mikoroshe kule wanapiga dawa na mambo kama hayo haya yote yatakwenda baada ya kuwa na tafiti endelevu. Mhe. Naibu Spika, sheria inasema katika kazi za shirika kununua na kuuza imetajwa na wenzangu waliotangulia nadhani hapa tukubaliane kwamba tukisema tutambae kwenye kauli zetu,

serikali sio ya kufanya biashara. Serikali imefanya ilipofanya tumeona matokeo yake tulikuwa na biashara ya maduka ya ndani, tukaja bizanje, sijui mashirika ya magari, tukawa tunauza vyarahani mle na baiskeli. Mhe. Naibu Spika, ilimradi yale yote ni mapungufu kwamba serikali sio kazi yake hebu iachie watu wapo wafanye hizi kazi, serikali inakusanya kodi na kodi zitapangwa kwa mujibu wa mapato anayopata huyo mfanyabiashara.

Mhe. Naibu Spika, namwambia Mhe. Waziri kwamba nia ni njema mimi nakuamini kabisa, lakini hebu washauri tena wenzangu kwamba hebu tufike mahali hapa ingesomeka vizuri kuwa na sasa serikali inabinafsisha zao hili. Ni kwamba haiondowi mkono serikali kwa sababu ndio yenye dhamana ya watu wa nchi hii hata kidogo itaendelea kututafutia masoko na kuona kwamba watu wetu hawataabishwi wala hawadhalilishwi katika suala la kuuza na kusafirisha.

Mhe. Naibu Spika, inapostahiki shirika wanasema watatoa msaada wa usarifu, ukusanyaji, upimaji na kadhalika. Ni hakika kwamba tokea tuanze tunasafirisha kwa magunia sana sana tunabadilisha tu ili *quality* ya gunia lakini bado ni maguni. Mhe. Naibu Spika, pengine mahitaji ya soko wengine badala ya kutaka gunia la kilo 50 au 100 anataka kilo 25, kilo 10 hivyo naomba twendeni na utaratibu huo, lakini sio vibaya kutizama kwamba ni *material* ipi itakuwa yakumvutia zaidi mteja wa huko duniani. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tutafute hayo kwa sababu chema chajiuza na kibaya kinajitembeza.

Mhe. Naibu Spika, sasa niseme kwamba teknolojia itumike lakini ndugu yangu Mhe. Waziri unasema kuondosha magendo na vitendo vyengine visivyokubalika, kuzuia au mambo yanayoathiri usambazaji na vitendo vinavyopunguza, uzalishaji maghalani na mengineyo mengi.

Mhe. Naibu Spika, namwambia Mhe. Waziri kwamba ameagiza jeshi kutoka nchi gani na kuja kulinda karafuu ili magendo yasitendeke. Hapa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi serikali imeonesha nia njema kabisa kwani wametafuta soko na soko limepatikana, imeongezwa bei ili mkulima afaidike, anayechuma karafuu na yeye apate, anayesafirisha kutoka pale kwa mkulima kwenda ZSTC na yeye afanikiwe. Lakini kwa ujumla taifa lifaidike na zao hili ni kwamba tatizo bado lipo, kwani magendo yameshamiri.

Mhe. Naibu Spika, tatizo jengine ni kwamba kuna msaada mkubwa wa vyombo vyetu vya ulinzi, mfanya magendo anaaga kwa chombo cha ulinzi kwamba naondoka saa mbili wakati watu wako msikiti sala ya Isha. Mhe. Naibu Spika, anaaga hivyo kwa Kamanda ya Kituo cha Ulinzi Mhe. Waziri kazi ni ngumu sana ya kuzuia magendo nchi hii kwa sababu uadilifu umeshuka katika nyanja zote. Mhe. Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana Mhe. Rais wa Zanzibar ni kwamba Wazanzibari wana imani naye kubwa walimpa ridhaa na wakaonesha imani yao ya kuchagua mfumo gani wanataka kuendesha serikali yao. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba walikuwa na matumaini makubwa lakini tumepata wenzetu ndani ya serikali hawana uadilifu, wana roho dhaifu, wanataka wapate wao peke yao, wenzao hawana haki. Mhe. Naibu Spika, haya yameifikisha nchi hii pabaya sana na

nadhani Waheshimiwa Wajumbe mtakubali kwamba matatizo tunayoyapata na wapiga kura wetu *source* ni watendaji wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, watendaji wa serikali wamepoteza kabisa mwelekeo yanatupata matatizo makubwa sana kwa sababu tuna *limit* ya mambo tunaambiwa kwamba hatuna nafasi ya bajeti kuikataa. Ni kwamba Baraza hili halina meno la kukamata hivyo tunakuta vituko kwenye taasisi za serikali zinavyohujumu mapato, uchumi lakini kwa sababu hatuna meno mambo yanabaki hivyo na tunapokuja tukasema hapa kwamba tunatatizo la harufu mbaya sehemu fulani tunataka twende tuchunguze. Basi serikali inasimama kifua mbele haijashindwa, inajua itasawazisha, kama wanajua kwa nini yafike yanayofika hivi sasa. Mhe. Naibu Spika, haya tunayokutana nayo kwa nini yafike kiasi hiki na serikali ipo mnaona na mnayajua.

Mhe. Naibu Spika, kilio ni kwamba mnatutesa sisi, sisi ndio tunaobeba mizigo, sisi ndio wawakilishi wa watu, hivyo wananchi matumaini yao yote yako kwa wawakilishi wao, serikali iko huko inapita hata tunapowaambia kwamba udhaifu upo hapa huwa hawataki kutuamini. Mhe. Naibu Spika, halafu baadae huwa wanalalamika kwamba serikali haina pesa, pesa hizo zitatoka wapi na wahazitaki. Ni kwamba mnawalinda watu wenu ndio maana uchumi huu haukuwi na hautakuwa maisha, utakuwa kwa kuandika ndani ya makabrasha. Lakini mwananchi naye kujisikia kweli ndani ya Zanzibar kiuchumi sasa haupo huo, hivyo naomba apewe fursa ya kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, namwambia Mhe. Waziri kwamba magendo yanalindwa na vikosi vya ulinzi, karafuu gunia 40 zinapita chini ya miguu ya vikosi vya KMKM hapa hapa. Mhe. Naibu Spika, karafuu zinakamatwa hizo zinazoletwa bandarini huwa zinaletwa zile wanazotaka wao walinzi, lakini waliokuwa na karafuu hawajaletwa hata siku moja wakaambiwa ni hawa hapa. Hivi kweli hatujuulizi kuna nini hapa zile karafuu zikishakutiwa ndani ya jahazi zinakwenda wenyewe? Mhe. Naibu Spika, makubaliano hayakufikiwa unaambiwa nendeni tuachieni sisi wenyewe basi nusu bin nusu wanagawana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema tumepoteza mwelekeo serikali lazima mujitazame tena mnaua huku, watu wana shida kubwa hii pesa ya namna hii ingepatikana basi yangelirahisika mambo, lakini kwa sababu hamtaki kutusikiliza sisi tunaowakilisha watu mnatupa mzigo mkubwa. Nadhani Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tutafute namna gani tuchukue nafasi yetu dhidi ya serikali. Sisi sio wa serikali, sisi ni wa wananchi hivyo tuwatendee haki wananchi wetu na msipotaka kufanya hivyo mjitayarishe na kesho. Mhe. Naibu Spika, mimi hili nalisema kwamba serikali haitaki kwenda sambamba na maoni yetu.

Mhe. Naibu Spika, kukamata na kutaifisha wanakwenda walinzi hawa karafuu bibi yangu ameweka kwenye ubamba wale wanaojua, nyengine anazo mjuu wake ziko kwenye kipolo. Mhe. Naibu Spika, ziko ndani ya nyumba hizo ndio zilizokamatwa zile za kule jahazini zinachukuliwa ukitaka njoo uuze ZSTC analazimishwa hivyo.

Mhe. Naibu Spika, asili yake mkulima wa karafuu huwa anaweka akiba karafuu yake siku ikifika ametokewa jambo anauza anapata pesa kutatua lilomsibu. Mhe. Naibu Spika, wanapofanya hivi kwamba hata ile kokwa ya mwisho akaiuze ZSTC akishapewa pesa hiyo watu wetu huwa hawakai na pesa hizo, utamaduni wa benki huko vijijini tabu watu hawajauelewa kuweka pesa benki anachokiweka ni ile karafuu yake. Mhe. Waziri hili naomba ulifahamu na naomba wafahamishe na hao wenzako.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kusema la mwisho kuhusu uongozi wa Shirika, uteuzi wa Mkurugenzi Mwendeshaji. Waheshimiwa Wajumbe nadhani sasa tumpunguzieni kazi Mhe. Rais si kwa maana haziwezi, lakini apate uhuru wa kuwasimamia hawa tunaowasema. Ni kwamba yanakusanywa matandu, majongoo, vyura vyote anapelekewa Mhe. Rais halafu anapewa jina ameteuliwa na Rais lakini vituko anavyovifanya havistahiki lakini ana nembo ya Rais. Kwa hivyo, hebu tutafuteni utaratibu kumvua Rais haya mengine anafanya vurugu basi iwe hapana kutumika lile jina la Rais kwani Rais ni mtu mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, tumekuja tukasema hapa jamani mahali hapa tuna tatizo hili lakini kwa sababu ni mteule wa Rais tukaambiwa tume hii tayari serikali wameshaunda na ripoti italetwa, serikali haijashindwa mpaka hivi sasa imeshindwa na tunafahamu kwamba ripoti ya tume ipo imeshaletwa lakini imedhibitiwa sababu wanazijua wenyewe. Mhe. Naibu Spika, ni kwa sababu huyu ni mtu wa Rais sasa hebu tutafuteni namna Rais apate nafasi nzuri yakuwasimamia hawa watu wa namna hii kwa sababu akishapata jina la uteuzi wa Rais basi wengine hawana nafasi ya kumkaribia hata kwa mkono.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nimalize kuna kipengele kinasema huyo Mkurugenzi Mwendeshaji awe Mzanzibari. Nzuri, na ndivyo ilivyo, na mimi nafurahia hilo, lakini kusema ni jambo jengine na tatizo kubwa tulilonalo hapa Zanzibar ni utekelezaji, utekelezaji wa tunayoyasema na utekelezaji wa sheria zetu. Kwa sababu tuna sheria humu kama tutakuja siku moja tukae tuzipitie siajabu tukazirudia hizo hizo, siajabu nasema. Utekelezaji ni tatizo na sasa nisisikie kusema ni kilema, lakini nasema ni tatizo kubwa sijui kwa nini.

Pale Darajani wale wenzetu wauza mikate, vitu vya mikononi vidogo vidogo marufuku sheria hiyo, lakini muuza mayai askari wa Manispaa anamfukuza mayai yake anayakanyaga, anavuruga, umasikini anamuachia pale. Kuna mmoja wao kapewa leseni ukipita ana miwani na kofia la mapembe mana anawaona wote wale si lolote si chochote, kapewa leseni na Manispaa wale Wazanzibari *menu*(halisi) wapo pale wanazalilishwa na wenzao, nina mashaka na hapa napo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tutakuja kukusuta vibaya mno, maandiko yapo yatakushtaki lakini na sisi kama tungalipo tutakuuliza kwa lugha ngumu kwa sababu yasemwayo na yaandikwayo sio yafanywayo. Hayo ni matatizo, tuna tabia mbaya sana.

Waheshimiwa Wajumbe wenzangu nakuombeni kwa heshima kubwa kwanza tutafuteni jinsi ya rais wetu awe mweupe, safi kagandamizwa na watu wa namna hii balaa, watu

wanapoteza imani sasa na serikali, tabu tupu maisha mabaya kila siku yanazidi ugumu. Rais anawekewa watu mtihani mtupu hawajui wote anapelekewa tu.

Mhe. Naibu Spika, hali yangu si nzuri nakuomba kwa heshima zote unisamehe na wajumbe mnisamehe.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa hali mbaya namna hiyo je ingekuwa nzuri ingekuwaje?

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa ajili ya kuchangia mswada huu. Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake ambao wamechambua baadhi ya mambo. Lakini kwa sababu mswada huu unasema kwamba, Shirika la Biashara pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Mimi nitachangia kwa jumla Mhe. Naibu Spika.

Kwanza kabisa nichukue nafasi hii nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, jinsi alivyokipa kipaumbele kilimo chetu cha zao la karafuu, ametia moyo na wananchi kwa kweli wamelipokea kwa furaha na amani kabisa suala hili, lakini penye mema makasoro hayakosi.

Mimi nasema tubadilike Mhe. Naibu Spika, sasa hivi ni wakati wa kubadilika tusikae pale pale. Nadhani si vibaya zao letu hili la karafuu tukarudia baadhi ya mambo ya zamani ambayo yalikuwa ni mazuri. Zamani walikuwa wenye mashamba ya karafuu wanakopeshwa pesa za kulimia mashamba halafu baadae wanakatwa wanapopeleka karafuu na kulikuwa na orodha maalum turudie hili suala. Kwa sababu tunajua wananchi wetu umasikini wao na bado hatujaweza kuutekeleza kuwasaidia kutokana na umasikini huu. Suala hili namuomba Mhe. Waziri alipeleke serikalini ili wananchi wetu wenye mashamba ya karafuu wakopeshwe pesa za ulimiaji mikarafuu yao.

Lakini si hilo tu Mhe. Naibu Spika, nimeseme kwa nini tubadilike tuna matatizo sisi, kwamba yule anayechuma basi huwa hapewi chochote, hili zao la karafuu tusiache mbachao kwa msala upitao. Zao la karafuu ndilo lililotufanya tukajenga nyumba za Michenzani lazima tulipe heshima yake ndilo lililoendesha Serikali hii ya Mapinduzi toka enzi za Ukoloni lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, ni vyema tukakaa tukapanga mipango yetu kuhakikisha kwamba karafuu ndio zao kubwa la kuendesha serikali yetu. Hilo moja.

Jengine kwa nini hizi karafuu ndizo zinazoichumia serikali na hatutafuti vyombo vya doria pesa hii ya karafuu ikatumiwa kwa vyombo hivyo halafu tunakaa tukalaumiana sisi wenyewe kwa wenyewe. Ni vizuri kwa sababu karafuu inaingiza fedha naiomba serikali kwamba fedha maalum zitengwe za kununulia vyombo vya doria. Kwa sababu wakati mwengine tunafanya mambo sisi wenyewe tunajitia hatiani, ni lazima tupange mipango yetu inayotekelezeka.

Wenzangu wamenifilisi sana hapa kuhusu suala hili la karafuu, lakini mimi nitachangia kwa jumla kama nilivyosema hebu tubadilike Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Nakubaliana na msemaji aliyepita fedha tumezikalia, fedha ziko nje lakini tumezikalia kwa sababu sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio tunaokwenda kusimamia huko na ndio tunaokagua wizara zote tunaona mazambi mengine hayasemeki, halafu tunasema hatuna fedha. Wallahi nchi hii watu milioni moja tunaweza tukawalisha na wasipate tabu kwa pesa iliyopo nchi hii, tunashindwa na China watu bilioni sasa hivi wanategemewa na ulimwengu mzima. Mimi naiomba serikali ikae, ipange mipango yake tuhakikishe kila mwananchi wa nchi hii hapati shida na tunao uwezo huo.

Mhe. Naibu Spika, nimesema haya kwa makusudi tuna wataalamu wengi, watendaji wengi lakini wao wanangojea Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waone pesa iliyopo sasa ya nini kuweka wataalamu basi tusingetumiwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tukaionesha serikali pesa hii hapa tafuteni.

Nasema haya Mhe. Naibu Spika, kwa ushahidi, sijisemei tu, kwa sababu najua hapa ni pahala pakubwa, pesa tunazo Wazanzibari lakini tumezikalia. Naiomba sana serikali, mimi naungana mkono na mwenzangu, rais tusimlaumu, rais anamteuwa mtu kwa amani kabisa, kwamba anaona atamsaidia matokeo yake hamsaidii. Na sisi tuko tayari wengine kuwafichua lakini ndio yale aliyoyasema mwenzangu hapa kwamba ukifichua jambo la serikali limemgusa mtu mkubwa itaundwa tume na tume haiwajibiki, hatutofika naomba tubadilike kama rais mwenyewe alivyosema tubadilike basi tubadilike.

Nasema tena tubadilike Mhe. Waziri, kule kwetu Pemba embe zinaozeana tu, kila mwaka tukisimama hapa tunazungumzia suala hili kwamba kwa nini hakutafutwi mbinu za kuwepo viwanda vidogo vidogo vya kuhifadhia embe jamani? Sio pesa hiyo kitu gani? Pesa hiyo. Mabungo hakuna juisi dunia nzima nzuri kama juisi ya bungo.

Mhe. Naibu spika, mimi mwaka 1986 nilikimbiza mwenye wa kimataifa wa amani duniani, basi wale wazungu tukaenda nao Pemba na Maalim Seif Sharif alikuwa ndiye Waziri Kiongozi, waliuliza juisi hii ni juisi ya aina gani? Ni pesa tumeikalia.

Lakini jengine tubadilike Mhe. Waziri. Mimi nadhani maduka tunasema fedha hatuipati tutaipata vipi na hatujataka kubadilika? Tuchukue mifano wenzetu Kenya kila duka unalokwenda kuna mashine na lazima watu wetu tuwazoweshe, tuanze kuwaambia sasa hivi hii ni fedha nyingi sana tunaikosa katika maduka ya biashara Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ukishakuwa na mashine na serikali ikijipanga fedha anayonunua mteja pale inajiandika huko huko hesabu yake hakuna tena mambo ya kuchukua mifukoni, kwa sababu pesa zinatiwa mifukoni.

Kuna maduka mengine hata leseni hayana wanapita watu wakikusanya ndio chakula chao. Mimi nadhani serikali tukae tupange lipi la kwanza, lipi la pili, lipi la tatu. Ama kuandika kwenye karatasi kwa sababu toka juzi tulikuwa na semina yameandikwa mambo mazuri sana utaona sasa hivi Zanzibar itakuwa *paradise*. Lakini yatizame yale yaliyoandikwa je, uwajibikaji upo, utekelezwaji upo? Hakuna kitu. Sisi Wazanzibari leo si wa kuwa hivi, toka tulikuwa watu laki tano sijui, laki tatu mpaka sasa hivi milioni moja laki tatu.

Mimi nadhani tumsaidie rais na kumsaidia kwake rais kwanza ni kuwa na imani ya roho, mshikamano, mashirikiano, umoja ndio huzaa amani na amani tumeipata jamani, tulikuwa hali mbaya lazima tuzungumze. Tulikuwa tunachinjana ovyo, tunahasimiana hatuzikani kwa kitu ambacho Mwenyezi Mungu alisema nyinyi nataka kukurudisheni muwe wamoja kama zamani na Mwenyezi Mungu katurejesha sasa kipi ambacho kinatufanya nchi hii isipate maendeleo? Kuna baadhi wana roho dhaifu lazima tukubali, wanapewa nyadhifa lakini roho zao dhaifu wameweka kitu mbele hawatizami maslahi ya nchi na wananchi.

Mimi naiomba sana serikali sisi wengine hakuna kitu kizuri kama kuwa na uzalendo, kama huna uzalendo huwezi kufanya kitu kizuri. Sisi wengine tuna uzalendo wa nchi hii kwa sababu hatuna pengine pa kwenda, jana nilisema kwenye semina, hatuna pengine kwetu ni Zanzibar, kwa hivyo uzalendo tunachokisema tunasema kwa uchungu hatusemi tuonekane kwamba tunasema wananchi watusikie tunasema kwa uchungu. Hii nchi bwana haitojengwa na Mjerumani, Muingereza wala Mmarekani nchi hii itajengwa na Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nimechangia na nilisema kwamba nichangie kwa pamoja. Kwa sababu lazima serikali ikubali kwamba sisi ndio wanasiasa wa nchi hii, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na sisi ni chombo kikubwa, mimi Mhe. Naibu Spika, tunakaa na watu wengi tu, sisi tunaonekana si lolote si chochote Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tunaonekana kama tunakula pesa za serikali. Tumshukuru sana Mhe. Aboud Jumbe kuunda chombo hiki, lakini nasema Mhe. Waziri kaeni mupange tena mipango! maana yake nataka niseme neno sina uhakikanalo, *ZSTC* mimi imenitoa amani utalipanga vipi tena? Mtalipanga upya au mtalifanyaje mpaka kiwe chombo kizuri kweli. Lazima tusimamie mambo yetu na mwanasiasa ndio wewe waziri usimamie watendaji wako.

Mhe. Naibu Spika, lazima tuzungumze, kuna mawaziri wengine watendaji hawawaambii yale mambo muhimu wanayachukua wao wanayaficha kisha wanafanya yao. Hayo yote tumeyaona katika ziara zetu. Sasa niseme kwamba nawaomba sana watendaji wawajibike ipasavyo, sikusudii mtu kuacha kazi, lakini kuwajibika ni kupenda kazi yake na kama huipendi kazi yako basi huwezi ukafanya kazi, lazika kwanza uipende kazi yako halafu baadae ndio unaweza kuifanya kazi yako vizuri. Naiomba sana serikali itupie macho, baadhi ya watendaji siwo.

Mimi naungana mkono moja kwa moja na Mhe. Assaa kwa sababu sisi ndio tunayaona, baadhi ya watendaji siwo, na tuache kupeleka mtoto wa shangazi na mjomba! mtoto wa baba mkubwa na baba mdogo! tuache tabia hizi tumshauri rais vizuri, tunampaka matope rais kwa ajili ya matakwa ya mtu, hebu tubadilike kama alivyosema mwenyewe hawezi kazi apishe wenzake wanaoweza kutumikia nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, leo nimekuwa mkali kwa sababu nina uchungu, nasema haya kwa uchungu kabisa. Tunamdhalilisha rais wetu wakati ana nia safi na mawaziri wake na watendaji wake wote aliopelekewa akaambiwa huyu anafaa, huyu anafaa, kwa sababu

anashauriwa lakini wengine anaoshauriwa siwo na mimi naunga mkono. Baadhi ya watendaji tusimsukumizie tu rais kateuwa tunamfedhehesha, tuangalie hali halisi.

Mimi nasema tuanze sasa hivi kufanya tathmini kila wizara, kila baada ya kipindi cha mwaka kimefanya nini, kimewajibika nini na kwa nini hakikuwajibika, tatizo tulilonalo hatufanyi tathmini mambo yetu. Tunaweza kuanzisha kitu kwa hamu na halafu tukaibua kitu chengine cha mamilioni kile tulichokianzisha tukakiacha.

Mimi nitoe mfano Mhe. Naibu Spika, Rais Mstaafu Dr. Salmin Amour Juma alianzisha mambo yake mazuri Tunguu kule na sasa hivi hii nchi ingekuwa na fedha nyingi sana kwa sababu tungekwishatangazwa zaidi huko duniani, lakini wakatokea watu wakatia maneno maeneo, yote yale yamechukuliwa mwitu ukipita mtupu maeneo yamegeuka rangi wakati kule lile eneo lilitengenezwa kwa mamilioni ya fedha na ingekuwa tumeliendeleza eneo lile basi Waziri wa Biashara usingepata tabu. Leo tunatoka hapa tunakwenda Tanzania Bara maonesho ya Saba Saba, sisi maonesho yetu tumeyaacha pale. Naomba Mhe. Waziri utafute sehemu na sisi tujiimarishe katika kuuza biashara zetu.

Tuliseme kuwe na maeneo huru, fedha hiyo! maeneo huru tumesema kwa mdomo sijui hata kama kumewekwa kitu halafu tunasema hatuna fedha tutazipata wapi tunaazisha kitu halafu hatukishughulikii kwa matakwa ya mtu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nimesema nachangia, hiyo ni fedha mambo ya biashara hayo usije ukaona nimekiuka huu mswada, nimeupitia vizuri lakini mambo ya fedha na mambo ya biashara.

Naomba sana Mhe. Waziri, Mswada huu ni mzuri kama utakalia tena na marekebisho ambayo wameyatoa wenzangu basi unaweza ukaisaidia serikali. Kwa ninavyokujua hukubali kushindwa unataka wizara yako ionekane ili ujulikane kwamba wewe ni mzalendo na unaisaidia nchi yako. Sisi tuna imani kubwa na tunamshukuru rais kukuteuwa wewe kuwa Waziri wa Biashara, kwa sababu amekuona nyanja zako na unavyofanya na kweli unafanya vizuri mpaka sasa. Lakini kuna baadhi ya sheria ndogo ndogo Mhe. Waziri zipitieni tena mzirekebishe, kuna vikwazo vidogo vidogo humu vinawasumbua wananchi wetu.

Mimi niseme kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na nikutakie kila la kheri ili vipengele vilivyomo humu viweze kusaidia nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipatia nafasi kidogo ya kuweza kuchangia katika suala zima la kuanzishwa Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Utunzaji Karafuu na Mazao mengine ya Kilimo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu waliotangulia tayari wameshatoa ufafanuzi wa kutosha katika mswada huu wa sheria na mimi naungananaye mkono kwa yale ambayo waliweza kuyapitia. Kwa sababu muda uliyopo ni mfupi sana, sidhani kama ninaweza kumaliza yale yote ambayo niliyapanga kutaka kuyazungumza. Hata hivyo, nitazungumza japo kwa ufupi kidogo niseme tu kwamba Shirika hili la *ZSTC* ni shirika la zamani, kongwe na la muda mrefu na limeweza kuliendesha shirika lake kwa muda huo bila ya kuwa na ridhaa ya wananchi. Mpaka juzi na jana na wiki zilizopita na miezi watu wote wanasema kwamba shirika hili bora libakie peke yake tuweze kutaifisha au kubinafsisha suala zima la karafuu.

Lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kufanya angalau kidogo kwa kuzivuta nyoyo za wananchi. Hali ilivyokuwa zamani ilikuwa ni mbaya sana, wanasema hii mali ni yetu hakuna sababu ya serikali kukamia kwenye mali ya mtu binafsi. Lakini kidogo Mhe. Waziri angalau amewapa moyo wananchi kwa kuweza kufikiria mambo kadhaa wa kadhaa kwa ajili ya kuwanyanyua wananchi hali zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona kwanza jambo la miaka mingi katika shirika hili la biashara halikuweza kufanya chochote mikarafuu hali ilivyokuwa hapo zamani na hivi sasa ni tofauti. Shirika hili halikuweza kutoa tathmini ni mikarafuu mingapi ambayo tayari imeshakuwa mikongwe na haifai na mingapi ambayo inahitajia kupandwa hivi sasa. Kama shirika hili lilikuwa linajua linapata faida ya kutosha kutokana na zao hili, kwa sababu ndilo lililokuwa uti wa mgongo wa nchi hii kabla ya huo utalii, lingeweza kwa miaka hiyo ya nyuma kulifanyia busara na hekima kubwa shirika hili lingeweza kuwasaidia wananchi na leo wananchi wangekuwa katika hali nzuri sana.

Lakini kwa sababu lilikuwa shirika hili linapata mapato na linajinufaisha shirika lenyewe, lakini wananchi walikuwa hawapati mafao wala maslahi yoyote. Pamoja na hayo niseme kwamba, Mhe. Waziri amejitahidi ingawa kuna mapungufu bado ya kutosha katika sehemu hii hapa.

Vile vile sasa tunasema kwamba shirika hili ni shirika la kitaifa ambalo linajitegemea wenyewe katika mambo yote. Lakini kuna mambo ambayo shirika imeyataja kwa mfano, neno lililokuwa linazungumzia ‘kuhamasisha wananchi’. Wananchi bado hawajahamasishwa katika suala zima la kibiashara hili la uchumaji wa karafuu. Kwa sababu watu wametupwa, wamepuuzwa, watu wanaangalia hali ile ya uchumi faida inayopatikana wananchi wamewekwa mbali hawashughulikiwi kitu. Kwa hivyo, wananchi bado hawajahamasishika.

La pili, kama tunahitaji tupate uzalishaji bora wa suala zima la karafuu bado uzalishaji haujaweza kupatikana kwa sababu kiwango cha tani zilizokuwa zikipatikana siku za nyuma na hivi sasa ni tofauti kabisa, sasa hivi tani zinazopatikana ni kidogo. Kwa hivyo, ni lazima waziri ajitahidi kuangalia ni jinsi gani tutaweza kuzalisha uzalishaji huu ukawa mzuri zaidi kuliko ulivyokuwa. Hivyo, vile vile tunahitaji kuongeza idadi ya mikarafuu miche mipya katika mashamba yote na tuweze kupata tathmini ya kutosha kwa maeneo yote ya Pemba na Unguja ni mikarafuu mingapi mipya inayohitajika. Jambo hilo kwa tathmini halijafanywa.

Vile vile tunashukuru kwa upande wake Mhe. Waziri pia kagusia habari ya masoko ya karafuu. Shirika linajitahidi kutafuta masoko, sawa masoko yanapatikana na uuzaji utakuwa ni mzuri, lakini sasa uuzaji wa karafuu utakuwa vile vile bado unakwenda kwa faida kubwa ya serikali kuliko wale wenye mikarafuu yenyewe.

Mimi nashukuru kuwa haijambo hiyo bei ya karafuu imepandishwa lakini bado iko kila sababu ya kuongeza bei ya karafuu, bei ya mchumaji kwa sababu hawa ndio wanaohangaika kuichuma ile karafuu mpaka ikapatikana na kuianika na kupatikana ya *first grade, second grade au third grade* ni hao hao watu. Kwa hivyo, bado wananchi wanayo nafasi kubwa ya kuweza kuhakikisha kwamba shirika hili bado liwawezeshe zaidi kuliko kiwango hiki tulichofikia sasa hivi. Kwa sababu twende na bei ya soko la dunia, bei ya soko la dunia kwa karafuu kama ilivyokwishakuzungumzwa na wenzangu ni kwamba soko bado bei yake ni kubwa. Sasa kama tutaendelea kuwakata sana wananchi hatutawasaidia na itakuwa yale malengo ya wananchi kujinufaisha na shirika hili itakuwa ni kidogo, kwa sababu shirika halijabinafsishwa bado linafanya kazi chini ya serikali basi bado linaendelea kuwanyonya wananchi.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa katika mswada huu habari ya ushindani wa karafuu. Katika suala hili zima halipo kabisa, ingawa katika mswada huu limetiwa ndani ya mashindani, hakuna suala la mashindani, mashindani mpaka upate mwenzako ushindanenae na humu hamna. Kwa hivyo, hili tunasema bado ni la shirika wananchi hawamo, kama inawekwa sekta binafsi kwa kuweza kujadili mambo haya basi tungeweza kusema pale shirika linapambana na watu binafsi katika utoaji wa bei na uhamasishaji wa mambo yote.

Pia tumeona katika mswada huu utachangia mambo ya madawa, mbolea na uvunaji. Lakini mimi nataka niseme pamoja na jitihada za shirika hili bado wananchi wanahitaji kwa baadhi ya mambo kupunguziwa bei. Kwa mfano majamvi, kwa sababu majamvi ni kitu muhimu bila ya karafuu kuianika katika majamvi haiwezi kuwa nzuri. Kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wanaianika karafuu kwenye barabara au magunia, sasa jamvi ni kitu cha pekee ambacho kinaweza kuifanya karafuu ile iwe *first grade*. Sasa hilo shirika lihakikishe kwamba majamvi yapo ya kutosha na kwa bei nafuu.

Lakini vile vile tuangalie kwamba suala moja ambalo mimi sikulisikia katika mswada huu ni mambo ya *product* ya hii karafuu, wakati *product* ya karafuu ni yale makonyo yenyewe ambayo yanazalisha mafuta, karafuu yenyewe inazalisha mafuta, majani yanazalisha mafuta; hili katika mswada huu halikutiwa. Hapa ipo nafasi ya shirika hili kuangalia namna gani kiwanda hiki kinachozalisha mafuta ya karafuu, makonyo na majani kinapata uwezo wa kutosha ili kuweza kupata mambo haya ambayo katika mswada huu haikuzungumzwa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri labda atakapokuja atwambie kwa nini suala hili halikupewa kipaumbele la *product* ya karafuu katika kiwanda chake kinachozalisha mafuta ya aina zote.

Jambo jengine ambalo nalifikiria mimi kwa watu wa zamani, unajua suala la mikarafuu kwa kipindi kilichopita ilikuwa wenyewe wananchi walikuwa wanajitegemea pamoja na matajiri waliokuwanao. Matajiri waliokuwa wananunua karafuu hizi walikuwa wanawaneemesha wananchi kwa kuwapa misaada ya fedha za mkopo kwa kulimisha mashamba yao na kuwasaidia katika maisha yao kabla zao la karafuu halijawa tayari. Sasa naona katika mswada huu tulionao hivi leo suala la mikopo halijatajwa kwa kiasi kikubwa sana, vipi wananchi watapewa mikopo katika kuwahamasisha katika suala zima la upandaji wa mikarafuu na usafishaji. Suala hili la fedha hatukuliona humu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atapokuja hapa atueleze kidogo juu ya suala hili la mikopo litakuwa vipi kwa wananchi ambapo wananchi wamezowea kupata mikopo kabla ya kuchuma karafuu zao.

Halafu jambo jengine ambalo Mhe. Waziri hakulizungumzia sana kwa kina ni suala zima la vitalu vya karafuu. Vitalu hivi ni muhimu sana, na tukifanya *average* ya kila sehemu mikarafuu ambayo inazalishwa haitoshi kwa maeneo yale. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anahitaji kupata tathmini ya kutosha kwa Pemba na Unguja atahitaji miche mingapi kwa kila mwaka ili suala la uendelezaji wa upandaji wa mikarafuu uwe mzuri. Sio hilo tu suala la kupeleka miche, pia kunahitajika wasimamizi wa kilimo watoe ushauri namna gani kuweza kuhuisha. Kwa sababu inasemekana kuwa mtu akipanda miche 50 pengine atapata miche 10 au 15.

Kwa hivyo, ningemshauri Mhe. Waziri hili suala pamoja na kuwa watu wamepewa uhuru wa kuweza kununua miche na kupanda au kupewa bure wakenda wakapanda katika mashamba yao lakini wanahitaji huduma na mtaalamu wa kilimo wa kuweza kuwaongoza katika suala zima la miche ya mikarafuu. Hawa ni wakulima na ni wakulima wetu ambao ni mahodari sana.

Jambo jengine ambalo ningelipenda Mhe. Waziri turudie yale mambo yetu ya zamani. Suala hili serikali au shirika haliwezi kwenda peke yake ni lazima shirika hili liweze kuwa na jumuiya zake. Jumuiya ni kitu muhimu sana, *Co-operative* tunasema, lakini vile vile tunao wale *Clove Growers Association*, hiki ni kitu cha msingi tuwe nao watu hawa na zamani watu hawa walikuwepo maalum kwa kuzungumzia mambo ya karafuu, mwenendo wa karafuu, mahitaji na matatizo watu hao walikuwa wanakuwepo. Jumuiya hizi lazima zihuwishwe kuhakikisha kwamba mikarafuu inakwenda vizuri, ni lazima papatikane *feedback* baina ya wananchi na shirika hili isiwe shirika peke yake na wafanyakazi au viongozi wanaoshughulikia mambo haya. Kwa hivyo, upatikane ule ushirika wa wakulima wote kwa jumla jumla.

Suala jengine la kuuza na kununua naona limezungumzwa sana na kwamba hili shirika linanunua na lihajitaji kuuza. Lakini pia shirika hili linahitaji kupata karafuu zilizokuwa nzuri za *first grade*, lakini tuangale kama kisiwa cha Pemba ni *very productive* kwa suala la mikarafuu kwa sababu mkarafuu unataka sehemu za milima, kama sehemu ya Kusini Pemba ndio sehemu ambayo inazalisha karafuu nyingi sana kutokana na ardhi yake ilivyo.

Lakini wakati ule ule *geographically* ni nchi ya milima na mabonde tabaan mvua zitakuwa nyingi sana. Hapa shirika halikuweza kusema kwamba litawasaidia vipi wananchi katika kuwasaidia wakati wa mapambano ya mvua nyingi ambapo zao lile lipo kwa sababu linapozalishwa zao lile tabaan na mvua inakuwa ipo nyingi. Kwa hivyo, hapa shirika ni lazima liwe wazi bila shaka lijue mazao ya karafuu yatapotea, chungu za karafuu zitaoza na hilo sio lengo tunataka karafuu zipatikane. Je, kutakuwa na tanuri za karafuu au *ZSTC* itafanya vipi kuhakikisha zao lile halipotei linamalizika kwa mvua? Kwa sababu wananchi hawatofurahi mtu shamba ni ya kukodi kwa fedha nyingi pesa zimepotea na mvua imechukua karafuu ile shirika halikupata na mwananchi hakupata kitu. Sasa nafikiria kwamba hili suala ni muhimu sana.

Suala lililobakia ni suala la magendo ambalo ndio la mwisho muda naona umefika. Magendo hayawezi kuondoka labda wananchi wawe wamejengwa sawasawa, wameridhika, lakini kama wananchi hawakuridhika sawasawa suala la magendo litakwenda tu. Kama walivyozungumza wenzangu suala hilo linaendelea kama kawaida kwa njia wanazozijua wao, binadamu ni *Swahibu-l-maarifa* anaweza kupitisha kwa njia zake anazozijua yeye kuwalaza watu wakapitisha. Mimi nafikiri njia nzuri ya kuondosha suala la magendo ni kuwafurahisha wananchi katika bei nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, naheshimu muda wako muda umefika na mimi nashukuru na naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana waheshimiwa wajumbe kwa michango yenu ya hivi kipindi cha asubuhi, tumebaki na wachangiaji wanane tunaomba waje mapema ili jioni waendelee, tunachokiomba kwamba baadhi ya wachangiaji wengi wametoka nje ya mswada na nimeshindwa kuwasimisha wengine hubabaika, sasa naomba wachangiaji wa jioni waende kwenye mswada tuliokusudia ili tuweze kuimarisha na tuweze kupata sheria iliyo nzuri zaidi.

Baada ya hayo machache naahirisha kikao.

(Saa 7:00 kamili Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kujadili mswada huu wa sheria ya kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji Biashara na Ukuzaji wa Karafuu na Mazao mengine ya Kilimo na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitowe shukrani kwa serikali kukaa kutafakari na kuamua kuleta mswada huu, wa sheria na hasa kwa zao hili la karafuu ambalo kwa muda mrefu kabisa zao hili lilikuwa halishughulikiwi ipasavyo, na matokeo yake Zanzibar moja

katika sababu kuu za kuanguka kiuchumi ni kutokana na kutolishughulikia ipasavyo kwa wakati ule zao hili la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kuchangia kidogo katika mswada huu kwa kufuata maelekezo ambayo umetupa kwamba tuchangie moja kwa moja kwa kufuata mswada, naomba kuzungumza kidogo kuhusu karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naipongeza serikali. Naipongeza kwa kuona umuhimu wa karafuu na kwa kuwatendea haki wananchi, kwa kuongeza mara dugu kabisa bei ya zao hili na ninaamini wakulima wa karafuu wanafaidika ipasavyo. Pia naamini taifa litafaidika ipasavyo, kwa sababu karafuu ni moja kati ya mazao muhimu katika dunia hii.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niishukuru wizara. Hivi karibuni tulipokuwa tukipitisha bajeti, tulipozungumza kuhusu wizara hii ilikuwa ni pamoja na kulizungumza kwa kina zao la karafuu na sisi tukatoa kila tunachokijua kutokana na makosa yaliyokuwa yakifanywa huko nyuma na tufanye vipi kwa maslahi yetu na wananchi. Namshukuru Mhe. Waziri kakubali kaitikia wito, katekeleza na katumia pesa nyingi tu kunijengea kituo kimoja kizuri kabisa cha kununua karafuu, ambacho mpaka juzi naondoka siku mbili za mwisho, basi kimenunua jumla ya gunia 176 za karafuu. Mhe. Naibu Spika, naamini ile hali ambayo serikali iliweka wenyewe kwa kutoshughulikia karafuu mpaka watu ikwa wanazisafirisha kwa magendo, basi kwa safari hii Jimbo la Mtambwe litakuwa ni jimbo linaloongoza kwa kuuza karafuu nyingi serikalini.

Mhe. Naibu Spika, ni vizuri tukiona mahala pana tatizo basi ni vizuri tulieleze. Kwa sababu karafuu mpaka kununuliwa kwake inapita katika mchakato kadhaa, kuna wapagazi, kuna wanunuzi, kuna wapasishaji na wote hao wameajiriwa kwa makusudi ili kushughulikia ununuzi wa zao la karafuu ili mkulima apate haki yake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, malalamiko ambayo nimeyasikia kwa wananchi na sikuyaona katika sheria hii, ni kuwa wakulima wanapopeleka karafuu zao vituoni, basi hulazimika kulipia fedha ambazo hazimo katika utaratibu. Kwa mfano, baada ya karafuu kupasishwa kutiwa ndani ya magunia na kupelekwa kwenye mizani. Gunia moja mkulima hulazimika kumlipa yule mpagazi yaani mchukuzu Shs. 5,000/- wakati wale ni watu ambao wameajiriwa na serikali kufanya kazi ile.

Leo nilikuwa nikibishana sana na mkulima mmoja wa karafuu katika kituo cha Bwagamoyo ambacho ni kituo cha muda, lakini kinanunua karafuu kwa wingi sana. Kwamba hata yule mlipaji hulazimika kuchukua Shs. 1,000/- kutoka kwa mwenye mali, mbali mpasishaji na kadhalika. Kwa hivyo, ningeomba sheria maalum iwekwe ili mtu anapokwenda kuuza karafuu zake iwe hakuna tofauti na mtu anayekwenda kuchukua bidhaa yoyote katika sehemu nyengine. Anapelekewa, anapimiwa, kilo zinajulikana na anapewa haki yake basi. Lakini ile kulipa lipa watu wengine wa nje iwe ni kwenye wizara husika.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, kwa sababu zao hili la karafuu linakuja kwa msimu, ningeomba pia kitu ambacho kidogo naona nilete kama muongozo kwa sababu Mhe.

Waziri atatunga kanuni hapo baadae, ni kuhusu wanunuzi wa karafuu. Mhe. Naibu Spika, tuna vijana wetu wamesoma, ni wazuri, na japokuwa ununuzi unakuwa ni kwa muda lakini na wao wangepata ajira hii ya muda ya kununua karafuu. Inanishangaza kwa nini mpaka leo unapokuja ununuzi wa karafuu basi wanachukuliwa watu kutoka serikalini, wanaacha kazi za wizara zao wakaja huku na kule wanalipwa na huku wanalipwa, wakati wapo vijana wetu tumewasomesha, wazuri na wenye ujuzi zaidi ya wao hawaajiriwi angalau na wao wakafaidika kwa kipindi hiki kifupi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika kanuni basi aweke mazingira haya ya ununuzi na wanunuzi, ili neema ikiingia basi iingie kwa wote.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika kuchangia mswada huu, kwanza niende kwenye ukurasa wa 248, pana neno waziri hapa yaani katika tafsiri. Imeeleza kuwa waziri maana yake ni mwenye dhamana ya masuala ya kibiashara. Mimi ushauri wangu kama itakuwa sawa basi ingeongezwa kuwa waziri maana yake ni waziri mwenye dhamana na masuala ya kibiashara, kuliko kuiwacha vile ilivyo, haiwezekani kuwa kila mwenye dhamana awe ni Waziri wa Biashara.

Halafu jengine Mhe. Naibu Spika, tukiufungua ukurasa wa 250, kifungu cha 7 sehemu ya 2(a) kimeeleza kama ifuatavyo. Kununua na kuuza karafuu na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani. Mhe. Naibu Spika, mimi ninavyojua unaposema kwa bei ya ushindani, iwe kuna wale wa kushindana nao, lakini katika mswada huu huu imeeleza kuwa muuzaji na msafirishaji pekee wa karafuu na mauzo yanayotokana na mazao ya karafuu. Ina maana sasa hili Shirika la Biashara linalotaka kuundwa, wao ndio watakaonunua karafuu kwa bei ya ushindani, lakini wao ndio wauzaji pekee wa karafuu pamoja na mambo mengine yanayotokana na hayo. Sasa mahali palipokuwa hapana ushindani basi sijui wizara itashindana na nani au sijui kama ni wakulima wa karafuu katika nchi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachopenda kueleza ni kuwa katika kushughulikia zao hili la karafuu, tokea ndani ya Baraza mpaka Waheshimiwa Viongozi wetu Wakuu walikuwa wakitembelea katika kambi za karafuu, waliahidi kuongeza zao la karafuu na nashukuru mkulima safari hii anafaidika kwa kupata kilo 1 kwa Shs. 15,000/-. Lakini walisema kuwa hii ni asilimia 80 ya bei halisi ya bei ya karafuu inayouzwa nje, yaani mkulima anapata asilimia 80. Pia walisema kama bei itaongezeka, basi na serikali itaongeza bei ya kununua karafuu kwa mkulima. Kadiri bei itakavyofika juu, itakuwa hairudi tena maeneo hayo tulikuwa tukiyasikia. Sasa Mhe. Naibu Spika, hoja yangu iko hapa.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ukiangalia soko la karafuu duniani na India ndio wanunuzi wakuu wa karafuu zetu, kwa pesa za Tanzania wananunua kilo kwa Shs. 41,252/- wakati mkulima anauza karafuu zake kwa kilo Shs. 15,000/-. Kwa vile serikali kwa nia safi iliongeza mpaka kwa asilimia 80 ya bei wakampa mkulima na waliahidi kila bei ikipanda juu na wao wataongezea. Sasa hii bei imeshakaa kwa muda mrefu sana, sijui kwa Mhe. Waziri kwa sababu ya bei hii ya dunia, kule India kuna mpango wowote wa kuwaongezea wakulima hawa bei ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu moja. Ulimwengu sasa hivi ni kijiji. Watu wanapata taarifa kutoka kwenye vianzio mbali mbali. Tuna maadui katika nchi hii na hawa tunawaita watu wa magendo ya karafuu, hivi sasa Mhe. Naibu Spika, wananunua pishi kwa Shs. 30,000/-, wakati serikali inanunua kwa Shs. 22,500 ni kusema kuwa huko kunakonunuliwa karafuu watu hawa wanazo taarifa zote za bei, siku hizi dunia ni kijiji watu wanavyosema. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama taarifa yangu itakuwa sahihi basi tuone kuwa inafika wakati wananchi hawa kufikiwa kuongezewa bei ya karafuu katika manunuzi kama Waheshimiwa Viongozi wetu Wakuu walivyokuwa wakielekeza.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa huu wa 8 kifungu nambari 9(1)(c) kinaeleza kuwa;

Kifungu 9(1)(cc) "kupanga ubora wa karafuu na mazao mengine ya kilimo", yaani hii ni kazi itakayofanywa na hilo shirika.

Mhe. Naibu Spika, katika ubora huu wa karafuu, kwenye manunuzi mimi nasema kuwa sasa ni lazima tubadilike, tutafute wataalamu ambao wanaweza kujua kuwa karafuu hii ni bora na hii sio bora. Nimeshuhudia kwa sababu safari hii mimi mwenyewe nilikuwa napita vituoni. Kuna mtu kaambiwa karafuu zake ni *grade* ya 2, lakini kwa sababu zisizojulikana pale pale akaambiwa ni *grade* ya mwanzo, nafikiri nimefahamika. Kwa maana hiyo sasa tuwe na wataalamu waliokuwa wazuri wa nafsi zao na wenye kuridhika na walichonacho, kwa hivyo wakipasisha kuwa hii ni *grade* basi iwe ni *grade* ya kwanza kwa maslahi ya taifa letu na biashara tunayoiuza. Isiwe chochote kumsaidia mtu ina sababisha kubadilisha msimamo na maana yake ni kuvuruga mfumo mzima wa bei.

Kwa hivyo, basi kama kweli tunajikita kabisa kuimarisha hili soko la karafuu katika ubora pamoja na mambo mengine tuangalie wapasishaji wetu ambao wanawekwa kwa sifa wanazojua wenyewe wawekaji. Lakini mimi sikuridhika nao kwa sababu chochote tu kinawapa kuweza kubadilisha msimamo, huo ni upande wa kutoka *grade* ya pili ukapeleka *grade* ya kwanza. Lakini pia wakati mwengine hutoka *grade* ya kwanza ikapelekwa *grade* ya pili, sisi tunayaona.

Jengine Mhe. Naibu Spika, naomba katika sheria hii kama inavyoeleza na iwe hivyo karafuu zetu ziwekwe kuwa ni kilimo endelevu. Tumeona, ilifika wakati karafuu zetu tukazisahau kabisa, mikarafuu ikapigwa kuni, mkaa, watu wakajengea tu na wengine wakapasua mbao na kadhalika na mikarafuu ikapotea na kila siku zikienda mbele, kiwango cha karafuu tulizokuwa tukizipata baada ya nyingi kusafirishwa kwa njia ya magendo, ilikuwa ni kidogo na serikali ilikuwa inaingiza pato dogo sana. Kwa hivyo, tubadilike kwa namna ambavyo mswada umeeleza basi tuone kuwa kilimo hiki kimeshughulikiwa ipasavyo. Tujuwe kwa nini mikarafuu mingi inayopandwa na wakulima inakufa njiani, pengine kuna sababu za kitaalamu. Kwa hivyo, wizara ione hasa kwa kushirikiana na hiyo Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na wataalamu wengine kuona kuwa upandaji wa karafuu unakua kwa kasi, watu wanapanda mbegu bora kutoka kwenye vitalu, wanashughulikiwa na kuona kuwa karafuu hizi zinaongezeka siku hadi siku. Ili tuweze kujikomboa katika nchi hii. Hivi sasa tuko katika hatari, tulisema kuwa utalii ni sekta kiongozi katika uchumi na juzi tuliona wanaingia watalii

wengi, lakini pesa ni kidogo uchumi umeshaharibika, utalii ni uchumi tegemezi hivyo tujikite katika kuimarisha kilimo chetu cha karafuu Unguja na Pemba.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo mimi linanisikitisha, serikali ina mashamba mengi sana ya mikarafuu, kuna mingine wamepewa watu hawayashughulikii isipokuwa ni kuchuma tu na inakufa ovyo. Kuna mikarafuu mingine Masheha kila ukifika msimu ndio wanakwenda kukodisha kama ni yao. Hii ni mali ya taifa, kwa sababu mali ya serikali ni mali yetu, sio vibaya, hivyo tubadilike kiuchumi serikali ikakaa kitako na kuweza kama kuna lazima ya kutoa mashamba yake na kuwapa watu, basi wapewe wale ambao wataishughulikia na tija kupatikana. Vyenginevyo wangeipiga mnada wanunuzi wako.

La mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, katika suala hili la karafuu, ninaomba kwamba hivi sasa watu wanachuma karafuu na Mwenyezi Mungu alivyowajaalia ndio hivyo, wengine wanachuma karafuu kutoka shehia moja wakenda wakachuma shehia nyengine, ikabidi warudi shehia hii wanayokaa kwa kuja kuchambua karafuu na kuzianika na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, matatizo makubwa yaliopo na naipongeza serikali kwa kuweka askari na vizuizi katika barabara siku hizi kwa ajili ya kushughulikia karafuu, napongeza sana jambo hili. Lakini matatizo makubwa yalioko ni kuwa watu wameshakwenda kuhangaika kuchuma karafuu zao, wengine wamepakia kwenye gari za ng'ombe, wengine kwenye baskeli na wengine gari za mizigo, kisha wakifika kule kituoni wananyanyaswa, wanadaiwa vibali za kusafirisha karafuu kutoka shehia moja mpaka nyengine wakati wale ni wachumaji, inakuwa ni adha kubwa sana. Kwa hivyo, mimi sipingani sana na utaratibu wa ulinzi wa karafuu. Lakini ningeomba sheha waelekezwe kiasi ambacho wale watu waliokuwa wanalazimika kuchuma karafuu zao hapa na kuzisarifu katika sehemu nyengine, wawape vibali maalum wapunguwe unyanyasaji.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho naunga mkono mswada huu kwa asilimia 99, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi).*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipatia fursa jioni hii nikaweza kuchangia mawazo yangu kidogo katika mswada huu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala, ambaye ametujaalia tukakutana jioni hii katika hali ya uzima.

Pia nikushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na kunipatia nafasi. Tatu nimshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote ambao walikaa na kushughulikia mswada huu na kuweza kutufikishia katika Baraza lako tukufu kwa wakati muafaka.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein kwa utekelezaji wake wa ahadi ya kupandisha bei ya karafuu wakati wa kampeni zake za uchaguzi, ambapo alilisema jambo hili na sisi tumekuwa ni mashahidi wa kuona Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein anatekeleza ahadi zake kwa vitendo.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kupitia fursa hii tumuombe Mwenyezi Mungu atuongoze na sisi viongozi. Mhe. Naibu Spika, samahani kifua changu hakiko katika hali ya usahihi, kwa hivyo sauti yangu inatoka vibaya naomba unisamehe kidogo kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, tumuombe Mwenyezi Mungu na sisi kama viongozi tuige mfano kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kutekeleza ahadi zake na sisi tuweze kutekeleza ahadi zetu tunapowaahidi wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika mswada huu katika kifungu kilichosema uanzishwaji wa Shirika la Taifa la Biashara kwa kifupi ZSTC. Mhe. Naibu Spika, hiki ni chombo kikubwa na ni chombo ambacho kweli Wazanzibari tunakitegemea. Kwa hivyo, mimi naanza katika kifungu cha 3(g) ambacho kinasema, naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 3(g)

> "Shirika linatuambia litakapokuwa tayari limeshakuwa tayari litaelimisha wadau kufahamu hadhi ya shirika, muundo na faida kupitia msaada wa kiufundi, elimu, mafunzo, maonesho na ukuzaji ujuzi".

Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia usemi huu sisi kama viongozi tunaelewa umuhimu wa shirika hili na tunaelewa vizuri tu hadhi yake, dhamani yake na faida yake kwetu na kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba hili shirika litakapokuwa tayari limekamilika kupitishwa sheria hii kuwa imekamilika, ningeomba hili shirika nalo lingejitambua kwa sababu inaonesha shirika lenyewe linakosa kujitambua na kuweza kufanya majukumu yake kama vile ilivyojipangia na hatimaye inapelekea kututoa imani sisi wananchi na chombo chetu hiki ambacho ni kikubwa na kina mwelekeo kwetu na kwa taifa letu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, humu shirika litakapokamilika limejipangi mambo mengi ambayo litaweza kuyafanya ili wananchi wa Zanzibar tuweze kufaidika na chombo hiki. Mhe. Naibu Spika, mimi nimuombe Mhe. Waziri kwamba shirika hili litakapokuwa tayari linatumika basi yale majukumu ambayo limejipangia, ahakikishe yeye anayasimamia na yanatekelezwa ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende katika zile kazi ambazo shirika hili limejipangia na niombe lisimamiwe kwa nguvu zote. Kwanza ni kupatiwa elimu wale wakulima wetu wa zao la karafuu. Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu kwa vile sisi wenyewe kwa muda mwingi tulikuwa tumelitupa na limeshindwa kupata hadhi nzuri, kwa hivyo wakulima na wao wamekuwa wakijifanyia tu wanavyojaaliwa.

Kwa hivyo, mimi niombe elimu ya kuwasaidia wakulima ambayo ni muhimu sana na elimu yenyewe ianzie kwenye upandaji wa mikarafuu yenyewe. Ni lazima wakulima waelimishwe juu ya upandaji wa mikarafuu, kwa sababu zamani sisi wenyewe tulikuwa

tunajipandia tu kiholela holela na hatukuwa tunazingatia ule upandaji bora. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nikuombe uungane na Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kwa kuwa wataalamu tunao basi tuanze kupata elimu juu ya upandaji wa mikarafuu, lakini pia usafishaji wa mashamba yetu ambapo inakuwa ni jambo muhimu, kwa sababu shamba la mikarafuu linaposafishwa, maana yake tutaweza kupata mikarafuu iliyo bora na kuweza kutoa mazao yaliyo bora vile vile.

Mhe. Naibu Spika, elimu hiyo bado naiomba iendelee pia katika uchumaji wa karafuu. Uchumaji wa karafuu nao unahitaji elimu kwa sasa kwa kuwa zao letu hili limekuwa ni muhimu, na ni bora na tunalitegemea kwa uchumi mkubwa wa nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, uchumaji wa karafuu kwa sasa, mikarafuu inakatwa tu ovyo, yaani anaweza akachuma tu mtu ambaye hata ujuzi hana kwa kutegemea tu atavuta matawi kwa kingowe na kuikata mikarafuu ovyo ovyo na hatimaye msimu mwengine unapofika basi mikarafuu inashindwa kuzaa vizuri. Kwa hivyo, naomba elimu hiyo pia ipatikane ili tuweze kuzichuma karafuu vizuri, ili msimu mwingine unapofika basi ziweze kuzaa tena vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna elimu ya uanikaji wa karafuu. Jambo hili nalo nimeliona ni muhimu niliseme kwa sababu hivi sasa tayari msimu wa karafuu uko na tumeshuhudia tunaona karafuu zinaanikwa kiholela holela, kuna wakulima wanaanika tu karafuu barabarani bila ya kuweka chombo chochote chini na sisi tunategemea tuweze kupata karafuu nzuri, ili na sisi tutakapoipeleka kuuza basi tuweze kupata soko zuri. Karafuu zinaanikwa tu barabarani bila ya kuzingatia kuweka chombo chochote chini, saa nyengine inaweza ikanyesha mvua na karafuu zikarowa, wakati hazikuanikwa katika chombo pia zinakuwa ni usumbufu wakati wa kuanua.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, shirika hili litakapoanza kazi yake basi liweze kuwapatia wakulima *motivation* japo kuwakopesha majamvi, kwa ajili ya kuanikia karafuu zetu na kuweza kupatikana karafuu nzuri ambazo zitakuwa na hadhi nzuri ya kuuzika katika Soko la Dunia.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii itakapokuwa tayari inatumika, shirika kwa kuwa sisi tayari tumeamua kwenda mbio basi ni lazima tuagane na nyonga zetu. Jambo linalorudisha nyuma sana ni magendo ambayo kwa kweli yanarudisha nyuma sana juhudi za serikali na kuona inapoteza mapato mengi.

Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kuhakikisha kwamba shirika hili wakati linaingiza fedha ni vyema kujipatia vyombo kwa ajili ya doria ambavyo vitaweza kudhibiti magendo hayo yasifanyike. Mhe. Naibu Spika, hata usafiri wa nchi kavu wakati mengine karafuu zinaweza kusafirishwa kupitia nchi kavu, lakini askari wetu wakashindwa kufuatilia kutokana na kukosa vyombo vya kufuatilia na magendo ya kapitishwa kama kawaida.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache sina zaidi, isipokuwa nilitaka nichangie na mimi kidogo angalau niwe nimejumuika kwenye mchangio wa mswada huu. Kwa hivyo, mimi

mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu mdogo sana kuhusiana na hoja iliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia chochote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa hai na pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi kwa ajili ya kutoa mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaanza kwenda ndani ya mswada nadhani nitoe machache kama *introductory statement* ya huu mchango wangu wa leo. Mswada wa leo umejikita zaidi katika mambo haya ya maslahi ya serikali zaidi na hili shirika kuliko maslahi ya wakulima. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimelazimika kusema *statement* hii, kwa sababu mchakato wa suala zima wa uchumaji, uvunaji mpaka zinauzwa katika soko kuna michakato mingi, michakato ambayo hupelekea gharama pamoja na nguvu binafsi za mkulima.

Kwa hivyo, baada ya kutupa macho kwenye vipengele kadhaa vya mswada wetu huu, nimebaini kwamba inaonekana wadau hasa wanaohusika na mambo haya ya karafuu hawakushirikishwa tangu hatua za awali za utayarishaji wa mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa uvunaji wa karafuu kuna matatizo mengi yanajitokeza kule. Kwa mfano, watu wanaanguka mikarafuu na kwa bahati mikarafuu mingi iko katika Kisiwa cha Pemba, ambapo huduma za afya na matibabu ni hafifu sana.

Sasa pamoja na bei nzuri ambayo wakulima wamepata, lakini mswada huu haukuweka ni kwa kiasi gani shirika au serikali inaweza kuwatupia macho watu ambao mara nyingi na kwa kiasi kikubwa huanguka mikarafuu wakati wa uchumaji.

Mhe. Naibu Spika, suala la gharama za kuhudumia au fidia za wale walioanguka mikarafuu katika kipindi cha uchumaji basi kingeekwa katika malengo ya hili Shirika la *ZSTC*.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye mswada. Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kwenye ibara ya 6(2)(c) naomba kunukuu.

Ibara ya 6(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

> “Kwa mujibu wa msharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki shirika litatoa msaada wa:- …
>
> (c) Tafiti za kilimo kwa karafuu na mazao mengine ya kilimo”.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna zao ambalo serikali imelisahau katika suala zima la utafiti kuanzia uzalishaji, ukaushaji pamoja na uuzaji basi ni zao la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, zao la karafuu liliingia hapa mnamo *century* ya 16 na liliingizwa na Mfanyabiashara wa Kiarabu aliyekuwa akiitwa Saleh Buhamereni, basi mkarafuu ule aliouleta Saleh Buhamereni katika *century* ya 16 ndio ule bado haujabadilika.

Wakati hivi sasa shirika hili linaazishwa mkarafuu uliopo ni ule na tumeshaona hapa serikali inafanya tafiti mbali mbali za mazao kadhaa ikiwemo miembe, minazi na yamo machotara ya miembe pamoja na minazi, lakini sijawahi kuona chotara la mkarafuu na huku ni kudharau, yaani hii ni dharau kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nadhani katika hili mswada huu wangeurudisha kwanza kwa ajili ya kwenda kukaa na wadau na kuweza kuona kwa kiasi gani wanaweza kuboresha zaidi.

Kutokana na hali hiyo, inasikitisha sana tokea 16 *century* mpaka leo hii bado tunategemea jua tu kwa ajili ya kukausha karafuu zetu, wakati kuna *scientific system* ya kutumia sehemu za kukaushia bila ya kutegemea jua, eti leo hii shirika linataka kupanga bei. Hivi mumezungumza na Mwenyezi Mungu kuhusu mvua na karafuu zikipigwa na mvua zinakuwa ni mpeta.

Nadhani hawakuwashirikisha wadau, kwa sababu kama wadau wangetushirikisha katika hili, basi tungewaambia kwamba tuangalie utaratibu mzuri wa kuweza kukausha karafuu zetu na wala sio kutegemea masuala ya jua tu, kwa sababu jua siku lipo na siku nyengine halipo na *grade* ya karafuu inaanguka.

Kwa kweli karafuu zinaanikwa barabarani kama alivyosema Mhe. Mjumbe aliyepita, yaani zinaingia tope na hatimaye zinakuwa mpeta. Kwa hivyo, sisi tunataka *scientific system* ya *drying* hapa na wala sio hii, kwa sababu tokea *century* ya 16 mpaka leo hii tunakaushia jua tu jamani, inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa serikali ambayo inayo wataalamu kama hii yetu nikiangalia katika safu ya mbele, basi nyote huko ni wataalamu Waheshimiwa Mawaziri na hata sisi huku *backbenchers* musituoni hivi tunayo taaluma kubwa. Kwa mfano, *backbenchers* mnatupa serikali leo, basi tutahakikisha karafuu zetu zinakuwa katika misingi ya kitaalamu, yaani tunazikausha kwa misingi ya kitaalamu na wala sio kwa kutumia jua. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu tuangalia jinsi mkulima au zao lenyewe la karafuu jinsi hivi sasa ambavyo halishughulikiwi. Mhe. Naibu Spika, nadhani serikali imekurupuka baada ya soko la karafuu kupanda huko duniani ndio ikaleta mswada huu, lakini juzi tu Pemba tulikuwa tukiona bora mabungo kuliko karafuu, yaani mabungo yalikuwa na bei zaidi kuliko karafuu na zao hili mumelidharau. *(Makofi)*

Rais Mstaafu wa Zanzibar wa Awamu ya pili Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi ah! *Astaghafiru Llah* Mwenyezi Mungu ampe maisha mzee Aboud Jumbe Mwinyi kwa kweli

alikuwa hapa mikarafuu ikikauka tu, yaani ikianza ugonjwa tu, basi alikuwa akileta wataalum kwa ajili ya kuitibu. *(Makofi)*

Lakini leo mikarafuu kule Pemba sehemu za Mtambwe, Mgagadu imekauka, isipokuwa ni jitihada zetu tulizofanya pale mpaka mikarafuu ikaendelea kuwepo na serikali inafumba macho. Sasa baada ya kuinuka soko la karafuu ndio mnajileta tena pamoja na kuleta mswada, jamani huu ni ubinafsi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nadhani serikali kuna haja ya kukaa hasa kwa ajili ya kuinua maisha ya mkulima. Kwa kweli hili zao la karafuu nafikiri mmekurupuka kwa sababu hamna vyanzo vyengine vya mapato ya serikali, basi msikurupuke. Kwa hivyo, ni vyema mkae na wataalamu pamoja na sisi wakulima muone ni vipi tunaweza kuboresha zao, lakini leo mnakuja tu na haya mambo.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 253 katika ibara ya 9(1)(f) naomba kunukuu.

Ukurasa wa 253 kifungu cha 9(1)(f) kinaeleza hivi:

> "Kukamata na kutaifisha karafuu zinazosafirishwa kinyume na sheria au zilizohifadhiwa kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Karafuu Nam. 11 mwaka 1985".

Kwa kweli hapa ni tatizo, kwa sababu mimi nakaa kwenye ukanda wa mashariki ya Kisiwa cha Pemba na wala sina mkarafuu hata mmoja bora ni *declare interest*, kwani kule kwetu ni maweni. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini kuna watu wanalima mikarafuu na wanatoka Vitongoji wanakwenda sehemu za Msuka, Konde pamoja na sehemu za Mkoani kwa ajili ya kulima mikarafuu. Vile vile masheha wanasimamia sana hii Sheria Nam. 11 ya mwaka 1985 pamoja na polisi.

Sasa mtu anakaa Vitongoji na karafuu zake ziko Kuyuni, hivyo ni lazima azihamishe karafuu zile aje azianike kwake Vitongoji, lakini siku zote watu wanakamatwa na mikoba pamoja na mapakacha ya karafuu almuradi tunadhalika sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala hili nadhani muliangalie Mhe. Waziri, ili usufumbu huu uwaondokee wakulima.

Vile vile kifungu cha 9(1)(c) naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 9(1)(c) kinaeleza hivi:-

> "Kupanga ubora wa karafuu na mazao mengine ya kilimo".

Mhe. Naibu Spika, ubora wa karafuu unapatikana baada ya ile *drying system* kuwa *controlled*. Sasa tatizo ni kwamba mnataka kupanga ubora nyinyi, lakini hivi sasa

tunakaushia jua. Kutokana na hali hii, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atakapokuja hapa anifafanulie kwamba ikiwa karafuu ni mpeta na tumekuja nazo kama kipindi hiki, ubora huo tutaupanga vipi.

Kwa maana hiyo, hii muondoshe kabisa kuwa karafuu itategemea hali yake ya ukaukaji na wala sio nyinyi ndio wenyewe uwezo wa kupanga ubora, kwa sababu mtatumaliza. Kwa mfano, wakati mwengine karafuu inakuja na *quality* sawa, lakini *grade* zinatofautiana. Sasa hapa naomba uniwekee sawa ni kipimo gani wataalamu wenu wanachokitumia mpaka karafuu wakaweza kupanga hii ni *grade* ya mwanzo, pili na tatu.

Kwa kweli katika suala hili tunaona kwamba kuna ubabaishaji pengine mtu anapewa *grade* ya pili kumbe vile ni ya kwanza. Kwa hivyo, tunaomba mtupe vigezo na wakulima nao wajue kuwa mimi napeleka zao langu hili, lakini kwa ninavyoijua hii ni *grade* kadhaa, basi mutupe elimu hiyo na kinyume na hivyo wataendelea hawa vijana wenu kutudhulumu.

Nikiendelea na mchango wangu niende kwenye kipengele cha 9(d) kinachozungumzia suala la zima la kupanga bei ya kununulia karafuu pamoja na mazao mengine ya kilimo. Nafikiri ni vyema shirika likashirikiana na wadau ndipo waweze kupanga bei.

Kwa hivyo, kipengele hiki naomba kibadilishwe na kiwe hivi “Shirika kwa kushirikiana na wadau wa zao hili litapanga bei ya kununulia karafuu pamoja na mazao mengine ya kilimo”.

Vile vile kwa upande wa haya mazao mengine ya kilimo ni vyema kutajwa, kwa sababu ikielezwa tu mazao mengine ya kilimo kwa kushirikisha na karafuu basi ni tatizo Mhe. Naibu Spika, kwani mazao mengine ni pamoja na ndizi. Kwa mfano, sisi tunavuna ndizi Pemba na kuziuza Unguja, Dar-es-Salaam pamoja na Tanga, lakini sheria imebana kwa karafuu.

Kwa hivyo, ni vyema kwa haya mazao ya kilimo tuwekewe wazi na kupangiwa bei na shirika, karafuu ndio imekuwa *total monopoly*, lakini haya mazao mengine ni yepi?

Mhe. Naibu Spika, nadhani katika suala zima la tafiti za karafuu ni vyema kujitahidi sana, kwa sababu wenzetu mbali mbali. Kwa mfano, Ghana hivi sasa wanafanya utafiti wa *cacao*, kwa hiyo kila baada ya muda mkulima wa *cacao* anafaidika na utafiti unaofanywa na nchi yake. Lakini hadi leo hii sisi Wazanzibari kuhusiana na zao la karafuu hatujaona lolote linaloendelea.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii adhimu ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara *ZSTC*. Vile vile nichukue fursa hii nipongeze kwa dhati hatua hii ya kufufua Shirika la Biashara la *ZSTC*, ambapo lilikuwepo tokea zamani. Pia nichukue nafasi hii kwa

kumpongeza waziri husika ambaye ametuletea mswada huu kipindi muafaka cha kuwakomboa wakulima wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaingia katika mswada nitoe maelezo kidogo na baadaye niingie katika kuchambua mswada.

Kwa kweli kumekuwa na kero ya wahudumu au matajiri wa karafuu. Mhe. Naibu Spika, kero kubwa wanayoipata hivi sasa wakati wanapokwenda kuuza karafuu zao, basi kule kwenye mizani kuna watu ambao wanabeba magunia, yaani wale ukiangusha gunia lako ukimaliza kupimiwa lazima uwalipe, hata kama umebeba mwenyewe basi ukeshaweka kwenye mizani lazima ulipe.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hii ni kero ya wananchi wetu tena inaendelea siku hadi siku, kwa maana hiyo itakuwa mkulima hafaidiki lakini karani atakuwa anafaidika.

Vile vile kwenye vituo vyetu vya kuuzia karafuu hakuna huduma bora, kwa sababu vituo teule vilivyoteuliwa kuuzia karafuu hakuna hata sehemu za kujisaidia, yaani hakuna vyoo na hili ni jambo muhimu sana, kwa sababu kuna mkusanyiko wa watu, ambapo watu wanakuwa kwenye foleni na endapo mtu atapata haja basi lazima aende. Hivyo, katika kuboresha mambo haya lazima huduma ya vyoo katika vituo vilivyoteuliwa basi pawe na huduma nzuri.

Lakini jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa Mhe. Naibu Spika, kibarua ambaye anaokoa zao la karafuu kutoa juu katika mswada huu hakutajwa na wala kuekewa mipango mizuri. Kwa mfano, juzi tu mnamo tarehe 10/09/2011 wakati ilipotokea ajazi ya Meli ya *MV. Spice Islanders,* kuna kijana mmoja wa Jimbo langu la Kojani mwenye umri wa miaka 18 alipona.

Sasa kwa bahati nzuri kufika kule akenda kwenye shughuli za uchumaji wa karafuu na Mwenyezi Mungu amemjaalia ameanguka, yaani ni tarehe 06/10/2011 na mimi mwenyewe nimemshuhudia pale Hospitali ya Chakechake yupo kwenye kigari cha kubebea wagonjwa, nimekutana na baba yake na kuniambia huyu ndio yule kijana wako uliyemkuta katika Hospitali ya Kivunge, wenzangu wale tuliokwenda kwenye Hospitali ya Kivunge walimuona kijana yule.

Kwa hivyo, hili ni tatizo kwa maana hiyo, lazima kuwekwe mazingira mazuri ya wale wanaoliokoa zao la karafuu kutoka juu wathaminiwe na kuwe na jambo maaluma endapo watapata maafa kama hayo, basi serikali au Shirika la *ZSTC* lenyewe ishughulikie.

Mhe. Naibu Spika, sasa nianze mchango wangu kwenye kifungu cha 7(2)(a) naomba kunukuu.

Kifungu cha 7(2)(a) kinachoeleza hivi:-

> “Kununua na kuuza karafuu na mazao mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani”.

Mhe. Naibu Spika, hapa tumeambiwa kwamba kutakuwa na kununua na kuuza karafuu kwa bei ya ushindani. Lakini inasemekana hapa ushindani wenyewe mimi bado unanipa matata sijui wa namna gani kama kuna makampuni yataruhusiwa au wakipata kibali kutoka *ZSTC* na wao wanunue au watu binafsi wanao uwezo wa kununua basi wakaruhusiwa kununua ama ni kushindana na mazao mengine yalioko Zanzibar. Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atufafanulie vizuri, ili atuweke sawa.

Kwa kweli ushindani hasa wa zao hili la karafuu basi kama mtawaruhusu watu kushindani basi wananchi watanufaika kweli na ukulima huu wa karafuu. Lakini kama ni nyinyi tu, basi pamoja na bei iliyopandishwa bado haijakidhi haja.

Kwa nini ninasema hivyo? Kwa sababu mtu anamiliki mikarafuu mia moja au mashamba matatu ya mikarafuu, lakini *Wallahi* hana hata kipande cha usafiri, yaani hata ile gari ya ng'ombe inamshinda. Kwa hivyo, hili ni tatizo na kama ukitaka kuwa-*check* basi wa-*check*. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kifungu cha 7(f) naomba kunukuu.

Kifungu cha 7(f) kinaeleza hivi:-

> "Kununua, kuhamasisha, kupanga na kuweka utaratibu wa kuuza, kutoa vifaa na kusaidia wateja juu ya namna ya uvunaji na ushughulikiaji, vifaa na teknolojia na mbinu, mafunzo na utaalamu, ujuzi, mfumo wa haki miliki kwa matumizi ya watu na taasisi zinazojishughulisha na karafuu na mazao mengine ya kilimo".

Sawa jambo hili ni zuri. Lakini utakuta mikarafuu mingi ya watu binafsi. Tunaomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa hawa wakulima wa karafuu kama kuna haki miliki, basi angalau wapatiwe vitambulisho kwa kujulikana kuwa hawa ni wakulima wa karafuu, ili wakati unapofika wa mavuno ya karafuu kuwe na wakulima bora na kuweza kupatiwa zawadi pamoja na kushiriki Mashindano mbali mbali ya Maonesho Duniani. *(Makofi)*

Hali halisi ni kwamba utamkuta mkulima wa karafuu anapomaliza tu msimu basi hata ile sehemu ya kwenda kukopa sukari haipati na hilo ni tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunaomba pia hawa watu wawe karibu na vyanzo vya fedha yakiwemo mambo ya benki, yaani wakopeshwe. Kwa mfano, mtu anayo mashamba ya mikarafuu mawili mpaka matatu, lakini hana haki ya kwenda kukopa na hili nalo ni tatizo na wala huwezi kumnyanyua mkulima huyo. Kwa hivyo, tunaomba sana liangaliwe suala hilo. *(Makofi)*

Vile vile kama wenzangu walivyozungumza hapa kwamba watu wanajua kuzichuma tu zile karafuu, lakini namna ya kuzishughulikia si nzuri. Kwa mfano, mimi mwenywe

nimeshughudia kuna watu utasikia wanaokota wale, basi mtu yuko juu ya mkarafuu anamkatia tawi yule ambaye yuko chini na baadaye kuchambua.

Kwa kweli hili ni tatizo na huko ni kuiangamiza mikarafuu. Kutokana na hali hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, suala hili lishughulikiwe kwa kina.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 256 kifungu cha 20(1) naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Ukurasa wa 256 kifungu cha 20(1) kinaeleza hivi:-

> "Shirika litaagiza kuweka na kuhifadhiwa vizuri vitabu vya hesabu kuhusiana na:-
>
> (a) Fedha zilizopatikana, zilizotumika na shirika pamoja na risiti za matumizi yaliyotokea;
> (b) Mali na madeni ya shirika na
> (c) Taarifa za mapato na matumizi ya shirika.

Mhe. Naibu Spika, ni sawa tena ni vizuri sana na napongeza kifungu hiki kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Lakini mavuno yakeshakufanyika, basi shirika liwe na agenda rasmi ya kuweza kuwakomboa hawa wananchi.

Kwa mfano, zamani kama alivyozungumza Mhe. Saleh Nassor Juma wakati wa Rais Mstaafu wa Zanzibar Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi, basi katika fedha hizi za karafuu tuliwahi kununuliwa meli MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo na hii ni neema moja wapo ya mapato ya karafuu. Kwa hivyo, kama fedha zikipatikana kutokana na tabu tulizonazo basi ziende katika fungu la kununua meli, ili usafiri uwe mzuri.

Mhe. Naibu Spika, inapofika wakati wa msimu wa karafuu basi watu wanatoka Tanzania Bara, Unguja na wanakwenda Pemba na wale wa Pemba wanakuja Unguja, yaani watu wanapishana na kama itakuwa hatuna usafiri mzuri basi hata kuzisafirisha karafuu bado hatuwezi. Kwa hiyo, tunaomba yatakapopatikana mapato ya Shirika la Biashara la Taifa la *ZSTC* ifikirie jambo hilo.

Kwa kweli inasikitisha sana katika jambo hili, ambapo kama tutaweka kwenye mambo mazuri, basi tunaweza kufikia malengo tuliyokusudia.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyozungumza ikiwa mtu anayo mashamba ya mikarafuu hamiliki hata gari moja ya ng'ombe ya kuweza kusafirisha na hili ni tatizo. Hivyo, tunaomba kwa msimu huu uliopandishwa bei za karafuu watu waweze kuneemeka.

Mhe. Naibu Spika, kwa mchango wangu huu mfupi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja mimi mwenywe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kojani. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii jioni ya leo kuweza kuchangia mswada huu unaohusiana na malengo ya kutaka kukuza biashara yetu ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri tangu alivyoanza kukaa kwenye kikao hiki ameshatuletea mambo mawili mazito tena ni mazuri, kwa lengo la kutaka kuwainua wananchi na jengine kwa lengo la kutaka kule vyakula vya kisasa na tumepitisha mswada hapa.

Vile vile namshukuru sana Mhe. Rais na yeye kwa kukazania mara hii kwa kutuletea bei ya juu na kujiamini, kwamba hivi sasa karafuu zitakuwa katika hali nzuri na itaokoa wananchi hasa wakulima katika kuondoa umasikini na kuwapeleka katika utajiri.

Mhe. Naibu Spika, nilisikia kauli yao kwamba twende kwenye mswada moja kwa moja, naheshimu sana kauli hiyo, lakini kuna jambo Mhe. Naibu Spika kwa uradhi wako naomba kidogo hili tuliseme, kwa sababu ni moja katika kuchangia na kuliweka Shirika la Biashara la Taifa la *ZSTC* katika sehemu nzuri, ili huko mbele likaja kuyumba.

Kwa kweli wenzangu wamezungumzia suala la uangukaji kwa wachumaji. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Mjumbe mmoja alisema hapa kuwa twenda kwa *science and technology* na kutoa mfano jinsi gani *science* hiyo inaweza kutusaidia, alisema kwamba tusitegemee jua tu kwa sababu hatuna ahadi na Mwenyezi Mungu na hilo ni kweli.

Kwa mfano, hivi sasa tayari karafuu zinapigwa na mvua katika mashamba mengine yenye rutuba hususan kama Kitope mvua ni nyingi usiku na mchana. Sasa wakati mwengine hao wachumaji wangu inapelekea sana kuanguka kwa wingi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe ni shuhuda wananchi wangu huko nyuma walianguka na nikafuatilia katika Shirika la *ZSTC* kwa ajili ya kupata malipo, basi lioneshwa orodha kubwa sana. Kwa hivyo, orodho hiyo tuliambia kwamba kuna mpango baina ya Wizara ya Fedha na Shirika la *ZSTC* kuhamisha madeni, kwa sababu Wizara ya Fedha inadaiwa na Shirika la *ZSTC*, kwani Mhe. Naibu Spika, tunawakopa sana huu mswada tunaopitisha hapa mimi siku zote huwa nasema jamani hebu tuwe *serious* kwa sababu tukiwa *serious* katika upangaji wetu tunaweza kwenda, upangaji mzuri lakini utekelezaji unakuwa hakuna hili tuseme ukweli, tunawakopa sana ZSTC tuna lengo gani, lengo lake ni kuwamaliza kabisa. Sasa tukaaambiwa wale watu watalipwa na Wizara ya Fedha mpaka hii leo ni wengi sana na wala hawajalipwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi naomba hili anijibu kuwa ni kweli suala hili wale watu wameshalipwa au mpaka leo wako mpaka kwenye listi, listi hii mpaka lini hili ni moja katika kuvunja nguvu Mhe. Naibu Spika, inavunja nguvu kuwa wananchi sasa wanauogopa ule mti sasa ikiwa wanauogopa basi twende kwenye sayansi na teknolojia ni vipi sasa. Tutafute mashine ambayo itavuna karafuu ili kuondoa usumbufu hiyo ni lazima twende kwenye sayansi na teknolojia sasa hivi, nchi hii imejipanga katika mustakabali mzuri na hata tulivyoanzia kwenye serikali ya kitaifa na kila mambo yake yanakwenda

kwa sheria, mwenzangu kasema hapa tugeuke, sasa hivi mnazi ukitaka kupanda utapanda tu lakini kuna mashine inaangua nazi juu sasa kwa nini mkarafuu tusiwe na mashine hiyo.

Kwa hivyo naomba na hili kwa kuwa Mhe. Waziri ni mtaalam tunaomba atutafutie mashine kwa kuokoa wananchi wetu wasianguke kwani hakuna malipo, ukweli ni huo Mheshimiwa.

Nakuja kwenye ukurasa wa 250 hapa kifungu cha (g) utoajiwa misaada uanzishwaji wa vikundi wallahi nawapa hongera sana wamefanya hivyo na wanaendelea kufanya hivyo, nimeshuhudia mwenyewe juzi tu mwananchiwangu wa Jimbo la Kitope nimekwenda kumchukulia dhamana kumuangalia jinsi gani anapokea cheki ile kwa ushuhuda, amepewa cheki ya milioni tatu, hongera sana Mhe. Waziri. Sababu amepelekea ili akaweze kuliokoa zao lile ili serikali ipate tija.

Mhe. Naibu Spika, wallahi kumsifu Mhe. Waziri sio vibaya namsifu kutokana na jinsi gani wizara yake ameikusudia kuijenga kwenye hiyo sayansi na teknolojia, lazima tumwambie tuseme ukweli. Lakini isijekuwa utendaji wake tu ukawa unarudi nyuma hapo mimi nitakuwa sikubaliani nae lakini sidhani kama atafanya makosa hayo hiyo ndio tabia yake waziri huyu, anatekeleza anatunga sheria tuipitishe ili kwa kufanya utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika kifungu cha (d) ukurasa huo huo kuingia katika makubaliano wakulima, wasarifu, wauzaji, waagiziaji, wasafirishaji maalum walioteuliwa hapa kidogo mimi nitakuwa na wasi wasi na kifungu hiki, tuwe *alert* sana na kifungu hiki. Kwa sababu pamoja na kwamba tunataka tufanye mambo mazuri lakini tuwe na tahadhari, wenzetu India walifanya mambo kama haya wakaingia mikataba na watu wa aina kama hiyo wakiwemo Marekani na nchi nyengine kwa masharti ya CD yale mazuri sana. Lakini baadae wakaamka wale watu wa India kumbe lengo lile la kuchukua wale wenzetu kwa miaka mitano kumbe waligundua kwamba huyu jamaa atatuangushia uchumi wetu, hatimae akaanza kumtengenezea CD feki na yule bwana akaamka akakatisha mkataba wenyewe.

Sasa na sisi kama tutafanya namna hii hatimae tutakuja kupoteza haiba yetu ya karafuu yetu, watakuja kutufanya wanavyotaka wenyewe kumbe tumekubali wenyewe na sheria tumepitisha wenyewe, hapa namuomba Mhe. Waziri kidogo awe muangalifu sana katika kusimamia jambo kama hili.

Nikiingia (h) kusambaza vifaa pamoja na usambazaji wa vifaa hivyo kwenye vituo tuangalie sana hizi mizani zetu, hizi wanavyosema wauzaji wa karafuu huwa zina walakini saa nyengine maana yake mpaka ipigwe kofi wakati mwengine ndio ifanye kazi, kama haikupigwa kofi basi muuzaji anapata hasara kwa sababu pale inakuwa tayari ameshazulumiwa katika zile kilo ambazo amekusudia. Sasa na hili nalo naomba katika uimarishaji wetu huu tuziangalie sana hizi tuhakikishe tunapeleka mpya kabisa zile mashine sio zile za tangu miaka ya nyuma za miaka nenda hata mimi sijazaliwa kwenye dunia hii, sasa zile nazo tuzikatae tujaribu sana kuziweka katika hali nzuri.

Mhe. Spika, ukurasa wa 251 ukodishaji wa mali kwa vile majengo na vituo vya kusafirisha, Mheshimiwa tusikodishe kwa nini tukodishe hebu tuangalie maghala yenyewe huna mengi sasa hivi, nikikuuliza una maghala mangapi utashinda kunijibu huna yote yameshauzwa huna hata moja sijui kama unayo angalau mawili matatu, hebu na hili nieleze Mheshimiwa maghala unayo?.

Mhe. Waziri halafu leo unatuletea sheria tukodishe mali pamoja na majengo ya vituo, mimi hili sitokubaliana nalo kwa mawazo yangu kwa sababu naona tunarudi nyuma tena badala ya kwenda mbele kwa hivyo naomba na hili nalo tuliangalie.

Tukija kwenye (m) ambalo linalingana na jina langu hapa hii nakubaliana nayo tuna muwakilishi wetu Dubai sijui kule iko je, tusiogope sasa kufungua vituo kwenye nchi za nje wakati tumekusudia sasa hivi zao hili kulikuza basi tusiogope, Dubai ipo twende na India pamoja na nchi nyengine tusiogope ndio lengo ambalo tunakuza biashara yetu tuking'ang'ania dubai tu hatufiki, biashara hutangazwa na biashara hasara, biashara itangazwayo ndio hutoka. Sasa kama tuking'ang'ania hivi hivi tu Dubai tu hatwendi tuende mpaka Abudhabi, tufike pahali ambapo sasa hivi tujue vituo vyetu tunavyo vya nchi za nje na hili zao letu liende vizuri basi hapo nakubaliana na wewe ili kuleta ufanisi mzuri.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika uanzishaji upatikanaji wa soko na kusimamia biashara ya fedha na matatizo ya kisheria nakubaliana nalo, Mheshimiwa tuletee sheria kama zinataka kufanyiwa marekebisho tuziweke vizuri kwa sababu kuna mambo mengi hapa inawezekana shirika lako likatokea *mistake* ya kisheria ikakosekana sheria, au kama sasa hivi hujui umshitaki nani kwa sababu wewe unadai fedha Wizara ya fedha huna sheria ya kumshtaki sasa hivi yule. Lakini sheria ikikaa sawa utakuwa na uwezo wa kumshtaki pesa nyingi Wizara ya Fedha inadaiwa, basi hapo mimi nakubaliana nalo kabisa nakuunga mkono asilimia mia kwa mia.

Nikija katika ukurasa huo huo hapa kwenye kifungu cha 3(b) uendelezaji wa karafuu na mazao unatokana na hali ya alama ya mazao ni kweli kwa sababu karafuu yetu watu hawaijui huko nje, wanaona ni karafuu ya Malasia wanaonda ndio ile ile Zanzibar, lakini ikiwa karafuu yetu ina nembo kwa kweli hapo ndipo soko litakapopatikana kwa sababu sasa hivi wenzetu Uganda sasa hivi wanaotesha mikarafuu, ukangalia kwa sura utaona ni zile zile lakini twende kwenye *quality* ya Zanzibar ni nzuri wewe mwenyewe unaiona ladha yake ukiitafuna tu unajua hii kweli ni mali ya Zanzibar, lakini watu wengine hawaijui kama ni mali ya Zanzibar.

Sasa mimi nafikiria hili suala hebu tuangalie lakini nieleze suala la soko la ndani, soko la ndani la karafuu sasa hivi ni wachache wanaoijua jinsi ya kuitumia karafuu hebu na hili tuwaelimishe wananchi jinsi gani ya karafuu ina tiba gani na nini madhumuni ya karafuu hapa Zanzibar na itamnufaisha nini katika kutumia, wenzetu China hivi karibuni nashukuru sana serikali yetu chini ya dhamana Mhe. Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf kanipeleka China. Hakufanya makosa kunipeleka China tumejifunza mambo mengi sana jinsi gani wenzetu wanavyotumia soko la ndani, mimi niliwauliza suala la

magari Mhe. Naibu Spika, kama utaniruhusu niseme kichina nitasema, lakini kama huniruhusu basi.

Lakini baada ya kuuliza suala la soko la magari wakasema je, sisi wenyewe ndani hazijatutosha hatuwezi kupeleka nje magari yao mazuri sana, sasa na sisi tuangalie soko la ndani kwanza karafuu ienee ndani Mheshimiwa toa viwanda, watu walala hoi tupo sisi wananchi wetu wapo kule hawana kitu lakini zipo mashine ndogo waelimishwe, kwa hivyo naomba hili uwe mchango mkubwa kwanza tulianzishe soko ndani tupate manufaa ndio baadae tukauze nje. Lakini tukikimbia nje utaambiwa kesho soko la dunia limeanguka mwananchi utamwambiaje upunguze bei, lakini kama utamzoesha mapema hapa anajua hata ikianguka kule tayari manufaa wanayo, karafuu inatibu maradhi si chini ya ishirini mpaka thalathini, una uwezo wa kufanye kwenye mafuta mazuri, kwenye *colgate* na masuala mengine, naomba na hilo nalo ujiandae kabisa kuwaletea wananchi wetu viwanda vya ndani ili waweze kutumia na karafuu waijue nini faida yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kaka yangu alimsema hapa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi ingawa yeye kamuua lakini mimi simuui najua yupo Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu, azidi kutusaidia fikra.

Mhe. Naibu Spika, mashamba kulikuwa na vikundi *special* ambavyo hivyo kazi yake ni kuhudumia mikarafuu tu tokea kuotesha mpaka kukua na mpaka kupata maradhi, lakini leo hakuna kikundi hicho kilikuwa kikishughulia hiliki, hiliki ya Zanzibar ilikuwa ni nzuri sana tena ilikuwa ya haiba na harufu. Zao hilo sasa hivi hakuna tusione karafuu tu nalo hilo lina fedha katika nchi za Comoro na sehemu nyengine, sasa nalo tulitunze na tulienzi tulitolee kama tunavyolitolea hili la karafuu, halafu sio vibaya tukawa na *special department* inayohusiana na Mkurugenzi wa mikarafuu tu hiyo nayo tuwe nayo, hapo ndio kweli tutajua kama tumekusudia hili zao la karafuu Mhe. Rais hilo suala alisikie kwamba atuwekee kitengo hicho na kiwe na Mkurugenzi wake hapo sasa hivi tutajua kwamba karafuu tunataka kuikuza.

Mimi nasema Mhe. Rais aangalie ili tuweze kupata *department* husika ya karafuu tu pamoja na hiliki, kwa sababu sasa hivi hiliki inapotea au imeshapotea kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba mimi mchango wangu leo utakuwa kidogo wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wanaunga mkono asilimia mia kwa mia, Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kupata nafasi ya kutoa machache juu ya mswada huu uliopo mbele yetu, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kufikia hapa tukawa wazima na kuendelea na shughuli zetu za Baraza kama kawaida.

Mimi nataka nianzie na kichwa cha habari cha huu mswada wenyewe kinachosema Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara, hili neno kuanzisha kama sheria inaanzishwa ina maana huko nyuma je kulikuwa hakuna sheria hata leo ikawa

sheria ya kuanzisha, kwa sababu Shirika ni kongwe Je, huko nyumba lilikuwepo bila ya sheria si kweli ilikuwa sheria ipo.

Kwa sababu hapa imetajwa Sheria namba 11 ya 1985 na imetajwa vile vile sheria ya mwaka 1968 ina maana sheria zilikuwa zipo, sasa kichwa cha habari kinasema kuanzisha yaani sheria hii ndio inaanzisha shirika, lakini huko nyumba tayari ziko sheria ambazo zimeanzisha. Kwa hivyo kwa maoni yangu hii *heading* ya huu mswada kidogo ina matatizo, kwa sababu tayari shirika hili lipo kisheria kwa sheria mbili hizi zilizotajwa.

Mhe. Naibu Spika, Shirika la Taifa la Biashara ZSTC kazi yake moja kubwa ni kununua na kusafirisha karafuu, lakini karafuu inatokana na mkarafuu ambao hauko chini ya Wizara hii, mkarafuu uko wizara nyengine na karafuu iko wizara nyengine. Lakini huu mkarafuu ambao ndio unaotoa karafuu kwa asilimia kubwa sana unaanza kupotea pole pole na katika muda mfupi ujao mkarafuu utakuwa ni historia tu, hata kule kwetu Pemba na zaidi wilaya ya Mkoani na ukanda wa mashariki.

Sasa basi eneo kubwa ambalo zamani lilikuwa na mikarafuu leo limegeuka kuwa ni eneo la kupanda mihogo na migomba, mikarafuu imetoweka, kuna sababu kazaa zilizosababisha hivyo. Moja pale karafuu serikali ilipoizarau kwa hivyo watu waliona mkarafuu hauna maana wakaukata na kupata maeneo ya kupandia mihogo.

Jengine serikali yenyewe ilichangia kuiua mikarafuu pale walipoleta kule Pemba tulikuwa tunaiita idara ile inaitwa *diabak* hao walikuja kuiua mikarafuu tu hakuna kazi nyengine waliyofanya ilikuwa kazi yao ni kuikata wakiipaka lami, sijui kama ilikuwa lami au dawa nyengine na hatimae mikarafuu ilianza kufa pole pole na hivi sasa inaendelea bila ya kizuizi. Bahati mbaya hakujakuwa na mkakati madhubuti wa kutuhamasisha juu ya upandaji wa mikarafuu mipya, linapozungumzwa hili ninatoa mfano wa Gando kulikuwa na kijishamba ndio mfano pekee unaotolewa hatupandi tu mbonga Gando kuko hivi, sasa nchi nzima kama iko Gando tu haijakuwa ni mfano ya kusema kwamba mikarafuu inakua, watu wanapootesha mikarafuu au wanapopanda baada ya miaka mitatu au minne katika baadhi ya maeneo yetu inaanza kufa vile vile.
Mhe. Salehe Nassor Juma hapa alisema kuna haja ya kufanya utafiti wa kina juu ya hili zao la karafuu, kwa hivyo shirika lisingojee karafuu tu kununua kwanza wautafute huu mkarafuu washirikiane na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Biashara kutafuta njia bora za kuimarisha, kuendeleza, kuutunza huu mkarafuu ili hatimae hiyo karafuu ipatikane. Kwa sababu mkarafuu ndio unaoleta karafuu.

Mhe. Naibu Spika, katika mswada huu Shirika la Biashara la Taifa la ZSTC linasema kuwa linanunua karafuu kwa ushindani, lakini mimi nitoke hapa niende barabarani mbio peke yangu hakuna anayenikimbiza halafu niseme nashindana, nakwenda mbio peke yangu hakuna anayenifukuza sasa nashindana na nani, halafu nikajifu nimetokea wa kwanza mpizani wangu ni nani. Kwa hivyo hapa hakuna bei ya kushindana kuna bei Shirika iliyojipangia wananunua kwa bei waliyojipangia lakini hakuna ushindani wa mtu peke yake, kwa hivyo hili neno ushindani katika bei halifai kwa sababu hakuna anayeshindana nae ananunua peke yake anasafirisha peke yake pia anauza peke yake, hashindani na mtu yoyote wala shirika lolote wala chombo chochote.

Halafu Mhe. Naibu Spika, katika hii sheria ya 1968 ambayo imetajwa kwamba ni sheria ya karafuu, iliyotaja kuwa mtu yoyote atakayesafirisha karafuu kwa magendo atachukuliwa hatua pamoja na karafuu zilizohifadhiwa, sasa kitu kimefanywa ndani ya nchi kulingana na hii sheria ya mwaka 1968 inaonyesha kuwa kuhifadhi ni kosa. Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa sisi Wazanzibari hasa kule Pemba hatuhifadhi pesa katika karafuu tunahifadhi zile karafuu na pale inapotokezea haja ndipo karafuu inapouzwa kwa kutekeleza ile haja yake, mimi nilipochaguliwa kuingia darasa la tisa huo mwaka niliochaguliwa babu yangu alichota karafuu pishi tatu akenda kuziuza akanipeleka kwa baniani kupima *uniform* ya kuingia darasa la tisa, kishati cheupe na kisuruali cheusi kipande.

Kwa kuwa aliitaka haraka haraka alitumia shilingi kumi na sita (16) wengine hapa shilingi kumi na sita hawazijui hakuhifadhi pesa alihifadhi karafuu ilivyotokea haja akauza karafuu, leo tunatakiwa tuhifadhi pesa sisi wa Pemba pesa haihifadhiki pesa ukiwa nayo ndani unaitumia tu. Kwa hivyo ningeomba kifungu hiki cha sheria kisitumike bado watu waaminifu waendelee kuachiwa kutunza karafuu zao majumbani na wauze pale haja itakapotokea.

Mhe. Naibu Spika, halafu kuna hii sheria ya 1968 ambayo imetajwa kuwa imefutwa, lakini itaendelea kutumika yale ambayo yameshapitishwa kwa mujibu wa sheria hii, sasa Mheshimiwa Naibu Spika, sheria imefutwa lakini imeambiwa itatumika chini ya sheria hii sijui imefutwa vipi, imetajwa imefutwa lakini yale yaliyoandaliwa kwenye sheria hii yataendelea kutumika pamoja na kwamba hiyo sheria imefutwa. Kwa hivyo huo mfuto wenyewe ningemuomba Mhe. Waziri anifahamishe imefutwaje halafu ikabidi mambo yake yaendelee kutumika pamoja na kuwa sheria yenyewe imefutwa.

Mhe. Naibu Spika, karafuu ina daraja zake kuanzia kupandwa kwa mkarafuu, kulea, kutaka kuzaa, kuchuma na hatimae kuuza hizo karafuu, hapa kuna hili kundi kubwa la wachumaji wachumaji wa karafuu ni miongoni mwa kazi moja ngumu kama zilivyo kazi nyengine zilizokuwa ngumu, kwa sababu hii inamfanya mchumaji abakie juu ya mti kwa muda mrefu yaani katika kuchuma na akiteremka kuna kazi nyengine mpya ya kuhesabu shada moja baada ya moja yaani kuzichambua.

Kwa hivyo hizi ni kazi mbili kubwa na ngumu mchumaji ambae ni mchumaji barabara anaweza kufika saa sita au saba bado hajalala na kesho akiamka anakwenda kuchuma nyengine, sasa pamoja na kuwa bei ya mchumaji kidogo imetononeshwa lakini iko haja ya mchumaji kumuangalia zaidi na yeye kutokana na kazi ngumu anayoifanya. Kwa sababu siku nzima yeye yumo kazini tu akipumzika usiku mkubwa na asubuhi mapema anatoka tena, kwa hivyo ipo haja ya kumuangalia zaidi hii bei ya shilingi elfu mbili kwa sababu wenye karafuu kidogo na wao ni wagumu walikubali kwa shingo upande na pengine kwa mbinde ilikuwa hawataki kuwapandishaia bei hiyo.

Lakini ingelitizamwa hii pishi moja ambayo analipwa shilingi elfu mbili mchumaji wa karafuu, femilia nyingi za Pemba mchele wanaokula ni kweli kweli kuna watu wanakula kilo mbili mpaka tatu na hawashibi, sasa achume pishi ngapi ili apate chai chakula cha

mchana na cha usiku na apate akiba kidogo ya kutafuta *uniform* za watoto na kanga ya mama watoto. Mpaka awe mchumaji mzuri ndio aweze kumiliki yote hayo kwa hivyo iko haja ya kumuangalia, mara nyengine mchumaji huyu hutoka na bahati mbaya akaanguka anapoanguka huko nyuma sana kidogo walikuwa wakihudumiwa na kusaidiwa kwa fidia ndogo, lakini hapa kati kati serikali ilikatisha huduma hii. Kwa hivyo ningeliliomba shirika au wizara husika huduma hii wairejeshe tena ili kuwapa moyo hawa wachumaji ambao wanapata ajali wakati wa kufanya hiyo kazi.

Halafu hili Shirika lina wafanyakazi Unguja na Pemba nasema Unguja zipo karafuu lakini Pemba zipo zaidi sina hakika ni upande upi wenye wafanyakazi wengi, kama wapo wengi Unguja ningeomba wawepo wengi Pemba kwa sababu ndio kwenye kazi zaidi kuliko huku Unguja na kama Pemba wapo wengi ndio sawa sawa. Kwa hivyo ningeomba kujua hawa wafanyakazi wapi kuna wengi zaidi lakini pia kwa kuwa ni kazi ya msimu sio endelevu ni kazi ya mwaka hadi mwaka, tuwaajiri watu ikiwa hakuna msimu ule mzigo usiwe mkubwa wa kuwalipa watu bila ya kufanya kazi kwa kipindi kirefu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache niseme kidogo kuhusu hii biashara ya magendo ya karafuu tumelipokuwa kwenye kamati tulikwenda katika Makao Makuu ya KMKM. Kwenye mazungumzo yetu tuliwauliza ilikuwaje nyinyi mnakamata karafuu siku zote lakini yule aliyekamatwa na karafuu hapatikani. Wakatujibu vizuri kuwa mara zote wale watu hatuwakuti nje yaani baharini hasa. Kwenye doria zetu tunawakuta bado wamo kwenye mikoko humu kwa hivyo wanapotuona wao wanakimbia sisi boti zetu haziwezi kuingia kule. Kwa hivyo wao wanakimbia kwa hivyo sisi tunabaki na hii mali tu. Inawezekana ikawa hoja yao ni ya kweli na inawezekana ikawa ni kwamba wametujibu tu. Hivyo ni kweli siku zote hizo hawajawakuta mkondoni. Siku zote wanawakuta humu mbago mbago ya bahari tu.

Mimi siwezi nikasema kuwa na wao wanashiriki kwa sababu sina ushahidi wa kisheria. Lakini labda kimazingira nahisi kuna haja ya kuimarisha huu ulinzi wa baharini ili hii karafuu isipenye.

Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Spika, ningerudia msemo wangu ule ule niliochangia wakati wa bajeti ambao Mhe. Waziri hakufurahikiana nao kuwa pale anapokamatwa mtu risasi isitumike. Kwani hasa karafuu ina nini? Ikiwa serikali ime *hand over* biashara zote lakini karafuu hawataki kuitoa. *What is inside it?* Ndani yake kuna nini? Mambo yote yalikuwa yamedhibitiwa na serikali, hata kanga ilikuwa tunauziwa na serikali, vitambaa vya serikali, kila kitu. Serikali ilikuwa imemiliki mambo yote lakini hatimaye waliyaacha yote, lakini karafuu wamekataa kuitoa. Inaonesha kuwa hawaitowi hasa. Kuna siri gani ndani ya karafuu. Wakati karafuu imekaa kama chumba cha mganga mkubwa sana anakwambieni vyumba vyote fungueni lakini hichi msifungue. Na serikali imesema biashara zote tutawaachia lakini hii hatutoi. *Why*? Kwa nini? Biashara zote fanyeni lakini hii hatutoi. Toeni bwana, kwa sababu na hii nayo ni biashara.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi Magharibi haya kumpa fursa ya kuchangia kidogo katika Mswada uliyokuwepo mbele yetu. Kwa ujumla na mimi ni mjumbe katika Kamati ambayo ilipitia Mswada huu kwa hiyo sitokuwa na mengi ya kuzungumza isipokuwa kuna kidogo tu na mimi nitapata kutoa dukuduku langu.

Mhe. Naibu Spika, katika kikao kilichopita cha Bajeti nilichangia ubinafsishaji au ukarabati wa Shirika la ZSTC. Nilitoa maoni yangu sana na nikasema sijui ni kwa sababu gani serikali inang'ang'ania katika kulifanyia ukarabati shirika hili.

Mhe. Naibu Spika, ninachokijua au kinachojulikana na wengi kwamba hili Shirika la ZSTC haliendi kibiashara au ni bovu kabisa. Hivi sasa lina madeni yasiyopungua bilioni 3. Lakini bado serikali inataka kulipa mzigo mwengine, japo wamekuja na lugha nyengine. Kwa sababu wanasema tunataka kuanzisha Shirika jipya la ZSTC kwa sheria nyengine.

Lengo kubwa ni kununua hizo hizo karafuu. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, kutokana na ongezeko la bei ya karafuu litahitaji shirika lipate mtaji wa serikali na ndio sheria inavyosema. Mtaji huu wa serikali kutokana na ongezeko la bei utakuwa ni mkubwa sana. Mimi nahofia kwa vile watendaji wetu hawatotoka mbinguni ni wale wale ambao wanatokana na sisi Wazanzibari tukaja tukaitia serikali hasara kubwa. Hakuna shirika hata moja katika nchi yetu ambalo linafanya vizuri. Shirika la Biashara ninavyojua mimi linakwenda vizuri, lakini nasikia linafungwa.

Mhe. Naibu Spika, hili Shirika la Biashara ya karafuu kwamba linafufuliwa vyengine kwa mtaji wa serikali, hizi pesa tunazihitaji kwenda katika sehemu nyengine za maendeleo. Utendaji watu kama tunavyoujua hatuna uwajibikaji unaotosheleza. Nahofia hapo mbele tukaja tukakwama tena na pesa tukawa tumeshaziingiza nyingi sana katika kulifufua shirika hili. Mimi ningeona serikali labda wasing'ang'anie sana, wangetafuta njia za kununua karafuu kama vile walivyokwisha kuweka sheria.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kusema ni kuhusu adhabu. Katika kifungu cha 22 kimewekwa adhabu ambao watakaopatikana na kosa aidha watafungwa miaka mitano au wengine watatozwa faini. Hii mimi nafikiri kwa mfumo tunaokwenda nao hivi sasa wa kufufua tusitumie tena kufufua shirika na kutaka mikarafuu ipandwe, iendelezwe. Utaratibu huu wa kuwafunga watu usiwepo.

Kuna utaratibu mwengine Mahakamani wa vifungo vya nje, hakimu anayo haki ya kusema atafanya vipi au watafanya vipi. Labda hiyo adhabu atakayopewa kwamba aende jela basi aende katika utaratibu mwengine wa kupewa adhabu ya kupanda mikarafuu, faida yake tutaiyona. Tukisema kwamba sisi mtu huyu tunakwenda kumuweka jela kwa sababu mwengine asiende magendo. Hiyo sio sababu ya kusema kwamba sisi tukimuweka ndani au tukimfunga wengine hawatokwenda. Watakwenda kwa kutafuta bei. Na wakijua kwamba ninakokwenda nitafaidika.

Mimi ningependekeza hapa wasingelifanya hivyo. Tungeliamua kuweka adhabu ya kupanda miti mpaka ifikie kiwango, ili taifa linufaike na sio kumuweka mtu ndani hii ni nguvu mali. Hasa tujenge mawazo kwamba hii karafuu ni mali ya mtu sio mali ya serikali. Bado ni mali ya mtu binafsi, tumeweka sheria tu kiasi kwamba mtu hana uhuru wowote wa kuitumia hii mali yake yeye mwenyewe. Sasa leo atajisikia vibaya kwamba mali yake mwenyewe imempeleka ndani kwa matumizi ambayo anayajua yeye mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo kidogo nakwenda kwenye ushindani wa bei. Katika vifungu vilivyotajwa humu tumeona kwamba shirika limekusudia au katika kazi zake ni kupanga ushindani wa bei. Tuchukue mfano wa Shirika la Uzalishaji wa Mwani. Mwaka uliopita wa 2010 walijitokeza wanunuaji wa mwani. Baada ya kujitokeza kwa wanunuaji wa mwani mwani umepanda bei, kutokana na kwamba kulikuwa kuna Kampuni moja, mbili, tatu, nne zinazonunua mwani. Hivi sasa wakitwambia ZSTC Shirika ambalo litakuja litaweza kununua mwani litaweka ongezeko au bei itakuwa ni nzuri, wao ndio wame – *monopolies* kila kitu si dhani. Labda katika kifungu hichi cha nyuma kwenye kifungu cha 9 wameelekeza wamesema kwamba kutakuwa na wadau, watashirikiana na watu wengine binafsi.

Mimi ningeomba hao watu wakawaanzisha mapema. Kama utaratibu mwengine ufanyike lakini kwa njia hii bei itadorora. Wananchi hawatakuwa na hamu ya kuendelea. Hivi sasa ulimwengu uko wazi, kila mmoja anajua bei ya soko ikoje. Sasa wewe unampangia unamwambia mimi nitanunua karafuu yako kwa 200 atakuwa hana hamu hata ya kuupanda huo mkarafuu akijua bei iko vipi ulimwenguni na yeye analipwa vipi serikali yake au hilo shirika lililopo. Naomba na hilo tulizingatie.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kifungu cha 22. Kifungu hichi kinasema kwamba mtu yeyote ambaye bila ya kibali cha shirika atanunua karafuu. Sasa pale pa kununua bila ya shaka atakuwepo na muuzaji. Ningeomba Mhe. Waziri akalizingatia hilo labda tungeliongeza katika kifungu hichi atanunua na atauza. Kwa sababu haiwezekani akawa atanunua mtu, kutoka wapi saa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba niunge mkono hoja.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Shirika la Kuanzisha Sheria ya Taifa ya Biashara. Ni wakati nzuri sana kulichangia shirika hili, hasa kwa utekelezaji wake mzuri wa kupata ununuzi wa karafuu kwa wingi kipindi hichi cha mwaka wa fedha.

Shirika limeanza vizuri kushughulikia shughuli za karafuu. Karafuu ni uti wa mgongo wa nchi yetu kwa hivi sasa linakwenda vizuri na tunakwenda nalo vizuri. Shirika linafanya ununuzi mzuri, linafaa kupewa hongera, hasa Waziri wa Biashara kwa kuongeza ya karafuu kwa wakati huu.

Isitoshe zao la karafuu sio peke yake kama lilivyozungumza Shirika lenyewe litakavyoshughulikiwa. Ukuzaji uongezwe kwenye mazao mengine ya wakulima, hasa

yale mazao yanayokaushwa, ili yafanane na zao la karafuu. Mambo ya kuyapa kipaumbele hivi sasa kuweza kushindana na zao la karafuu ili nchi iweze zaidi kupata maendeleo. Namuomba Mhe. Waziri aendelee kutoa kipaumbele kwa zao la mwani ili liweze kupambana na zao letu la karafuu. Huenda tukapata fedha za kigeni zaidi ambazo zitatupa tija hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa zao la mwani ni zao la kutia tama, kwa sababu linakaushwa sawa na lile zao la karafuu. Zao la karafuu hatukuweza kupata muhisani yoyote kutoka Marekani au Uingereza au India kuja hapa Zanzibar kusema leteni karafuu nitawapatia fedha nyingi au nitawaongezea bei ya zao la karafuu. Serikali ilisimama wenyewe kutoka nje ya Zanzibar kwenda nchi za nje kutafuta fedha ili kulitangaza zao la karafuu kupata fedha ili kuweza kuendesha nchi yetu. Hivi sasa ni vyema kama tulivyotoka kutafuta zao la karafuu tukaweza kugundua kwamba bei ni nzuri ya ulimwengu na tunaweza kushindana popote katika ulimwengu kuuza karafuu zetu.

Hivi sasa ipo haja tuweze kutoka tena kwenda nje kufanya utafiti wa zao la mwani ili kupata fedha za kigeni kuweza kuendesha nchi yetu kwa vizuri. Mazao ni mengi ya kukausha yanaweza yakaleta tija katika nchi yetu ili, hasa kwa kuwasaidia wakulima wazalishaji amali.

Hivi sasa tuna uwezo wa kulizungumzia zao jengine la majongoo ambayo yanalimwa katika bahari sawa sawa na mwani. Zao la majongoo kama tutatoka kweli kwenda nchi za nje hasa nchi za wenzetu ambazo zinatumia majongoo. Sisi Zanzibar hatujui faida ya majongoo lakini kama tutakwenda mbio kufika China au Japani, Marekani, tunahakikisha kwamba dola tutakazozipata Zanzibar zitafanana na kuweza kuchimba mafuta kwa wakati wowote. Wenzetu zao majongoo wanalithamini sana ingawa sisi hatujui linatumiwa vipi, lakini wenzetu wanajua jongoo linatumika vipi. Tukilikausha likiwa safi kama tunavyozikausha karafuu hapo tunaweza tukapata Euro ama dola katika nchi yetu ya Zanzibar. Nafikiria Mhe. Waziri aanze kutumia *back benchers* wa Baraza hili wakati wao wa mapumziko ya tarehe 26 wakirudi majimboni, iwape nafasi *back benchers* kutoka nje ya nchi, kwenda kutafuta biashara.

Pia mapezi ya papa yakikaushwa ni pesa nyingi kwa nchi yetu. Hivi sasa tunao papa ambao hatujui tunawatumia vipi, tunawatumia kwa kitoweo tu. Wakati mapezi ni biashara kubwa nchi za nje. Kwa hivyo tusiangalie tu biashara ya karafuu kumbe tuna rasilimali nyingi za kuweza kuzidisha mapato hapa Zanzibar na tukaweza kuwa matajiri kuliko nchi nyengine za ulimwengu wa leo.

Tuna hakika kama tutashughulikia kukausha kamba hizi za usumba hivyo tunawezekana tukafanikisha zaidi kupata dola ya kuhakikisha nchi yetu inakwenda vizuri. Kuhakikisha kwamba zao la karafuu tunalibeba na linakuwa linafanana na mazao mengine ambayo yapo nchini lakini hivi sasa hatuyatilii maanani. Mhe. Waziri tunaomba uyatilie maanani sana katika Shirika hili jipya litakaloundwa la Taifa, lihakikishe vitu vya kukausha isiwe karafuu peke yake liwe na mazao mengine ambayo yanahitajika sana nchi za nje.

Tukikumbuka hapa Zanzibar zao kubwa zaidi ya karafuu ilikuwa pilipili hoho. Ilikuwa inakaushwa safi sana na hivi sasa inatakiwa sana katika ulimwengu wa leo. Hasa tukifua nchi nyingi sasa hivi zinapambana na vita vya dunia hii. Mabomu ambayo yanatumika mazuri ni mabomu ya pilipili hoho. Kama tutaitumia pilipili hoho kuikausha vizuri ni wazi kwamba inawezekana tukapata masoko katika ulimwengu na tukaweza kuondokana na umasikini tunaouita umasikini. Zanzibar sio masikini kwa sababu ina mazao mazuri ambayo nchi nyingi haina katika ulimwengu wa leo. Si nchi nyingi ambazo zinaweza kulima pilipili hoho, hata kuzifahamu zinatumika vipi au zinalimwa vipi hawafahamu. Wao wanaziona wanapelekewa zimeshakaushwa tu. Sisi ndio tunajua vipi pilipili hoho tunavyozipata hapa nchini.

Naliomba shirika hili lisisitize na litoe bei kinaga ubaga hasa pilipili hoho itanunuliwa bei gani, kama inavyotoka bei ya karafuu. Mashamba mengi yanaweza kulimwa pilipili hoho baada ya kujua wananchi wanaweza kuuza kiasi gani katika shirika hili. Kama hivi sasa ilivyokuwa yanalimwa mashamba ya mikarafuu usiku na mchana kwamba bei zake wanavifahamu kinaga ubaga.

Mhe. Waziri ahakikishe kwamba kila sekta ambayo anaitaka kuifanyia mazuri au kuianzisha katika Shirika hili la Taifa la Biashara aitangaze kama anavyotangaza bei ya karafuu kwa faida ya wakulima wetu hapa nchini.

Pia zaidi nampongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara kwa juhudi zake za kuweza kulingaza shirika hili kwamba litakuwa ni shirika bora. Litakwenda kileo na kisasa hasa kwa kuzidisha kutoa Wajumbe wake wa *back benchers* wa Baraza la Wawakilishi kwenda nchi za nje kutafuta masoko wenyewe na kuleta hapa nchini. Hivyo asiwe na muda mrefu sana ili kuhakikisha mapumziko ya mwezi unaofuata tarehe 26 apange vijana wazuri ambao wanaotoka katika Kamati zetu, waweze kwenda nje kutafuta masoko ya nchi yetu. Tusikae tu kwamba tumepata nafasi ya mapumziko, tunarudi majimboni lakini tuhakikishe na nje tunakwenda kuweza kupata masoko ya biashara kwa ajili ya nchi yetu ya Zanzibar. Zanzibar nahakikisha sio nchi masikini, Zanzibar ni nchi tajiri katika nchi tajiri za ulimwengu wa leo.

Mhe. Naibu Spika, kwa yote tuliyoyazungumzia kuhusu mchanganuo wa Shirika letu jipya la taifa la biashara na kuweka masharti bora kwa ajili ya usarifu, uendeshaji wa uzalishaji biashara, ukuzaji wa karafuu na mazao mengine yanayohusiana na mazao ya wakulima. Mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tunaunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Allah kwa uwezo wake kujaalia jioni hii, kusimama mbele ya Baraza hili na mimi kuweza kutoa mchango wangu katika sheria hii ya kuanzisha Shirika la Taifa la Biashara na Kuweka Masharti Bora kwa Ajili ya Usarifu, Uendelezaji, Uzalishaji, Biashara na Mambo Mengine.

Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wengi wameshachangia sana katika sheria hii. Lakini kwa vile na mimi sina budi kutoa mawazo yangu, mawazo haya nitaanza katika kifungu cha 4 Sehemu ya Pili kinasema "Kuanzishwa kwa Shirika la Biashara la Taifa ZSTC"

Mhe. Naibu Spika, hapa kwanza niipongeze serikali kwa kupitia Wizara ya Biashara, kwa mawazo yao waliyoona kwamba kuanzisha huku lakini kulibakisha jina takatifu ZSTC. Nimeona ni vyema kuwapongeza, kwa sababu shirika hili ni shirika moja mama ambalo linaitangaza Zanzibar katika nchi mbali mbali duniani. Karafuu yetu inapata soko zaidi kwa kupitia jina hili la ZSTC. Kwa hivyo si vibaya kuwapongeza wenzetu watu wa Wizara ya Biashara kuweza kuliona kwamba tuendelee kuwa na jina hili hili la ZSTC.

Mhe. Naibu Spika, tumo katika kupitisha sheria ya Shirika hili. Inaelekea kwamba huko tulipoanza kulikuwa kuna mapungufu mengi. Halafu kulikuwa kuna mrundiko wa wafanyakazi wengi. Haliyakuwa uzalishaji kwa wakati huo ulikuwa ni mdogo. Kwa hivyo kwa makusudi serikali ijaribu kuliangalia upya hili shirika ili liweze kuwa lina meno ya kuweza kufanya kazi zake kiumakini.

Mhe. Naibu Spika, ninaloliomba sana kwa shirika hili, sisi Wazanzibari tunahitaji kuwa na Shirika lililokuwa bora sio ubora wa Shirika. Ni lazima sasa tulete mabadiliko kwa Zanzibar na wananchi wa Zanzibar sio mabdiliko ya wanashirika.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea katika kifungu cha 6 kuna malengo mbali mbali ya shirika. Nataka nitoe mchango wangu mfupi tu katika kifungu cha 2(ii)(a) kuna malengo mbali mbali shirika hili linalokuja limejiwekea ili kuweza kulinyanyua zao la karafuu na wazalishaji wa karafuu. Wamekusudia kutoa huduma za aina mbali mbali za kilimo, vifaa, mbolea na utaratibu wa uvunaji.

Nataka nitoe mawazo yangu katika, utaratibu wa uvunaji wa zao la karafuu. Mheshimiwa katika zao moja gumu ni zao la uvunaji wa karafuu. Usumbufu wake ni mkubwa mpaka ukiipata hiyo karafuu. Mara nyingi serikali inaangalia karafuu sio mkarafuu. Kwa hivyo tunaliomba sana shirika hili haya maandiko waliyoyaandika yafanyiwe kazi, yasibakie katika kumbukumbu.

Mchumaji wa karafuu huondoka nyumbani asubuhi saa 2 inawekana akarudi nyumbani saa 12. Sio kwamba akifika nyumbani huduma imekwisha, hapana. Anaendelea na kuisafisha karafuu ile. Inaweza ikafika saa 4 za usiku bado hajalala. Kwa hivyo katika uvunaji huu bado mzalishaji huyu ni kibarua hatujamuangalia vizuri. Tumeangalia tumeangalia kwamba kibarua analipwa shilingi 2000 kwa pishi. Lakini Mhe. Naibu Spika, ukizingalia shilingi 2000 kwa masaa hayo kwa kweli hazimkifu kibarua. Ni vyema shirika likamuangalia huyu sana kwa sababu kama hakuangaliwa itafika wakati basi karafuu zitaanguka wenyewe kwani karafuu ina kazi kubwa. Kwa hivyo, kwa shilingi 2000 anazopewa kibarua kwa matangazo ya shirika hii ni ndogo, baada ya kibarua kuisafisha karafuu iliyobaki ni kazi ya mkulima mwenyewe ya kupima na kuianika karafuu ile mpaka ikaweza kufika ZSTC.

Mhe. Naibu Spika, tunasifu sana kwamba karafuu bei ni kubwa, mimi nasema sio kubwa kwani hali hii ni kama ya yule kipofu Mwenyezi Mungu alipomjaalia macho akaona akaona jogoo halafu akaleta upofu tena, ikawa kila anapokwenda anasimulia kwamba hakuna mnyama mkubwa kama jogoo. Lakini mimi nasema bei hii sio kubwa ni ndogo mno. Mhe. Naibu Spika, mara zote wakulima wetu wanapoingia katika mfumo huu wa karafuu wanapomaliza biashara ile basi hapana aliyekuwa na akiba, pesa zote zinakwenda katika gharama.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa hii bei tuliyonayo basi wananchi wote wanapomaliza kwa sababu watu hawafanyi tathmini mapema itakuja kuonekana kwamba faida inayopatikana haimpatii kijio cha wiki tatu. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri tuliangalie sana soko la karafuu na kuwanyanyua wakulima wetu wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kama karafuu hazikupanda katika soko la dunia leo tusingelikuwa na mazungumzo haya, ingelikuwa karafuu bado inadharauliwa wala haina msukumo wa aina yoyote. Lakini kupanda kwa zao hili na sisi ndio tukaanza kukurupuka tukasema karafuu sasa tutainunua kwa bei. Mhe. Naibu Spika, kwa nini wakati karafuu imepata bei, kwa nini mwananchi wetu asifaidike tukaona kwamba shilingi 15,000 kwa kilo moja mkulima inamkifu. Hapana, ni vyema shirika hili likawa na huruma kwa sababu shirika mwenzake ni mkulima. Kwa hivyo, ningeliomba serikali hiki ni kipindi cha kufaidika wakulima wa karafuu, wewe huoni lazima wakulima wetu wa karafuu wafaidike, tusiwe na hesabu kwamba shilingi 15,000 kwa kilo ni nyingi. Kwani pesa zile zinarudi wapi? Pesa ile inarudi hapa hapa serikalini kwa hivyo fursa hii Mwenyezi Mungu aliyotuletea ni vyema serikali ikawaonea huruma sana wananchi wetu wakaweza kumudu maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, katika kuivuna hii karafuu hapa panahitaji taaluma kwa wakulima. Mheshimiwa kama shirika litatoa elimu kwa wakulima kuna tatizo kubwa wakati wa kuvuna karafuu, kwani mikarafuu mingi inakufa kutokana na kuwa inakatwa matawi na kubakishwa juu ya mikarafuu. Kwa hivyo, kwa hali hii ni vyema shirika sasa liweze kutoa elimu kwa wakulima ili kuinusuru hii mikarafuu iliyobakia iweze kurudi katika yake ya kawaida ili kila mwaka serikali iweze kuingiza mazao ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kifungu cha 7 tokea asubuhi tunapiga kelele sana kwamba wananchi karafuu wanaziuza magendo. Mhe. Naibu Spika, mimi hili linaniumiza sana kusema kwamba wananchi ndio wanaouza magendo, ni mawazo mazuri lakini mimi naona kwamba sio wananchi wanaouza karafuu magendo ni serikali na vyombo vyake. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tamaa ya maisha imekuwa kubwa, mtu anapopata nafasi anataka ndio uhai wake na wajukuu zake na wanaokuja waweze kuishi kwa ule muda wake yeye. Kwa hivyo, tunapokosa usimamizi na kuweka mbele tamaa ya maisha ndipo unapomlazimisha sasa mwananchi akufuate vile unavyotaka wewe. Kwa hivyo, lawama tusiwatupie tu wazalishaji wetu, kwa sababu usimlaumu mtu kama hujajiangalia wewe, kwanza jiangalie mimi nataka nimlaumu mimi je nikoje. Hivyo, kweli lawama hizi zitamdhuru au nitadhurika mimi.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba kila siku tunapiga kelele kwamba wananchi karafuu wanazisafirisha magendo, wanafanya hivi na hivi na nchi hii ina vikosi havipunguu 12 vya ulinzi vya Muungano na vya Zanzibar karafuu hii itatokaje iuzwe magendo. Kwa hivyo, kwa hali yoyote itakuwa serikali inashiriki, hivyo hebu kama tuna ukweli wa kuyadhibiti magendo kwanza tuwadhibiti hawa watendaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, huko tunakotoka karafuu imeshachukuliwa katika yale maghala na ikasafirishwa magendo. Kwa hivyo, kama hatujajisafisha sisi watendaji itakuwa mwananchi tunamuonea, hivyo ni vyema ukitaka msema mtu aibu zake kwanza taja zako. Kwa hivyo, lazima tubadilike na kama hatukubadilika tutaweka sheria elfu kwa elfu lakini mwenendo wetu utakuwa ndio ule ule kazi yetu itakuwa ni kurundika masheria yasiyo fanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo mimi naipongeza sana serikali hii ya awamu ya saba, lakini ule moto uliokuja nao imefika pahali sasa inaanza kupwaya. Mimi nasema kwamba watendaji wetu sio malaika kwamba ni watakatifu hawana baya, hilo haiwezekani. Hebu kama serikali imekusudia kuondosha magendo Mhe. Asaa amesema asubuhi kwamba hivi sasa karafuu zinasafirishwa magendo, na kumewekwa ulinzi kila kituturi cha barabara. Mhe. Naibu Spika, kama utatoka Mkoani mpaka ufike Konde basi si chini ya vituo 7 vya polisi na ngazi mbali mbali wameweka mle kuzuia watu na gari zinazopita na mizigo, tena maeneo mengine ni hatari ya kusababisha ajali ya wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, hili halisaidii mimi ningelikushauri sana Mhe. Waziri kuondosha magendo ya karafuu ni kumlipa vizuri mkulima wa karafuu hakuna jengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo mimi ni miongoni mwa kamati hii ningelimuomba sana Mhe. Waziri wetu maoni yetu ayakubali, tumuweke vizuri mkulima afaidike kwa hatua hii tuliyonayo leo na ili tuondoshe haya magendo basi ni kumpa kipaumbele mkulima na hakuna mkulima atakayemuuzia mtu mwengine kinyume na serikali yake hii tuliyonayo ya awamu ya saba. Kwa maoni yangu hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono mswada huu mia kwa mia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii na naomba nitoa mchango wangu kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri kwenye mswada huu muhimu ambao kwa kweli unagusa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kifungu cha 7 cha mswada huu kwenye kazi za shirika, kifungu cha 7 (2a) Mhe. Waziri ametwambia kwamba kazi moja ya shirika itakuwa ni kununua, kuuza karafuu na mambo mengine ya kilimo kwa bei ya ushindani. Mhe. Naibu Spika, hata kwenye Kiengereza kumeandikwa ushindani wa bei na hata kwa lugha ya kawaida ya mitaani, ushindani maana yake kuna mtu (a) na (b) huo ndio ushindani. Kwa hivyo, shirika hili linakuwa ni peke yake sijui ushindani huo utakuwa ni wa aina gani. Mimi ni miongoni mwa watu ambao wanasema kwamba Shirika la ZSTC ni letu ni muhimu kuwepo lakini ili kuwafanya wafanyakazi kuongeza tija kwa taifa lazima kuwe na chombo chengine ambacho watashindana kwenye kununua zao la karafuu kama ambavyo wakulima wanashindana kwenye kuzalisha zao lenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kuwaachia shirika hili kuwapangia maslahi wakulima kwa kweli ni dhahiri kwamba kuna mwelekeo wa kuwaonea wakulima. Mhe. Naibu Spika, mimi nina wasi wasi kwamba mswada wenyewe kwa nini umezingatia karafuu tu, usizingatie kilimo chengine. Kwa hivyo, nikusema kwamba pengine mswada unakusudia kuwabagua Wazanzibari kwamba Mzanzibari kwa karafuu tu ndio wanazingatiwa, lakini mazao mengine mtu ajifanyie anavyotaka. Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri aje na njia muafaka ya kuleta ushindani kwenye shirika hili ili tuweze kupata tija kwa taifa letu na Wazanzibari waweze kunufaika.

Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ambacho ningezungumzia hicho hicho cha 7 (h) hapa Mhe. Waziri amezungumza kwenye mswada huu kwamba kazi nyengine ni kusambaza vifaa vya usimamizi wa shughuli, majengo, utengenezaji wa vituo na kuzuia maghala. Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri wakati tunatunga mswada huu kwa ajili ya kuhifadhi maghala hayo, hivi leo Zanzibar tuna maghala mangapi? Zipo taarifa kwamba maghala mengi ya wizara yake mengine yamegeuzwa nyumba na mengine yamegeuzwa maduka.

Kwa hivyo, leo Mhe. Naibu Spika, tunaambiwa kwamba mswada huu unataka kulinda maghala na kuyatengeneza wakati maghala yenyewe tayari watu wameshayagawa na mengine yameuzwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atwambie kwamba wakati mswada huu unakuja kwa ajili ya kurekebisha mambo kwa sasa ni maghala mangapi ambayo anayo ili tujue kwamba tunaanzisha mswada huu wa sheria Zanzibar ikiwa ina maghala mangapi ndani ya mikono yetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kifungu cha 7 (q) Mhe. Waziri amesema kwamba kazi nyengine ni kufanya biashara kwa ujumla wakati wa hali ya dharura kama itakavyoelekezwa na serikali. Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani hili ni muafaka kwa sababu kwa kweli kama shirika hili lingepewa uwezo huo wa kufanya biashara leo mmong'onyoko na upandaji wa bei kiholela wa vyakula kwa kweli ungekuwa haupo. Kwa hivyo, mimi hili naunga mkono kwamba ZSTC pia ipewe uwezo wa kufanya biashara kwa dharura ili kuwaokoa Wazanzibari. Leo kila aliyepewa kibali cha kufanya biashara anauza chakula anavyotaka mwenyewe na serikali imeshindwa kuwadhibiti wafanyabiashara katika upangaji wa bei ya vyakula.

Kwa hivyo, shirika hili kwa niaba ya wananchi kama kweli litakuwa na nia hiyo basi nadhani litawaokoa Wazanzibari kwa ajili ya kufanya biashara hasa katika nafaka ikiwemo mchele, ngano, maharage na mambo mengine. Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari kwa sasa wanatumia vyakula hivi katika hali ngumu sana, hivyo shirika hili likipewa uwezo wa kufanya biashara hizi nadhani Wazanzibari watakuwa sasa na kimbilio la kufanya biashara halali na upatikanaji wa bei.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ningeligusia ni kwamba mswada huu pia unazungumzia masuala ya magendo na kwa kuwa tumekuwa tukisikia kwamba kuna baadhi ya watendaji wa serikali na hata viongozi wanashiriki kwenye masuala haya. Kwa hivyo, wakati tunaamua kuweka safu mpya ya sheria ni vyema Mhe. Waziri akatwambia kipindi hiki ni watu wangapi wamehusika na suala hilo la magendo kwa sababu zipo

taarifa kwamba watendaji wake mwenyewe ndani ya wizara yake pia wanashiriki kwenye suala hili la magendo Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine kwa haraka haraka ambalo ningependa kuligusia ni suala zima la upekuzi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inawezekana nia ya serikali ikawa nzuri kwenye kudhibiti magendo, lakini ya watendaji wa serikali wanatumia fursa hii katika kuwakandamiza Wazanzibari. Leo kila anayepewa fursa ya kufanya upekuzi basi anafanya lile analiloagizwa na lile ambalo halikuagizwa na uongozi wa wanasheria. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba hapa tuwe makini sana kwamba watendaji wetu wasitumie fursa hizi za sheria kuwakandamiza Wazanzibari kwa mali ambazo ni zao wenyewe.

Leo tulikuwa tukipokea kesi kwamba mtu ameanika karafuu zake zimechumwa, zimepimwa ziko polisi siku ya pili akaenda anaambiwa karafuu zimepunguwa. Mhe. Waziri nakuomba sana kwamba sheria hii tunaipitisha lakini izingatie maslahi ya Wazanzibari kwamba wale wajanja na wale wakandamizaji wasipate fursa ya kuwakandamiza Wazanzibari kwa mali ambayo ni yao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ningeligusia haraka haraka ni suala zima la muundo wa bodi. Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 13 kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya shirika ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi Mjumbe Mkurugenzi Mwendeshaji ningeomba sana asiwe Mjumbe wa Bodi kwa sababu yeye mwenyewe anawajibika kwa bodi. Kwa hivyo, ikiwa huyo atakuwa Mjumbe wa Bodi halafu anawajibika kwa bodi sidhani kwamba kutakuwa na haki. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mfumo huu wa sheria kwamba Mkurugenzi pia awe Mjumbe wa Bodi naomba sana uzingatiwe na ningemuomba sana Mhe. Waziri amtoe asiwe miongoni mwa Wajumbe wa Bodi kwa sababu uwajibikaji wake utakuwa ni mdogo sana ikiwa bodi inapaswa kumchunguza yeye na kumuongoza. Lakini yeye ni sehemu ya bodi wenyewe nadhani kutakuwa hakuna haki na naomba sana Mhe. Waziri huyu amtowe kwenye ujumbe wa bodi ambakishe mtendaji mkuu wa shirika hili ili yeye mwenyewe awajibike mbele ya bodi ya shirika wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ningeligusia haraka haraka ni mambo ya jumla ambayo ningeyasema kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwenye mswada huu ningependa kuzungumza mambo ya jumla, kuhusu suala zima la mashamba ya karafuu ya serikali na yale mashamba ya eka tatu tatu ambayo wananchi walipewe. Mhe. Naibu Spika, leo tunapitisha mswada huu hatujui serikali ina mashamba mangapi na hatujui serikali ilitoa mashamba mangapi ya eka tatu tatu na je, yangalipo au tayari watu wamegaiana.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wanalalamika kwamba mashamba haya sasa yanamilikiwa na vigogo. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri utwambie kwa sasa Zanzibar serikali ina mashamba mangapi yenye mikarafuu na mangapi wamepewa Wazanzibari kwa mfumo ule wa eka tatu tatu ili kulinda na kuenzi dhana nzima ya mapinduzi ya mwaka 1964 Mzee Abeid Amani Karume ambayo ametuwekewa.

Mhe. Naibu Spika, nasema hili kwa sababu inawezekana mashamba haya baada ya sheria hii kupita sasa yakasahaulika na yakawa vitega uchumi vya watu fulani na ile mali ya serikali kwa maana ya mali ya umma ikapotea ndani ya mikono ya watu ambao kwa kweli itakuwa sio haki. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba sana utakapokuja kufanya majumuisho unambie Zanzibar kwa sasa serikali yetu ina mashamba mangapi ya mikarafuu na mangapi walipewa wananchi kwa mfumo ule wa eka tatu tatu na vipi hali yake hadi sasa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo ningetaka lizingatiwa kwenye mswada huu ni changamoto. Changamoto ya kwanza ni mezani nazo ni kongwe mno wananchi wetu wanalalamika sana kwamba kadri wanavyopimiwa karafuu zao basi hakuna haki inayotendeka. Kwa maana ya kwamba mezani tangu za mwaka 1964 ndio mezani ambazo sasa hivi tunatumia. Lakini pia na pishi kule kwetu kuna pishi zinaitwa bin Abeid, pishi moja ya kawaida basi zile za kwetu sisi ni tatu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, pishi tatu za wananchi wetu ndio pishi moja ya Shirika la ZSTC, Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri ungetwambia pishi halali hasa ni kiwango gani kwa ajili ya kuleta manufaa kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni ukiritimba wenzangu wamezungumza hapa kwamba mfanyakazi anaajiriwa analipwa mshahara, anapewa over time lakini na mimi mwenye karafuu lazima nimlipe kila gunia wakati ninapouza. Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Waziri hili pia angelitwambia utaratibu huu ni utaratibu gani anaoutumia. Nadhani kwamba mtu aliyeajiriwa kwa niaba ya shirika hili basi afanye kazi ya serikali na asitegemee mgongo wa mkulima wa kawaida kwa ajili ya kunyonya ile karafuu anayoipeleka.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo Mhe. Waziri angelilizingatia ni suala zima la bima ya mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, mikarafuu mara nyingi huingia moto na inapoingia moto hakuna fidia anayoipata mkulima wa mikarafuu. Kwa hivyo, nadhani mswada huu ungeweka kifungu maalum kwa ajili ya bima ya mikarafuu pengine tungeamua kwamba kila mkarafuu uliotimia eka moja basi huo ungekuwa na bima halali ya mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, vyenginevyo uhalifu wa uwindaji wa nyuki na hata kwa bahati mbaya mikarafuu inaweza ikenda na wakulima wetu wakala hasara bila ya kuwepo kwa bima ya mikarafuu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ni fidia kwa watu wanaoanguka mikarauu nadhani mswada huu pia ungezungumza au pengine Mhe. Waziri ataniambia sheria nyengine itakuja pengine kumlinda huyu mmiliki wa mikarafuu lakini kuna haja ya kuwaangalia wachumaji wa karafuu. Leo tumeambiwa hapa kwamba kuna orodha ndefu tangu miaka ya 80 kuna watu hawajapewa haki zao pale walipoanguka. Kwa hivyo, mswada huu nini hatma ya watu hawa ambao kwa kweli wametumikia taifa hili kwa ajili ya kupata zao muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisaMhe. Waziri ajue kwamba sio watu wote Zanzibar wenye mikarafuu, mimi na wenzangu walioko ukanda wa mashariki hatujauona wala

hatumiliki mikarafuu kazi ni kilimo cha manjano, mwani na pilipili hoho. Mhe. Naibu Spika, leo bei ya manjano kule Mwambwe kilo moja ni shilingi 16,000 inalingana kabisa na kilomoja ya karafuu. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri wataalamu wako na baada ya sheria hii kufanya utafiti ule ukanda wa mashariki kwa ajili ya kuliangalia lile zao la manjano kwa ajili ya kutuwezesha sisi ambao hatuna mkarafuu kama Mwambwe, Matemwe, Nungwi, Makunduchi nadhani hakuoti mkarafuu, sisi kazi yetu ni mwani, manjano na pilipili. Kwa hivyo, nakuomba sana Mhe. Waziri utusaidie kwa hili ili kuweza kujenga usawa mbele ya Wazanzibari wetu mwenye mkarafuu uumpe kipaumbele na mwenye manjano basi utusaidie kitaalamu ili na sisi tuweze kupata matunda yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono mswada huu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi nadhani itakuwa ya mwisho kutia baraka zangu katika mswada huu ambao tunaunda shirika muhimu kweli kweli la biashara. Mhe. Naibu Spika, mimi sisemi kama ni mtaalamu wa karafuu, lakini nina uzoefu mkubwa wa karafuu kwa hivyo hayo nitakayoyasema hapa nitakuwa nayasema kwa uhakika kabisa.

Mhe. Naibu Spika, labda kama walivyoanza wenzangu na mimi nianze katika mambo ya jumla kabla sijaingia kwenye huu mswada wenyewe. Kwanza naipongeza serikali kwa kuongeza bei ya karafuu hili ni jambo muhimu sana kwa sababu kuna wenzangu waliotangulia kusema hapa tulifika wakati sasa tukawa tunathamini bungo kuliko karafuu zetu kutokana na hali halisi ilivyokuwa. Lakini sasa karafuu ni mali na sidhani kama kuna mtu sasa atasema bora bungo kuliko karafuu. Kwa hivyo, mimi naipongeza sana serikali na hii inalenga zaidi kwenye huu uhamasishaji wa uendelezaji na usarifu wa hili zao la karafuu, kwa sababu nina hakika kama kuna mashamba ya mikarafuu yaliyokuwa porini sasa wenyewe wataitafuta na watailimia.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe pongezi vile vile kwa serikali kwa kuamua kuliboresha Shirika hili la Biashara, shirika hili ni muhimu sana na umuhimu wake zaidi unakuja kwa sababu ndio shirika pekee hapa Zanzibar linaloshughulikia mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, huko tunakotoka kwa kweli lilikuwa likisuasua sana hili shirika mpaka tukafika pahali tunajiuliza je liwepo au lisiwepo. Lakini nashukuru serikali wameona umuhimu wake, na leo ndio tunalipa meno hivi, kwa hiyo ni jambo jema sana hili.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nasoma huu mswada sana wenzangu wengi wamesema kama kuna hii marufuku ya kuondoa karafuu pahali pamoja na kuzipeleka pahali pengine kwamba inaleta usumbufu kwa wakulima wa karafuu. Bahati mbaya sikuona lakini inawezekana nimeangalia kwa upeo kabisa, lakini kama ndani ya sheria hii mna kitu hiki basi nafikiri sio kizuri, sio kizuri kwa sababu kitasababisha usumbufu mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema mimi nina uzoefu mkubwa sana wa karafuu. Sisi kule Pemba wale watu wanaokaa Mashariki ya Kisiwa cha Pemba kule mkarafuu hauoti kule, lakini mababu zetu wote walielekea upande wa jua linakotulia na kule ndiko walikokwenda kupanda mikarafuu. Kwa hivyo, mashamba ya mikarafuu yako

Magharibi ya Kisiwa cha Pemba lakini wengi wa wamiliki wa mashamba yale wako Mashariki wa Kisiwa cha Pemba. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tulivyozoea msimu ukifika tunakwenda kule Magharibi tunachuma karafuu, lakini hatimae tunazisafirisha kutoka kule tunazipeleka huo ukanda wa Mashariki kwa kuchambua na kuzianika. Tulikuwa tukifanya hivyo kwa sababu kule ndio kwetu

Lakini (b) ukanda wa mashariki ndio ukanda ambao hauna mvua nyingi, mara nyingi jua likuwa linachapuka ukilinganisha na ukanda wa magharibi ambako kuna karafuu nyingi. Mara nyingi inatokea mwaka ambao karafuu zinazaliwa sana ndio mwaka ambao mvua zinanyesha sana. Kwa hivyo, ukizirundika karafuu kule zitaoza na matokeo yake utapata mpeta. Sasa tulikuwa na utamaduni huo wa muda mrefu, tukisafirisha karafuu toka siku hizo hatuna usafiri wa magari tulikuwa tunachukua kwa punda tukizipeleka mashariki tukachambua, tukaanika, tukapata karafuu zenye *grade* nzuri.

Sasa ukija ukisema unazuia utaratibu huo maana yake utatusumbua kweli kweli. Nasema sijaona hicho kifungu humu, lakini wenzangu wengi wamesemea habari hii. Sasa kwa vile wamesemea inawezekana labda kuna kanuni au jambo gani, lakini mimi nafikiri utaratibu huu serikali ingetafuta namna nyengine ya kudhibiti magendo ya karafuu lakini hii wawaachie wananchi wahamishe karafuu zao mbichi kutoka kule mikarafuuni na kuzipeleka ukanda wa mashariki kwa ajili ya kuzishughulikia.

Jambo jengine katika mambo ya jumla ambayo nilisema niseme ni kwamba shirika hili pamoja na wizara na ikiwezekana hata kama watashirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu ni vizuri sana waangalie barabara zinazokwenda katika maeneo yenye mikarafuu mingi. Kuna tatizo kubwa zile *feeder road* ambazo zinakwenda kwenye mashamba ya mikarafuu ni mbovu na zinasumbua watu sana.

Nitatoa mfano pale Ngomeni, nafikiri wanaopajua Ngomeni na hata Mhe. Waziri nafikiri anapajua, kwa ile kusini ya Kisiwa cha Pemba sasa hivi Ngomeni ni eneo moja lenye mikarafuu iliyokuwa bado ni makini na mingi mno. Kwa karibu asilimia 40 karafuu za kule kusini sasa hivi zinatoka pale Ngomeni, pana kijipande cha barabara hakizidi kilomita mbili.

Hivi ninavyokwambia Mhe. Naibu Spika, hivi sasa haipitiki hiyo barabara, kwa sababu mvua imenyesha na ni msimu wa karafuu sasa watu wanahangaika kubeba magunia ya karafuu kupeleka barabarani. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri suala hili pamoja na shirika lake walione kile kipande wakitengeneze. Na sio kile tu, na mwengine pia zimo sehemu kama hizo. Kwa hivyo, kuboresha miundombinu ni miongoni mwa kazi za shirika nimeona humu ni kutoa huduma, kusaidia vifaa na mambo mengine basi na hii miundombinu ya barabara ni jambo moja muhimu sana. Naomba sana barabara ile ya Ngomeni iangaliwe *special* kuna karafuu nyingi sana kule Mhe. Naibu Spika.

Nafikiri baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, mimi niingie sasa kwenye vifungu na nataka nianze na kifungu cha sita (6). Ukisoma kifungu hiki cha 6(1)(a) pana maelezo pale yaani malengo ya shirika yatakuwa ni kutia nguvu na kuhamasisha ufanisi, uzalishaji bora, usarifu, kukuza thamani, mfumo unaofaa wa usambazaji na mfumo au utiaji

thamani na masoko ya karafuu na mazao mengine ya kilimo. Sasa hoja yangu imekuja hapa na mazao mengine ya kilimo.

Mazao mengine ya kilimo ni neno la jumla sana, maana yake mazao mengine ya kilimo ni maembe, nyanya, ndizi, mwani, ni mambo mengi kwa kweli hata mchicha ni mazao ya kilimo. Sasa ukishasema shirika hili unalibebesha mzigo wa mazao mengine ya kilimo maana yake sasa tunarudi kule kule tulikotoka, mimi nilidhani tunaunda hili shirika ili lipate nafasi ya kutosha na meno ya kushughulikia zao la karafuu, lakini ukishalibebesha mzigo wa mazao mengine ya kilimo ambayo ni mengi kweli kweli sasa utalinyima muda na hata uwezo wa kushughulikia zao la karafuu. Hii mimi nilidhani imeandikwa mara moja lakini imerudiwa rudiwa takriban vifungu vingi sana. Hata ukiangalia kifungu cha 6(2) limerudiwa kuna a, b, c, d, e, mote kuna mazao mengine ya kilimo, mazao mengine ya kilimo.

Ukija kifungu cha 7 kwenye kazi za shirika mazao mengine ya kilimo yanajirudia kama kwamba inakuwa linatiliwa nguvu vile. Sasa kwa mawazo yangu mimi nadhani si vyema, Shirila la *ZSTC* kulibebesha na mzigo mwengine.

Mhe. Naibu Spika, nimeona kifungu nafikiri cha 26 kwamba waziri anaweza kwa kutoa tangazo katika Gazeti Rasmi la Serikali kutoa orodha ya mazao mengine ya kilimo kwa madhumuni ya sheria hii. Sasa hii inaweza ikavua yale niliyoyasema kuwa yatakuwa yote ya kilimo, lakini hata wakiteuwa mengine matatu au yasizidi matatu bado ni mzigo kwa shirika.

Zamani Shirika la *ZSTC* lilikuwa likishughulikia karafuu na nazi, sasa hivi nazi hatuna tena za kutosha kwa sababu ya utalii. Lakini mimi nilikuwa nadhani shirika hili lipewe nafasi ya kushughulikia karafuu, karafuu zinachangamoto nyingi sana. Hivi sasa nahisi shirika liwe na wataalamu wa kutosha kwa sababu mikarafuu karibu asilimia 50 tayari imeshakufa na ni zao ambalo tunalitegemea sana kwa uchumi wan chi yetu. Sasa tuwe na wataalamu wa kushughulikia kwa nini mikarafuu imekufa, tufanye nini? Kuna maradhi ya mikarafuu yametokea au kuna upungufu wa kitu gani katika ardhi yetu.

Tumeambiwa humu kuna utafiti umefanywa lakini bado hatujaambiwa huo utafiti hatujui sisi walichogundua ni kitu gani. Sasa nilikuwa nahisi shirika hili liachiwe kazi hiyo ya kushughulikia karafuu, kufanya utafiti, na mambo mengine, mmoja akasema tupate na machotara ya mikarafuu. Mimi sidhani kama ni jambo zuri kwa sababu uzoefu wangu nilionao siku zote ukiwa na mnazi chotara maisha yake mafupi, ukiwa na mchungwa chotara maisha yake mafupi na ukiwa na mwembe chotara hivyo hivyo. Sasa mimi siungani kusema kwamba tuboreshe mbegu ya mikarafuu sasa tuwe na mikarafuu chotara zitakuwa kama zile karafuu za Indonesia ambazo thamani yake ni ndogo. Lakini kuna haja ya kuimarisha na kujua matatizo ya mkarafuu kwa nini unakufa.

Mhe. Naibu Spika, labda niangalie kifungu cha 7(2)(d). kifungu hiki nimegundua kina tatizo kidogo na kifungu cha 9(1)(a) naomba nikisome kidogo kinavyosema na hizi ni katika kazi za shirika. Moja katika kazi za shirika ukiangalia (d) hapo ni kuingia katika makubaliano na wakulima, wasarifu, wauzaji, waagiziaji na wasafirishaji maalum

walioteuliwa. Sasa hiki kifungu kinatoa fursa kumbe kuna wauzaji wengine wa karafuu. Lakini ukisoma kifungu cha 9(1)(a) kinasomeka kwamba, yaani huo sasa ni uwezo wa shirika. 'kuwa muuzani yaani shirika katika kutekeleza kazi zake chini ya sheria hii itakuwa na uwezo wa (a) kuwa muuzaji na msafirishaji pekee wa karafuu na mazao yatokanayo na karafuu'.

Sasa kifungu hiki ni shirika pekee lenye uwezo wa kuuza karafuu, lakini ukija kwenye kifungu cha 7(2) kinatoa mwanya kuwe na mtu mwengine japo kuwa idhini ya shirika, lakini naona ni *contradiction* ya sheria hii. Sasa nafikiri si tatizo kubwa lakini wanasheria watafute lugha nzuri zaidi ya kutuwekea sawa.

Mwisho niangalie kifungu cha 22 kuna makosa na adhabu pale. Kifungu hiki kinasema, "Mtu yeyote ambaye bila ya kibali cha shirika atanunua karafuu au mazao mengine ya kilimo na kilichonishitua zaidi ni hii au mazao mengine ya kilimo, sasa mtu huyo atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni kumi au kifungo kwa muda usiozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili ya faini na kifungo. Sina tatizo mimi mtu akikamatwa ananunua karafuu kwa sababu tunataka kukomesha yale magendo ya karafuu. Lakini ukishasema na mazao mengine ya kilimo hivyo Mhe. Naibu Spika, mtu akikamatwa ananunua embe Muyuni kule Muyuni ndio apewe adhabu hii? Au ananunua matenga ya tungule apewe adhabu hii?

Mimi nafikiri na ndio pale nilipoangalia ile mantiki yangu ya kusema hili shirika liachiwe kazi ya karafuu haya mazao mengine yaachwe kule kule kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili. Lakini hii ni sheria na sisi hapa tunatunga sheria sasa sheria hivi ndivyo inavyosema. Kwa hivyo, siku moja mtu anaweza akamkamata mtu kanunua embe muyuni anakuja nazo sokoni Mwanakwerekwe akampeleka mahakamani kavunja sheria hii, jaji akaangalia kweli kavunja sheria hii akamfunga miaka kumi. Kwa kweli mimi sioni kama itakuwa tunafanya jambo makini hapa. Sasa mimi nadhani pamoja na kifungu cha 26 kumpa uwezo waziri kuandaa orodha ya mazao mengine lakini bado nahisi shirika la *ZSTC* tuliachie karafuu peke yake, kwa kuwa nazi hazipo tena basi iwe kazi yao ni kushughulikia karafuu tu na hapo ndipo tutakapopata ufanisi wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo nina matumaini kwamba waziri atazingatia hii hoja na kuboresha boresha humo ambamo tumetoa mawazo yetu na mimi sina pingamizi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha kikao naomba niseme mambo matatu. Jambo la kwanza naomba niwatambulishe tuna mgeni Mhe. Balozi Moh'd Ramia, Mshauri wa Rais kuhusu Ushirikiano wa Kimataifa naomba asimame muweze kumtambua.

Jambo la pili nawaambia waheshimiwa muda uliobakia ni mdogo tumpe fursa Mhe. Waziri ili kesho aje na majumuisho mazuri, tumpe nafasi akakae na wataalamu wake, baada ya kipindi cha maswali tumwite afanye majumuisho na tuupitishe mswada.

Jambo la tatu na la mwisho niwashukuru wachangiaji wote wa tangu awamu ya asubuhi na hii ya jioni kwa ushirikiano mkubwa mliotupa. Baada ya hayo natamka kuahirisha kikao hiki hadi kesho saa tatu za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 18/10/2011 saa 3:00 asubuhi)